**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA MABADILIKO YA KATIBA**

# RANDAMA YA RASIMU YA KATIBA

**FEBRUARI, 2014**

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ........................................ i
**UTANGULIZI** ........................................ xii
**UTANGULIZI WA RASIMU YA KATIBA** ........................................ 2
**SURA YA KWANZA** ........................................ 3
**SEHEMU YA KWANZA** ........................................ 3
Ibara ya 1: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ........................................ 3
Ibara ya 2: Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ........................................ 6
Ibara ya 3: Alama na Sikukuu za Taifa ........................................ 8
Ibara ya 4: Lugha ya Taifa na Lugha za Alama ........................................ 9
Ibara ya 5: Tunu za Taifa ........................................ 10
Ibara ya 6: Mamlaka ya Wananchi, Utii na Hifadhi ya Katiba ........................................ 11
Ibara ya 7: Watu na Serikali ........................................ 11
Ibara ya 8: Ukuu na Utii wa Katiba ........................................ 12
Ibara ya 9: Hifadhi ya Utawala wa Katiba ........................................ 13
**SURA YA PILI** ........................................ 14
Ibara ya 10: Malengo Makuu ........................................ 14
Ibara ya 11: Utekelezaji wa Malengo ya Taifa ........................................ 15
Ibara ya 12: Sera ya Mambo ya Nje ........................................ 16
**SURA YA TATU** ........................................ 17
**SEHEMU YA KWANZA** ........................................ 17
Ibara ya 13: Dhamana ya Uongozi wa Umma ........................................ 17
Ibara ya 14: Kanuni za Uongozi wa Umma ........................................ 18
Ibara ya 15: Zawadi katika Utumishi wa Umma ........................................ 19
Ibara ya 16: Akaunti Nje ya Nchi na Mikopo ........................................ 20
Ibara ya 17: Wajibu wa Kutangaza Mali na Madeni ........................................ 20
Ibara ya 18: Mgongano wa Maslahi ........................................ 21
Ibara ya 19: Matumizi ya Mali ya Umma ........................................ 22
Ibara ya 20: Utekelezaji wa Masharti ya Maadili ........................................ 22
Ibara ya 21: Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma ........................................ 23
Ibara ya 22: Marufuku ya Baadhi ya Vitendo ........................................ 23

**SURA YA NNE** ....................................................................................................25
**SEHEMU YA KWANZA** ....................................................................................25
Ibara ya 23: Uhuru, Utu, Usawa wa Binadamu ..............................................25
Ibara ya 24: Haki ya Kuishi ..........................................................................25
Ibara ya 25: Marufuku ya Ubaguzi .................................................................26
Ibara ya 26: Haki ya Kutokuwa Mtumwa ........................................................26
Ibara ya 27: Uhuru wa Mtu Binafsi .................................................................27
Ibara ya 28: Haki ya Faragha na Usalama wa Mtu ..........................................27
Ibara ya 29: Uhuru wa Kwenda Mtu Anakotaka ..............................................28
Ibara ya 30: Uhuru wa Maoni .......................................................................28
Ibara ya 31: Uhuru wa Habari na Vyombo vya Habari ......................................29
Ibara ya 32: Uhuru wa Imani ya Dini ..............................................................29
Ibara ya 33: Uhuru wa Mtu Kujumuika na Kushirikiana na Wengine ...................30
Ibara ya 34: Uhuru wa Kushiriki Shughuli za Umma .........................................31
Ibara ya 35: Haki ya Kufanya Kazi ..................................................................31
Ibara ya 36: Haki za Wafanyakazi na Waajiri ...................................................31
Ibara ya 37: Haki ya Kumiliki Mali ..................................................................32
Ibara ya 38: Haki ya Uraia .............................................................................32
Ibara ya 39: Haki ya Mtuhumiwa na Mfungwa ..................................................33
Ibara ya 40: Haki ya Watu Walio Chini ya Ulinzi ..............................................33
Ibara ya 41: Uhuru na Haki ya Mazingira Safi na Salama ..................................34
Ibara ya 42: Haki ya Elimu na Kujifunza ..........................................................34
Ibara ya 43: Haki ya Mtoto .............................................................................35
Ibara ya 44: Haki na Wajibu wa Vijana ............................................................36
Ibara ya 45: Haki za Watu Wenye Ulemavu ......................................................36
Ibara ya 46: Makundi Madogo Madogo katika Jamii ...........................................37
Ibara ya 47: Haki za Wanawake ......................................................................38
Ibara ya 48: Haki za Wazee .............................................................................39
SEHEMU YA PILI ..............................................................................................40
Ibara ya 49: Wajibu wa Raia ............................................................................40
Ibara ya 50: Wajibu wa Kushiriki Kazi ...............................................................40
Ibara ya 51: Ulinzi wa Mali ya Umma ...............................................................41

Ibara ya 52: Haki na Wajibu Muhimu ........................................................................41
Ibara ya 53: Hifadhi ya Haki za Binadamu ..................................................................42
Ibara ya 54: Usimamizi wa Haki za Binadamu .............................................................43
Ibara ya 55: Mipaka ya Haki za Binadamu ..................................................................43
Ibara ya 56: Uraia wa Jamhuri ya Muungano ..............................................................45
Ibara ya 57: Uraia wa Kuzaliwa ....................................................................................45
Ibara ya 58: Uraia wa Kuandikishwa ............................................................................46
Ibara ya 59: Hadhi ya Watu wenye Asili au Nasaba ya Tanzania ....................................46
**SURA YA SITA** ........................................................................................................48
Ibara ya 60 Muundo wa Muungano ...........................................................................48
Ibara ya 61: Vyombo vya Utendaji vya Jamhuri ya Muungano. .......................................55
Ibara ya 62: Mamlaka ya Serikali ya Muungano............................................................55
Ibara ya 63: Mambo ya Muungano...............................................................................56
Ibara ya 64: Nchi Washirika ........................................................................................58
Ibara ya 65: Mamlaka ya Nchi Washirika .....................................................................58
Ibara ya 66: Mahusiano kati ya Nchi Washirika ............................................................60
Ibara ya 67: Mawaziri Wakaazi ...................................................................................61
Ibara ya 68: Mamlaka ya Wananchi .............................................................................61
Ibara ya 69: Wajibu wa Kuulinda Muungano ................................................................62
**SURA YA SABA** .......................................................................................................64
**SEHEMU YA KWANZA** ..................................................................................64
Ibara ya 70: Serikali ya Jamhuri ya Muungano .............................................................64
Ibara ya 71: Rais wa Jamhuri ya Muungano.................................................................65
Ibara ya 72: Madaraka na Mjukumu ya Rais ................................................................65
Ibara ya 73: Utekelezaji wa Madaraka ya Rais..............................................................66
Ibara ya 74: Rais Kuzingatia Ushauri ...........................................................................67
Ibara ya 75: Rais Kushindwa Kumudu Majukumu Yake ...............................................68
Ibara ya 76: Utaratibu wa Kujaza Nafasi ya Rais Kabla ya Kumaliza Muda Wake .............69
Ibara ya 77: Utekelezaji wa Majukumu ya Rais Akiwa Hayupo .......................................69
Ibara ya 78: Uchaguzi wa Rais.....................................................................................70
Ibara ya 79: Sifa za Rais .............................................................................................71
Ibara ya 80: Utaratibu wa Uchaguzi wa Rais ................................................................71

Ibara ya 81: Malalamiko Kuhusu Uhalali wa Uchaguzi wa Rais ........................................72
Ibara ya 82: Kiapo cha Rais na Muda wa Kushika Madaraka ...........................................73
Ibara ya 83: Haki ya Kuchaguliwa Tena ..........................................................................74
Ibara ya 84: Madaraka ya Kutangaza Vita .......................................................................75
Ibara ya 85: Madaraka ya Rais Kutangaza Hali ya Hatari. ...............................................76
Ibara ya 86: Mamlaka ya Kutoa Msamaha ......................................................................76
Ibara ya 87: Kinga ya Mashtaka Dhidi ya Rais ................................................................77
Ibara ya 88: Bunge Kumshtaki Rais.................................................................................78
Ibara ya 89: Maslahi ya Rais...........................................................................................79
Ibara ya 90: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ...............................................79
Ibara ya 91: Upatikanaji wa Makamu wa Rais ................................................................80
Ibara ya 92: Sifa za Makamu wa Rais .............................................................................80
Ibara ya 93: Kiapo cha Makamu wa Rais ........................................................................81
Ibara ya 94: Wakati wa Makamu wa Rais Kushika Madaraka ..........................................81
Ibara ya 95: Bunge Kumshtaki Makamu wa Rais. ...........................................................82
Ibara ya 96: Upatikanaji wa Makamu wa Rais Wakati Nafasi Hiyo Inapokuwa Wazi ..........82
**SEHEMU YA PILI** ............................................................................................84
Ibara ya 97: Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri ...............................................................84
Ibara ya 98: Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri.......................................................84
Ibara ya 99: Waziri Mwandamizi ....................................................................................85
Ibara ya 100: Kazi na Mamlaka ya Waziri Mwandamizi...................................................85
Ibara ya 101: Sifa za Mawaziri na Naibu Mawaziri .........................................................86
Ibara ya 102: Kiapo, Muda na Masharti ya Kazi ya Waziri na Naibu Mawaziri ...................86
Ibara ya 103: Utekelezaji wa Shughuli za Serikali Bungeni .............................................87
Ibara ya 104: Mwanasheria Mkuu wa Serikali.................................................................88
Ibara ya 105: Katibu Mkuu Kiongozi ..............................................................................88
Ibara ya 106: Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu .............................................89
Ibara ya 107: Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu .........................................................89
Ibara ya 108: Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ...........................................................90
**SURA YA NANE** ...........................................................................................91
Ibara ya 109: Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali .................................................91
Ibara ya 110: Malengo ya Tume ......................................................................................92

Ibara ya 111: Majukumu ya Tume ....................92
Ibara ya 112: Sekretarieti ya Tume ....................93
**SURA YA TISA** ....................95
**SEHEMU YA KWANZA** ....................95
Ibara ya 113: Kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano ....................95
Ibara ya 114: Muda wa Bunge ....................95
Ibara ya 115: Madaraka ya Bunge ....................96
Ibara ya 116: Mipaka ya Bunge Katika Kutumia Madaraka Yake....................96
Ibara ya 117: Madaraka ya Bunge Kutunga Sheria ....................97
Ibara ya 118: Utaratibu wa Kubadilisha Katiba ....................97
Ibara ya 119: Utaratibu wa Kubadilisha Masharti Mahsusi ....................98
Ibara ya 120: Utaratibu wa Kutunga Sheria ....................98
Ibara ya 121: Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo ya Fedha ....................99
Ibara ya 122: Madaraka ya Mkuu wa Nchi Kuhusu Muswada wa Sheria ....................99
Ibara ya 123: Kupitishwa kwa Hoja za Serikali ....................100
Ibara ya 124: Uchaguzi wa Wabunge ....................101
Ibara ya 125: Sifa za Kuchaguliwa Kuwa Mbunge ....................101
Ibara ya 126: Utaratibu wa Uchaguzi wa Wabunge....................102
Ibara ya 127: Kiapo na Masharti ya Kazi ya Bunge ....................103
Ibara ya 128: Kupoteza Sifa za Ubunge ....................103
Ibara ya 129: Haki ya Wapiga Kura Kumwajibisha Mbunge ....................104
Ibara ya 130: Uamuzi wa Suala Kama Mtu ni Mbunge....................105
Ibara ya 131: Tamko Rasmi la Wabunge Kuhusu Maadili ya Uongozi....................105
**SEHEMU YA TATU** ....................106
Ibara ya 132: Spika na Mamlaka ya Spika ....................106
Ibara ya 133: Ukomo wa Spika ....................106
Ibara ya 134: Naibu Spika ....................107
Ibara ya 135: Sifa za Mtu Kuchaguliwa Kuwa Spika au Naibu Spika....................107
Ibara ya 136: Utaratibu wa Uchaguzi na Kiapo cha Spika na Naibu Spika ....................108
Ibara ya 137: Katibu wa Bunge....................108
Ibara ya 138: Sekretarieti ya Bunge ....................109

**SEHEMU YA NNE** .......... 109
Ibara ya 139: Kanuni za Kudumu za Bunge .......... 109
Ibara ya 140: Rais Kulihutubia Bunge .......... 110
Ibara ya 141: Mikutano ya Bunge .......... 110
Ibara ya 142: Uongozi na Vikao vya Bunge .......... 111
Ibara ya 143: Akidi ya Vikao vya Bunge .......... 111
Ibara ya 144: Kamati za Bunge .......... 111
**SEHEMU YA TANO** .......... 112
Ibara ya 145: Uhuru wa Majadiliano .......... 112
Ibara ya 146: Mipaka ya Majadiliano Bungeni .......... 112
**SEHEMU YA SITA** .......... 114
Ibara ya 147: Tume ya Utumishi wa Bunge .......... 114
Ibara ya 148: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge .......... 114
Ibara ya 149: Mfuko wa Bunge .......... 115
**SURA YA KUMI** .......... 116
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 116
Ibara ya 150: Kuanzishwa kwa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano .......... 116
Ibara ya 151: Misingi ya Utoaji Haki .......... 116
Ibara ya 152: Uhuru wa Mahakama .......... 117
**SEHEMU YA PILI** .......... 118
**MUUNDO WA MAHAKAMA** .......... 118
Ibara ya 153: Muundo wa Mahakama .......... 118
Ibara ya 154: Mahakama ya Juu .......... 118
Ibara ya 155: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Juu .......... 119
Ibara ya 156: Mamlaka ya Mahakama ya Juu .......... 119
Ibara ya 157: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu .......... 120
Ibara ya 158: Uteuzi wa Jaji Mkuu .......... 120
Ibara ya 159: Uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu .......... 121
Ibara ya 160: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu .......... 122
Ibara ya 161: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu .......... 122
Ibara ya 162: Muda wa Kuwa Madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Juu. .......... 122

Ibara ya 163: Utaratibu wa Kukaimu Nafasi ya Jaji Mkuu ............................................123
Ibara ya 164: Utaratibu wa Kushughulikia Nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu ......123
Ibara ya 165: Mahakama ya Rufani......................................................................124
Ibara ya 166: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Rufani..............................................125
Ibara ya 167: Mamlaka ya Mahakama ya Rufani........................................................125
Ibara ya 168: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani..........................................125
Ibara ya 169: Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani .....................................126
Ibara ya 170: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani .........................126
Ibara ya 171: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani.............................................127
Ibara ya 172: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani.............................................127
Ibara ya 173: Muda wa Kuwa Madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani ..........................................................................127
Ibara ya 174: Utaratibu wa Kukaimu Nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani ......128
Ibara ya 175: Utaratibu wa Kushughulikia Nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani ..128
Ibara ya 176: Msajili Mkuu wa Mahakama ..................................................................129
Ibara ya 177: Majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama .............................................129
Ibara ya 178: Mtendaji Mkuu wa Mahakama...............................................................129
Ibara ya 179: Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama..........................................130
**SEHEMU YA TATU**..............................................................................................131
Ibara ya 180: Tume ya Utumishi wa Mahakama.........................................................131
Ibara ya 181: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama.....................................131
Ibara ya 182: Uanachama Katika Vyama vya Siasa....................................................132
Ibara ya 183: Mfuko wa Mahakama .........................................................................132
**SEHEMU YA TATU**..............................................................................................134
**SURA YA KUMI NA MOJA** ....................................................................................134
Ibara ya 184: Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma...................................................134
Ibara ya 185: Ajira na Uteuzi wa Viongozi Katika Taasisi za Serikali .............................134
Ibara ya 186: Tume ya Utumishi wa Umma ...............................................................135
Ibara ya 187: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma................................................135
Ibara ya 188: Mamlaka ya Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma.........................136

**SURA YA KUMI NA MBILI** .......... 137
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 137
Ibara ya 189: Ushiriki Katika Uchaguzi na Kura ya Maoni .......... 137
SEHEMU YA PILI .......... 138
Ibara ya 190: Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi .......... 138
Ibara ya 191: Kamati ya Uteuzi .......... 138
Ibara ya 192: Ukomo wa Kushika Nafasi ya Madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi .......... 139
Ibara ya 193: Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi .......... 139
Ibara ya 194: Malalamiko kuhusu Uchaguzi .......... 140
Ibara ya 195: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi .......... 140
Ibara ya 196: Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi .......... 141
**SEHEMU YA TATU** .......... 142
Ibara ya 197: Usajili wa Vyama vya Siasa .......... 142
Ibara ya 198: Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa .......... 142
Ibara ya 199: Wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa .......... 143
**SURA YA KUMI NA TATU** .......... 144
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 144
Ibara ya 200: Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji .......... 144
Ibara ya 201: Uteuzi na Sifa za Wajumbe .......... 145
Ibara ya 202: Kamati Maalum ya Uteuzi .......... 145
Ibara ya 203: Majukumu ya Jumla ya Tume .......... 145
Ibara ya 204: Muda wa Kukaa Madarakani kwa Mjumbe wa Tume .......... 146
Ibara ya 205: Kuondolewa Madarakani kwa Mjumbe wa Tume .......... 146
Ibara ya 206: Uhuru wa Tume .......... 147
Ibara ya 207: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali .......... 147
**SEHEMU YA PILI** .......... 149
Ibara ya 208: Tume ya Haki za Binadamu .......... 149
Ibara ya 209: Kamati ya Uteuzi .......... 149
Ibara ya 210: Kazi na Majukumu ya Tume .......... 150
Ibara ya 211: Muda wa kukaa madarakani kwa Kamishna wa Tume .......... 150
Ibara ya 212: Kuondolewa Madarakani kwa Kamishna wa Tume .......... 151
Ibara ya 213: Uhuru wa Tume .......... 151

Ibara ya 214: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali ....................................................152

**SEHEMU YA TATU** ....................................................................................153

Ibara ya 215: Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.....................153

Ibara ya 216: Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .........................153

Ibara ya 217: Kazi na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ....154

Ibara ya 218: Muda wa Kukaa Madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ........................................................................................................154

Ibara ya 219: Kuondolewa Madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ........................................................................................................155

Ibara ya 220: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali ....................................................155

**SURA YA KUMI NA NNE** ........................................................................................157

Ibara ya 221: Mfuko Mkuu wa Hazin**a** .........................................................................157

Ibara ya 222: Masharti ya Kutoa Fedha za Matumizi Katika Mfuko Mkuu wa Hazina........157

Ibara ya 223: Utaratibu wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Zilizomo Katika Mfuko Mkuu wa Hazina.......................................................................................................158

Ibara ya 224: Utaratibu wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali Kuanza Kutumika .........................................................................158

Ibara ya 225: Mfuko wa Matumizi ya Dharura ...........................................................159

Ibara ya 226: Mishahara ya Baadhi ya Watumishi Kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ......................................................................................................................159

Ibara ya 227: Deni la Taifa.........................................................................................160

Ibara ya 228: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Kukopa ............................160

Ibara ya 229: Mamlaka ya Serikali za Nchi Washirika Kukopa .......................................161

Ibara ya 230: Masharti ya Kutoza Kodi .......................................................................161

Ibara ya 231: Vyanzo vya Mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano .......................161

Ibara ya 232: Ununuzi wa Umma.................................................................................162

Ibara ya 233: Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano .....................................................163

Ibara ya 234: Benki za Serikali za Nchi Washirika ......................................................163

**SURA YA KUMI NA TANO** ........................................................................................165

Ibara ya 235: Usalama wa Taifa .................................................................................165

Ibara ya 236: Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa ...............................................165

Ibara ya 237: Kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa ...........................166

Ibara ya 238: Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa ...............................167

Ibara ya 239: Kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ........................167
Ibara ya 240: Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ..................................................168
Ibara ya 241: Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu ............................................................168
Ibara ya 242: Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania .................169
Ibara ya 243: Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano..................................................169
Ibara ya 244: Misingi ya Utendaji wa Jeshi la Polisi.....................................................169
Ibara ya 245: Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi.........................................................170
Ibara ya 246: Uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi .........................................................170
Ibara ya 247: Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi......................................................171
Ibara ya 248: Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa...........................................171
Ibara ya 249: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa .............................172
Ibara ya 250: Usalama katika Nchi Washirika.............................................................172
**SURA YA KUMI NA SITA**.........................................................................................174
Ibara ya 251: Utaratibu wa kujiuzulu Katika Utumishi wa Umma..................................174
Ibara ya 252: Masharti Kuhusu Kukabidhi Madaraka ...................................................174
Ibara ya 253: Baadhi ya Watumishi wa Umma Kutoshika Madaraka .............................175
Ibara ya 254: Ufafanuzi ...........................................................................................176
Ibara ya 255: Jina la Katiba na Kuanza Kutumika .......................................................176
Ibara ya 256: Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya 2 .............................................................................................................176
**SURA YA KUMI NA SABA**........................................................................................178
**SEHEMU YA KWANZA** ...........................................................................................178
Ibara ya 257: Matumizi ya Baadhi ya Masharti ya Katiba, Sura ya 2 .............................178
**SEHEMU YA PILI**...................................................................................................178
Ibara ya 258: Kuendelea Kutumika Masharti ya Katiba................................................178
Ibara ya 259: Kuendelea Kutumika Sheria za Nchi......................................................179
Ibara ya 260: Kuendelea Kuwepo kwa Rais Madarakani .............................................181
Ibara ya 261: Kuendelea Kuwepo kwa Makamu wa Rais Madarakani............................181
Ibara ya 262: Kuendelea kwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri. ......................182
Ibara ya 263: Kuendelea kwa Watumishi wa Umma ...................................................182
Ibara ya 264: Kuendelea kwa Ubunge na Uongozi wa Bunge.......................................183
Ibara ya 265: Kuvunjwa kwa Bunge ..........................................................................183

Ibara ya 266: Kuendelea kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ........................ 184
Ibara ya 267: Kuendelea kwa Mashauri Yaliyopo Mahakamani ..................................... 185
**MASHARTI YA MPITO** ........................................................................................ 185
Ibara ya 268: Muda wa Mpito ........................................................................... 185
Ibara ya 269: Utekelezaji wa Masharti ya Katiba Mpya ............................................... 186
Ibara ya 270: Kamati ya Kusimamia Muda wa Mpito. .................................................. 187
Ibara ya 271: Kufutwa kwa Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito ......................... 187
**KIAMBATISHO Na. 1:** MUUNDO WA MUUNGANO KATIKA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO YA MWAKA 1977 ........................................................................................ 188
**KIAMBATISHO Na. 2:** MUUNDO WA MUUNGANO KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO 189
**KIAMBATISHO Na. 3:** USIMAMIZI NA URATIBU WA MAMBO YA MUUNGANO NA YASIYO YA MUUNGANO KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO ................................. 190
**KIAMBATISHO Na. 4:** MUUNDO WA VYOMBO VYA KUTUNGA SHERIA KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI UA MUUNGANO WA TANZANIA ................................................................ 191
**KIAMBATISHO Na. 5:** MFUMO WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MUJIBU WA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO YA MWAKA 1997 NA KATIBA YA ZANZIBAR YA MWAKA 1984 ....................................................................... 192
**KIAMBATISHO Na. 6:** MUUNDO WA VYOMBO VYA UTOAJI HAKI KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA........................................................................ 193
**KIAMBATISHO NA.** 7: UTATUZI WA MIGOGORO KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO NA NCHI WASHIRIKA NA KATI YA NCHI ZA WASHIRIKA ZENYEWE ............................................................................................. 194
**KIAMBATISHO NA.8:** MISINGI YA UTENDAJI YA MUUNGANO WA SERIKALI TATU ..195

## UTANGULIZI

Randama hii imetayarishwa ili kutoa ufanunuzi wa Rasimu. Walengwa wakuu wa randama hii ni wa aina mbili. Kwanza imetayarishwa kuwasaidia Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba katika majadiliano yao Bungeni. Ni muhimu Wajumbe hao wawe na uelewa wa kutosha kuhusu misingi ya mapendekezo yaliyofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika Rasimu ya Pili.

Walengwa wa pili ni wananchi wenyewe. Rasimu imelenga kuwasaidia wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika mijadala itakayojitokeza na kuendelea wakati wa majadiliano katika Bunge Maalum na hata nje ya Bunge na baada ya hapo kuelekea

Kura ya Maoni. Ni muhimu kwamba Wajumbe wa Bunge Maalum na wananchi kwa jumla washiriki wakiwa na uelewa wa kina kuhusu Rasimu ya Pili na masuala ya katiba kwa ujumla.

Randama hii inawasilisha Rasimu Ibara kwa Ibara. Kila Ibara inawasilishwa katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni lile ambalo linaainisha maudhui ya Ibara husika kwa ufupi inavyowezekana. Eneo la pili linatoa madhumuni au malengo ya Ibara hiyo.

Madhumuni na Malengo ni ya aina mbili. Kuna malengo ya moja kwa moja yanayohusu matumizi ya katiba na sheria. Vile vile kuna malengo ya muda mrefu yanayohusu kujenga tabia na hatimaye utamaduni wa ukatiba.

Sehemu ya tatu katika mawasilisho haya inatoa uchambuzi na sababu ambazo ziliifanya Tume kufikia maamuzi ya kupendekeza kama ilivyofanya. Kuna sababu aina tano. Kwanza ni maoni ya wananchi. Pili ni uzoefu wa Tanzania kihistoria chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, 1977 na ile ya Zanzibar, 1984 kama zilivyorekebishwa mara kadhaa. Tatu, uzoefu wa nchi nyingine katika eneo husika la katiba.

Nne, taarifa za tafiti mbalimbali zilizofanywa na Tume, ikiwa ni pamoja na mapitio ya maeneo ambayo yalitajwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, na kutaka Tume iyazingaitie. Tano, wajibu wa Tanzania kufuata mikataba ya kimataifa iliisaidia Tume katika kufikia maamuzi yake.

Randama hii itasaidia kurahisisha uelewa wa Rasimu na kwamba siyo mbadala wa Rasimu kwa ukamilifu wake wala ripoti na nyaraka nyingine zinazoambatana na mawasilisho ambayo yanayofanywa na Tume.

Randama itakuwa ni kichocheo cha mijadala ya kina yenye lengo hatimaye kupatikana Katiba mpya ambayo ina mwafaka wa kitaifa na yenye ridhaa ya wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano.

## UTANGULIZI WA RASIMU YA KATIBA

### a. Maudhui ya Utangulizi

Maudhui ya utangulizi wa Katiba (*Preamble*) yamegawanyika katika maeneo makuu manne. Kwanza inaeleza aina ya nchi na jamii ambayo wananchi wa Tanzania wameamua kuijenga kuwa ni ile inayoheshimu na kuzingatia misingi ya utu, uhuru, haki, usawa, udugu, amani na mshikamano katika nyanja zote za maisha katika nyanja zote za maisha ya Watanzania.

Pili, utangulizi unasisitiza aina ya jamii inayoweza kutekeleza misingi hiyo kuwa ni ile yenye mfumo wa demokrasia na utawala bora yenye mihimili ya dola inayowajibika kwa wananchi inayolinda na kudumisha haki za binadamu na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa ukamilifu, inayoheshimu utawala wa sheria, kujitegemea na kuwa na nchi isiyofungamana na dini.

Tatu, utangulizi unasisitiza kuheshimu urithi wa waasisi wa Taifa na unaorodhesha mambo ambayo yatalindwa, kuimarishwa, kudumishwa na kukuzwa ukiwemo Muungano wa Tanzania, kujitegemea, utawala bora, ukuu wa mamlaka ya watu na utii wa mamlaka ya Katiba na uzalendo.

Nne, utangulizi unaeleza umuhimu wa kutunza mali ya umma, matumizi endelevu ya maliasili na kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kukuza amani, umoja, urafiki miongoni mwa watanzania na Afrika. Aidha, unasisitiza kupiga vita uharibifu na ubadhirifu wa mali za umma.

### b. Madhumuni na Lengo

Kuwa na utangulizi katika Katiba ni muhimu kwa sababu ndiyo mtima wa Katiba unaoonyesha dhamira ya kutungwa kwake na unaotoa msingi wa tafsiri ya jumla ya Katiba. Utangulizi unatoa taswira halisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watu wake, historia yao, matarajio yao, misingi na masuala muhimu ambayo wanataka kuyaendeleza katika jamii na kuyarithisha kizazi hadi kizazi.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu ya kuwa na utangulizi wa Katiba ni kuutambua kuwa ni sehemu muhimu ya Katiba ya nchi. Pia ni kuendeleza utaratibu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuwa na utangulizi katika Katiba zote ilizoziandika hata kabla ya uhuru. Aidha, ni uzoefu wa nchi nyingi duniani kuwa na utangulizi katika Katiba.

# SURA YA KWANZA

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## SEHEMU YA KWANZA

## JINA, MIPAKA, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA

### Ibara ya 1: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaeleza kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi na Shirikisho lenye mamlaka kamili ambalo limetokana na Muungano wa nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ambazo kabla ya Hati ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, zilikuwa nchi huru na Jamhuri.

Aidha, Rasimu ya Katiba imeweka bayana na kufafanua aina ya Muungano wa Tanzania kuwa ni shirikisho la kidemokrasia linalofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, usawa wa binadamu, kujitegemea, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na lisilofungamana na dini.

Hati ya Makubaliano ya Muungano iliyorejewa katika Ibara hii, ndiyo msingi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba hii, kwa kadri ilivyorekebishwa na itakavyorekebishwa, itakuwa ni mwendelezo wa Makubaliano hayo.

### b. Madhumuni na Lengo

Sababu ya kuweka Ibara hii ni kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuwepo, inaimarishwa na kudumishwa; na kuhuuisha Muungano. Aidha, lengo la Ibara hii ni kuainisha aina na hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni Muungano wa Shirikisho lenye Mamlaka Kamili (*Sovereign Federal State*).

Hatua hii ina lengo la kuimarisha Muungano kwa kuipa Mamlaka ya Kidola Jamhuri ya Muungano na kubainisha utambulisho, uwezo na mamlaka ya Nchi Washirika katika Muungano.

Vile vile, lengo la Ibara hii ni kuainisha mfumo wa utawala wa Jamhuri ya Muungano na kupanua misingi muhimu ya nchi ikilinganishwa na ilivyo katika Ibara 3 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoeleza kuwa, "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyo kuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa".

Lengo jingine ni kuonyesha kuwa Hati ya Muungano ya 1964 ndio chimbuko la Muungano wa Tanzania na kadri ambavyo imekuwa ikibadilika kwa haja na madhumuni ya kukidhi mabadiliko ya wakati na utekelezaji.

Pia, ni kwa madhumuni ya kuipa hadhi ya kikatiba Hati hiyo ya Muungano kwa kuihamisha kutoka kwenye Ibara ya 98 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Pili, Orodha ya Kwanza na badala yake kuingizwa ndani ya katiba kama ibara inayosimama yenyewe.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kifungu cha 9(2)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 kimeielekeza Tume katika kutekeleza masharti ya sheria kuongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya jamii ya kuhifadhi na kudumisha kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuondoa utata wa aina na muundo wa Muungano ambao umesababisha kuvunjwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Serikali zote mbili mara kadhaa.

Sababu nyingine ya kupendekeza aina hii ya Muungano ni kuhifadhi asili, taswira na hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jumuiya ya kimataifa kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Mkataba wa Montevideo wa mwaka 1933 unaohusu Haki na Majukumu ya Nchi (*Montevideo Convention on Rights and Duties of States*) "*the federal state shall constitute a sole person in the eyes of international law*" inayomaanisha nchi yenye muundo wa shirikisho katika sheria za kimataifa ni dola moja.

Kumekuwa na mijadala miongoni mwa Watanzania kuhusu aina ya Muungano uliopo Tanzania iwapo ni shirikisho au la. Katika medani ya kisiasa mjadala juu ya jambo hili ulijitokeza mwaka 1983 mpaka 1984 kwa uwazi na kwa nguvu wakati wa zoezi la wananchi kutoa maoni juu ya mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM juu ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, 1979.

Zoezi hilo lilidumu miezi tisa na lilikamilika kwa kufanyika kwa Mabadaliko ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1984 na kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984. Hali hiyo ilipewa jina la "Kuchafuka kwa Hali ya Hewa" na ilisababisha aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Aboud Jumbe Mwinyi, kujiuzulu.

Kwa mujibu wa Kumbukumbu za Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi katika Mkutano wa Tano, ambao ulikuwa maalum, uliofanyika Dodoma Januari 24-30, 1984, Mwalimu Nyerere alitamka kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiangalia kwa jicho la Zanzibar ni wa shirikisho lakini ukiangalia kutoka upande wa Tanzania Bara ni Serikali moja.

Mwalimu alikuwa akimjibu Makamu Mwenyekiti wa CCM, Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi aliyesema kuwa Muungano wa Tanzania umeunda Shirikisho (*Federation*) na sio Serikali moja (*Unitary State*).

Mfumo wa shirikisho unaopendekezwa katika Rasimu hii unaendeleza hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni Nchi na ni dola moja lenye mamlaka kamili yenye serikali tatu. Shirikisho hili linatokana na muungano wa hiari wa Tanganyika na Zanzibar ambazo zilikuwa Jamhuri zenye mamlaka kamili kabla ya kuungana tarehe 26 Aprili 1964.

Kwa kawaida nchi ambazo zimeingia katika muungano zinaweza kuchukua moja kati ya sura hizi tatu zifuatazo:

1. Muungano wa Serikali Moja (*Unitary State*);
2. Muungano wa Shirikisho (Federation); na
3. Muugano wa Mkataba (*Confederation*)

Kwa vyovyote vile, mfumo wa shirikisho unakuwepo pale ambapo nchi mbili au zaidi zimeungana na hazikuunda serikali moja. Kwa maana hiyo shirikisho (*Federation*) linamaanisha mfumo wa utawala wa nchi wenye sifa zifuatazo:

1. Kunakuwa na ngazi mbili za serikali zinazotawala eneo moja la nchi na raia wale wale; moja ikisimamia mambo ya muungano (shirikisho) na nyingine mambo yasiyo ya Muungano (yasiyo ya shirikisho);
2. Kila ngazi ya serikali, yaani ile ya shirikisho na ile ya nchi washirika inakuwa na mamlaka kamili na maeneo ya utendaji na uhakikisho wa kikatiba wa uhuru wa kutoingiliana baina ya serikali hizo katika maeneo waliyo na madaraka nayo bila ya kushauriana. Mfumo huu ni tofauti na ule wa dola moja lenye serikali moja (unitary state) ambapo serikali kuu inaweza kuamua kuzinyang'anya serikali za chini yake madaraka kadri inavyoona inafaa;
3. Katika muundo huu, serikali ya muungano ndiyo yenye mamlaka juu ya masuala yote yaliyokubaliwa kuwa ya muungano (shirikisho). Serikali za nchi washirika zinakuwa na mamlaka ya kikatiba ya kushughulikia mambo yasiyo ya muungano katika maeneo yao ya utawala; na
4. Katika muungano wa shirikisho mamlaka kuu ya kidola (*sovereign powers and functions*) yapo chini ya serikali ya shirikisho (muungano).

Ingawa katika mfumo huu wa muungano wa shirikisho kunakuwa na serikali zaidi ya moja kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya Mkataba wa Montevideo wa Haki na Majukumu ya Nchi (*Montevideo Convention on Rights and Duties of States*) katika sheria za kimataifa na mahusiano ya kimataifa nchi inayofuata mfumo wa muungano wa shirikisho huchukuliwa na kuhesabiwa kuwa nchi moja.

Sura ya shirikisho la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni nchi yenye mamlaka tatu na serikali tatu inajidhihirisha katika masharti yaliyomo katika Ibara za 61, 63, 64, 65, 66, 67, 70, 71, 72, 110, 111,117, 119, 156 na 235.

Miongoni mwa mifano ya nchi zinazofuata muundo wa muungano wa shirikisho ni nchi za Ethiopia, Marekani, Nigeria, Ujerumani, India na Brazil. Hata hivyo Muungano wa Tanzania ni tofauti na miungano ya shirikisho iliyotajwa kwa sababu ni wa hiari na usiotokana na ubeberu au ukoloni na ulihusisha nchi mbili zilizokuwa jamhuri kamili kabla ya kuungana. Kwa aina hii ya Muungano wa hiari huwezi kufuta kuwepo kwa utambulisho wa nchi washirika zinazounda au zilizounda Muungano.

**Ibara ya 2: Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutamka kuwa ni eneo lote la iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika ikijumuisha sehemu yake ya bahari na eneo lote la iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ikijumuisha sehemu yake ya bahari.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukamilifu na kuiweka Tanzania katika ramani ya kimataifa na kuweka bayana mipaka na nchi jirani.

Ibara hii pia inalenga kuhamasisha Watanzania kujenga tabia ya kutambua na kulinda mipaka ya nchi yao. Maelezo hayo yasomeke pamoja na Ibara za 49, 51 na 235 za Rasimu ya Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Umuhimu wa kubainisha eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuridhia kiu ya wananchi waliotaka kuwepo kwa ufafanuzi thabiti kuhusu eneo na mipaka ya nchi. Kufanya hivyo, kutatunza historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuondoa utata na hisia kwamba mipaka ya nchi hizi mbili inabadilika.

Baadhi ya nchi ambazo zimeweka mipaka yake katika katiba zao ni pamoja na Kenya, Msumbiji, Sudan ya Kusini na Ethiopia. Lakini pia nchi za Uganda na Siera Leone zimekwenda mbali zaidi kwa kutumia vipimo vya kisasa vya Global Positioning System (GPS) kuweka mipaka yao katika katiba za nchi.

Katika kuweka vifungu vya mipaka katika Katiba zao, nchi ya Msumbiji inayopakana na Tanzania Ibara ya 6 ya Katiba yake inatamka:

> *"1. The territory of the Republic of Mozambique is a single whole, indivisible and inalienable, comprising the entire land surface, maritime zone and air space delimited by the national boundaries."*
>
> *"2. The breadth, limits and legal order of Mozambique's territorial waters, the exclusive economic zone, the contiguous zone and seabed rights shall be fixed by law."*

Pia, sababu ya mapendekezo haya ni kubainisha mipaka ya Jamhuri ya Muungano inayotambulika na mikataba mbalimbali ya kimataifa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria za Bahari wa mwaka 1982 (*United Nations Law of the Sea Convention*) kama ulivyoainishwa katika sheria ya *Teritorial Sea Exclusive Economic Zone Act*, Sura ya 238 na *Deep Sea Fishing Authority Act*, Sura ya 389 ya Sheria za Tanzania.

Kwa undani zaidi, Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act*, Sura ya 238 inatamka katika Kifungu cha 3 kwamba:

*"The breadth of the Territorial Sea of the United Republic shall comprise those areas of the sea extending up to 12 nautical miles measured from the coastal low-water line as determined under Section 5 of this Act."*

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria hii, msingi wa kupima bahari ya Jamhuri ya Muungano umeelezewa kuwa ni:

*"The baseline from which the breadth of the Territorial Sea of the United Republic is measured shall be the low-water line along the coast of the United Republic including the coast of all islands , as marked on a large scale chart of map officially recognized by the Government of the United Republic."*

Kutokana na Sheria hii bahari yote ndani ya kilomita 12 za bahari inachukuliwa kuwa ni maji ya ndani na si ya kimataifa. Kifungu cha 4 kinaeleza kuwa:

*"The internal waters of the United Republic of Tanzania include any areas of the sea that are on the landward side of the baseline of the Territorial Sea of the United Republic."*

Sheria ya Deep Sea Fishing Authority Act, Sura ya 389 inabainisha katika Kifungu cha 2 kwamba:

*(1)"This Act shall apply to Tanzania Zanzibar as well as Mainland Tanzania.*

*(2)"The Act shall be construed as being in addition to and not in derogation of the Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act, 1989 and shall for all intents and purposes compliment that Act."*

Mikataba ya Kimataifa ya Mipaka ya Tanzania na Mataifa jirani ni kama ifuatavyo:

a) **Mpaka wa Tanzania na Burundi** [*Protocol between the Belgium and British governments relative to the Tanganyika-Ruanda-Urundi border (5 August 1924); Anglo-Belgium Agreement (2 November 1934)*].
b) **Mpaka wa Tanzania na Rwanda** [*Treaty between Belgium, Great Britain and Northern Ireland concerning the Boundary between Tanganyika and Ruanda-Urundi (22 November 1934)*].
c) **Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** *[Convention between German and Belgium (11 August 1910); Protocol signed by Great Britain and Belgium (5 August 1934)*].
d) **Mpaka wa Tanzania na Kenya *[***Agreement between Great Britain and German respecting Zanzibar, Heligoland and the Spheres of Influence of the two countries in Africa (1 July 1890); Agreement between Great Britain and German respecting Boundaries in East Africa from the mouth of Umba River to Lake Jipe and Kilimanjaro (25 July 1893); Protocol of Agreement between the British and German governments respecting the Jassin and Umba valley Boundary (14 February 1900); Draft Agreement respecting the Boundary between the British and German Territories in East Africa from mount Sabino to Lake Jipe (4 July 1914); British Mandate for East Africa (20 July 1922)]*.

e) **Mpaka wa Tanzania na Msumbiji** *[Declaration of Spheres of Influence between Portugal and German (30 December 1886); Anglo-Portuguese Treaty (11 June 1891)]*.

f) **Mpaka wa Tanzania na Uganda** [*Anglo-German Delimitation of Spheres of Influence in East Africa: Exchange of Notes (29 October -1 November 1886); Anglo-German Agreement (1 July 1890); Anglo-German Agreement (14 may 1910)]*.

g) **Mpaka wa Tanzania na Zambia** [*Agreement between Great Britain and Germany relative to the Boundary of the British and German spheres of interest between Lake Nyasa and Tanganyika (23 February 1901)];* na

h) **Mpaka wa Tanzania na Malawi** [*Anglo-German Agreements (1 July 1890 and 23 February 1901), na Protocol (11 November 1898).*

Serikali ya Tanzania (wakati huo "Tanganyika") iliridhia mikataba hii yote ya mipaka isipokuwa eneo la mpaka wake na Malawi katika Ziwa Nyasa.

**Ibara ya 3: Alama na Sikukuu za Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inataja alama za Taifa zinazoonyesha taswila mahsusi na utambulisho wake. Miongoni mwa alama zilizopendekezwa na Tume kuwa alama za taifa ni pamoja na Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Nembo ya Taifa.

Aidha, Tume inapendekeza sikukuu tatu zenye umuhimu wa kipekee katika uasisi wa Taifa na ambazo kwa matukio yake hazitabadilika na hivyo zitajwe ndani ya Katiba. Sikukuu hizo ni:-

1. Sikukuu ya kuasisiwa Taifa huru la Tanganyika ambayo inaadhimishwa kila tarehe 9 Desemba,
2. Sikukuu ya kuasisiwa Taifa huru la Watu wa Zanzibar ambayo ni siku ya Mapinduzi inayoadhimishwa kila tarehe 12 Januari; na
3. Sikukuu ya kuasisiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoadhimishwa kila tarehe 26 Aprili.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuhakikisha kuwa Alama na sikukuu za kitaifa zinapewa hadhi ya kikatiba na kutambulika kuwa ni vielelezo vya utaifa na alama kuu za dola na watu wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Wananchi wengi katika maoni yao walipendekeza kuwa alama na sikukuu za kitaifa zitambuliwe bayana katika katiba kwa madhumuni ya kubainisha utaifa, kujenga uzalendo, mshikamano na umoja wao.

Sababu nyingine ni kuondoa utata au kutoeleweka kwa uhakika ni zipi alama za taifa kwa mitizamo ya kiitikadi au mawazo ya makundi ndani ya Tanzania.

Uzoefu umechukuliwa katika nchi kadhaa za eneo letu na mabara mingine juu ya suala hili zikiwemo Kenya, Venezuela, Msumbiji na Namibia ambazo zimeweka alama za taifa na Sikukuu za kitaifa katika katiba zao.

Kwa mfano, Katiba ya Msumbiji kwenye Ibara cha 13 inaeleza: "*The symbols of the Republic of Mozambique shall be the national flag, emblem and national anthem*."

**Ibara ya 4: Lugha ya Taifa na Lugha za Alama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatamka kuwa Lugha ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano ni Kiswahili na itatumika katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kiserikali. Lugha ya Kiingereza au lugha nyingine yoyote inaweza kutumika kuwa lugha rasmi ya mawasiliano ya kiserikali pale itakapohitajika.

Rasimu ya Katiba imetambua matumizi ya mawasiliano mbadala ikiwemo lugha ya alama kwenye sehemu muhimu za umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii ya Rasimu imelenga kuitambua kikatiba lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha ya Taifa na umuhimu wake katika kuwaunganisha Watanzania na kujenga umoja na utaifa kama ilivyopendekezwa na wananchi wengi.

Pia, ni kujenga msingi kuwa lugha ya taifa ni kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano baina ya wananchi, dola kwa wananchi wake na pia kuimairisha utamaduni, mila na desturi zao.

Kadhalika, Rasimu ya Katiba imeitambua lugha ya alama kwa lengo la kuwawezesha wananchi wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum kuwa na haki ya kupata habari na taarifa mbalimbali za kitaifa na kimataifa ili kujenga misingi ya usawa na haki ya mawasiliano.

Kujenga msingi kwa Serikali kuwajibika kuweka miundo mbinu na kutoa elimu na vifaa ili kuwawezesha wananchi wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata haki hiyo kikatiba sawa na wananchi wengine kwa jumla. Ibara hii inaweza kusomwa sambamba na Ibara ya 10 (3) (b), inayoelezea juu ya Malengo Makuu, Ibara ya 11 na Ibara 45 juu ya haki ya watu wenye ulemavu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Dhamira ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa ina historia ndefu. Tanganyika ilitangaza nia hiyo toka mwaka 1963, na hata baada ya kuundwa Jamhuri ya Muungano suala hilo limebaki kuwa la kisera bila ya kupewa nguvu ya Kikatiba.

Hata wananchi wengi waliotoa maoni walitaka Kiswahili kiwe lugha ya kitaifa na hili litiwe ndani ya Katiba kwa ajili ya kukienzi na kukitukuza.

Tanzania ndiyo mhimili na chimbuko la Kiswahili lakini juhudi za kukiendeleza na kukienzi Kiswahili zimeshamiri ngazi ya kimataifa ambapo Kiswahili kina sifa ya kuwa lugha pekee ya Kiafrika iliyo na hadhi katika mashirika ya kimataifa. Kwa mfano,

Kiswahili ni Lugha Rasmi ya EAC na AU jambo lililoungwa mkono si na Tanzania peke yake, lakini pia na aliyekuwa Rais wa Msumbiji, Mheshimiwa Joachim Chisano, aliyekuwa Rais wa Nigeria, Mheshimiwa Olesugun Obasanjo na Mwenyekiti wa Kwanza wa AU Bw. Alpha Konare.

Kiswahili pia kinafundishwa katika zaidi ya vyuo vikuu 150 katika bara Asia, Marekani na Ulaya. Ni lugha ya Kiafrika inayotumika zaidi na mashirika ya maendeleo ya nchi nyingi. Pia Kiswahili kimetumika katika harakati za ukombozi barani Afrika.

Halikadhalika idhaa kadhaa maarifu duniani kwa mfano Idhaa ya Kiswahili ya Uingereza (BBC), Deutsch Welle, Radio ya Umoja wa Mataifa, Radio Iran, Radio ya Ufaransa na Radio Japan International hutumia Kiswahili katika matangazo yao. Kwa sasa kuna juhudi za kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha za Umoja wa Mataifa jambo ambalo litapata msukumo zaidi iwapo nchi iliyojitoa katika kukienzi na kukiendeleza itakitumia katika mawasiliano yake rasmi.

**Ibara ya 5: Tunu za Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inapendekeza kuwa Utu, Uzalendo, Uadilifu, Umoja, Uwazi, Uwajibikaji na lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi ya Taifa, ziwekwe katika Katiba kuwa ndiyo Tunu za Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Haja ya kuweka Ibara hii ni kujenga mwafaka miongoni mwa Watanzania kuhusu mambo yanayowaunganisha na kuwatambulisha kama taifa.

Vivyo hivyo, ni kujenga moyo wa kujithamini na kuthamini misingi muhimu ya maadili na taratibu mbalimbali katika taifa letu na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Tunu za Taifa ndiyo mtima na fahari ya Taifa. Wananchi walitaka ibara hii kiwepo hasa walipokuwa wakizungumzia kumomonyoka kwa maadili na kupungua kwa uzalendo. Umuhimu wa kujumuisha Tunu za Taifa ni kuwezesha ziote mizizi na ziweze kuenziwa na kurithishwa vizazi baada ya vizazi.

Uzoefu unaonyesha kuwa nchi kadhaa zimeingiza Tunu za Taifa katika Katiba zao kusisitiza sifa za msingi zinazowaunganisha wananchi kama vile Ghana na Kenya.

Kwa mfano, Ibara ya 10 (2)(a) ya Katiba ya Kenya inajumuisha Tunu zifuatazo: *(a) patriotism, national unity, sharing and devolution of power, rule of law; and participation of the people.*"

Ibara ya 10 (2)(b) ya Katiba hiyo ya Kenya inataja Tunu za Taifa zifuatazo; *"human dignity, equity, social justice, inclusiveness, equality, human rights, non-discrimination and protection of the marginalized"*.

Eneo hili la Katiba linapaswa kusomwa kwa pamoja na Utangulizi wa Rasimu hii na Ibara za 7, 8, 9, 10, 11, 13, 184 na 235 za Rasimu hii.

**Ibara ya 6: Mamlaka ya Wananchi, Utii na Hifadhi ya Katiba**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaainisha mamlaka ya wananchi, uhalali wa serikali na wajibu wa Serikali kwa raia hususan kuhakikisha ustawi wao. Ibara pia inabainisha ukuu wa wananchi kama chimbuko la katiba na mamlaka zote za nchi. Mwisho, Ibara inawapa wananchi uwezo wa kikatiba kuisimamia na kuidhibiti serikali na mamlaka zake ikiwemo kwa kuchagua viongozi na kuwawajibisha wawakilishi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara ni kuweka wazi kikatiba kuwa wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi, ambao kwa umoja na ujumla wao, wataimiliki na kuipatia Katiba uhalali. Aidha, ni kuweka dhana kuwa lengo kuu la Serikali ni kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi na kwamba Serikali itawajibika kwa wananchi; na wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kutambua kuwa wananchi ndiyo msingi na chimbuko la mamlaka yote ya nchi na kuifanya Serikali iwajibike kwa wananchi kwa kuhakikisha kuwa inasimamia maendeleo na ustawi wa wananchi wake na kutengeneza mazingira ya kikatiba yatakayowezesha wananchi kushiriki shughuli mbalimbali za nchi. Aidha, Ibara hii inafanana na Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayotambua mamlaka ya wananchi na wajibu wa serikali na ndiyo Ibara iliyowapa wananchi uhalali wa kushiriki moja kwa moja katika kufanya mabadiliko ya Katiba ya 1977.

Katiba za Kenya, Uswisi na Marekani zina vipengele vya namna hii. Ikumbukwe kwamba katika nadharia ya demokrasia, mamlaka na sauti ya mwisho ni ya umma (*popular control of public power*).
Katika muktadha wa Rasimu hii, Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 7, 10 (3), 11, 78, 119, 124 na 129 za Rasimu.

**Ibara ya 7: Watu na Serikali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaeleza kuwa muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake katika uendeshaji na utekelezaji wa shughuli zake, utazingatia azma ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa, kuhifadhi na kutumia rasilimali za Taifa ikiwemo ardhi, kwa manufaa ya wananchi wote.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kusisitiza Umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa, kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi kwa kulinda haki za binadamu na kuakisi maslahi ya wananchi katika sera, sheria na shughuli zote za serikali, kuhimiza usawa na ulinganifu

wa haki, fursa na manufaa kama misingi ya utendaji na kukuza umakini na uwajibikaji katika shughuli za serikali; na matumizi na ulinzi wa rasilimali za taifa.

### c. Sababu ya Mapendekezo

Suala la ardhi na rasilimali za nchi ni miongoni mwa maeneo yaliyotolewa maoni kwa wingi na wananchi. Dai lao kuu ni kuitaka Katiba iweke masharti kuhakikisha Serikali na vyombo vyake inalinda na kuhifadhi haki za binadamu na rasilimali za Taifa ikiwemo rasilimali kuu ya ardhi.

Pia, Ibara hii inaendeleza masharti yaliyopo katika Ibara ya 27 ya Katiba ya 1977 inayoweka wajibu wa kulinda mali asili na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu nchini. Taarifa nyingi zinazotathmini utendaji wa serikali, zikiwemo zile za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, zimeonyesha upungufu mkubwa katika usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa katiba, sera, sheria na mipango ya nchi katika ngazi zote za serikali jambo linalodhibitiwa kwa kuhimiza umakini na ushiriki wa wananchi katika masuala ya kitaifa.

## Ibara ya 8: Ukuu na Utii wa Katiba

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatamka kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano itakuwa ndiyo Sheria Kuu na Mamlaka zote za nchi, taasisi mbalimbali na wananchi watawajibika kuiheshimu, kuitii na kuifuata katika utekelezaji au maamuzi yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo ni kuondoa utata kuhusu ukuu wa Katiba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ni kuondoa utata wa mipaka ya mamlaka kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba za Nchi Washirika.

Aidha, Ibara hii inatambua ukuu wa wananchi,mmoja mmoja na ujumla wao, inaipa Katiba ukuu juu ya mamlaka na sheria zote. Hivyo, Katiba hii ndiyo sheria kuu ya nchi na ipo juu ya sheria na mamlaka zote za nchi. Pia, Rasimu inaelekeza kwamba maudhui ya katiba hii yabebwe katika Katiba, sheria, sera na mipango ya Nchi Washirika.

Kadhalika, madhumuni ya Ibara hii ni kuhakikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafuata utawala wa kikatiba kwa kusisitiza ukuu, uhifadhi na utii wa Katiba. Aidha, Ibara hii inaweka wajibu wa kukuza uraia kwa kuhimiza uelewa wa katiba miongoni mwa raia.

Suala hili pia limo katika Ibara 64(3) ya Katiba ya mwaka 1977.

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba isomwe pamoja na Ibara za 10, 11, 12, 64, 69, 110, 111, 117, 156, 167, 231, 233, 234 na 235 za Rasimu hii.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Umuhimu wa Ibara hii ni kubainisha hadhi na ukuu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya mfumo wa shirikisho. Pia, Ibara hii inadhamiria kubatilisha sheria, kanuni, maamuzi na mienendo inayokwenda kinyume na masharti ya Rasimu hii.

Ukuu na utii wa katiba unaainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar 1984 ingawa haya hayazingatiwi kwa ukamilifu. Katiba za Ethiopia, Ujerumani, Uswisi na Australia zina vifungu vinavyohusu ukuu na utii wa katiba kama msingi wa taratibu zote za kuendesha nchi. Vifungu hivyo vinawafanya wananchi na mamlaka za nchi kuwajibika kuiheshimu, kuilinda, na kuitii Katiba; pamoja na kuhakikisha kuwa uamuzi wowote ambao hauwiani au kwenda sambamba na masharti ya Katiba kuwa ni batili.

**Ibara ya 9: Hifadhi ya Utawala wa Katiba**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inakataza mtu au kikundi cha watu kuchukua au kushikilia mamlaka ya nchi isipokuwa kwa mujibu wa Katiba. Kitendo chochote kinachokiuka masharti ya Ibara hii ni batili na ni kitendo cha uhaini kama itakavyoelezwa katika sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumunii ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kushika madaraka ya nchi kwa mujibu wa Katiba ikiwemo kwa njia ya uchaguzi. Kukiuka Katiba na kuchukua madaraka ya nchi kwa nguvu ni kitendo cha uhaini. Hivyo, Ibara hii inajenga utamaduni wa kutii, kutetea na kulinda utawala wa Kikatiba miongoni mwa wananchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Historia ya Bara la Afrika baada ya uhuru na hata siku za karibuni (mfano huko Mali, Ivory Coast, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan ya Kusini) imeshuhudia mapinduzi ya kijeshi na utawala wa kiimla dhidi ya serikali zilizochaguliwa na watu. Nchi zilizopitia mapinduzi ya kijeshi au utawala wa kiimla kama Togo, Ghana, Nigeria, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Benin na Zaire zimeshuhudia matendo makubwa ya uuaji, dhulma na ubadhirifu

Katiba za nchi nyingi duniani zimeweka Ibara za aina hii ili kuzuia kupora madaraka kinyume na misingi ya kidemokrasia na katiba.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 63, 69, 78, 91, 235, 239 na 241 za Rasimu hii.

## SURA YA PILI

## MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA

### Ibara ya 10: Malengo Makuu

#### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inataja Malengo Makuu ya Taifa na kueleza kuwa msingi wake ni kulinda, kuimarisha na kudumisha haki, udugu, amani, umoja na utangamano wa wananchi kwa kuzingatia ustawi wa kila raia na jamii kwa jumla.

Aidha, malengo haya yanajikita katika kujenga Taifa huru lenye demokrasia, utawala bora, maendeleo endelevu na kujitegemea.

Malengo Makuu hayo yamegawanywa katika mafungu makuu matano yafuatayo:

1. Malengo ya kisiasa
2. Malengo ya kijamii
3. Malengo ya kiuchumi
4. Malengo ya kiutamaduni
5. Malengo ya kimazingira

Lengo la jumla la kisiasa ni kukuza demokrasia, usawa na utawala bora na kujenga ukomavu na uvumilivu wa kisiasa.

Kijamii ni kulinda heshima ya binadamu; kutoa fursa sawa kwa raia wote; kujenga utamaduni wa amani, maelewano na maridhiano; upatikanaji wa huduma za msingi, kuweka msingi wa hifadhi ya jamii; kuimarisha mawasiliano ndani ya jamii na kujenga fursa ya wananchi kupata na kufikia ushauri wa kisheria.

Kiuchumi ni kupatikana maisha bora kwa kila mwananchi, kujenga mazingira ya kufaidi na kushiriki kikamilifu katika fursa za kiuchumi, kuwapa sauti wazalishaji na kujenga misingi ya kujitegemea. Pia kuendeleza matumizi ya sayansi na kukuza ubunifu.

Kiutamaduni ni kulinda, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, mila, desturi, urithi wa asili, mali kale na lugha ya Kiswahili.

Kimazingira ni kuhakikisha panakuwa na umiliki wa umma wa haki za kijenetiki na maarifa ya asili, kulinda na kudumisha mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

#### b. Madhumuni na Lengo

Madhumini na malengo ya Ibara hii ni kuweka misingi ya wananchi kufikia ndoto, dira, vipaumbele na matarajio yao kama mtu mmoja mmoja na pia kama jamii na taifa.

Kuweka misingi na vigezo imara vya kuwawezesha wananchi kuwajibisha serikali na viongozi wao kwa jumla.

Ni kuweka misingi ya kikatiba kuongoza muelekeo wa sera, sheria na shughuli za kitaifa. Halikadhalika ni kutoa na kuweka fursa ya kufaidi haki.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Chemchemu ya malengo na misingi mikuu ya taifa kuwekwa katika katiba za nchi ni Katiba ya Uhuru ya Ireland ya mwaka 1916 walipojiondoa kutoka ukoloni wa Kiingereza. Walitaka Katiba hiyo isionekane kuwa imejikita katika kuunda na kusimamia vyombo tu, bali pia iwe inatoa fursa kwa wananchi kuweza kuota, kutamani na kutarajia tunu na ustawi wao.

Pia ilikuwa ni kujenga utamaduni mpya ambao unatoa nguvu kwa wananchi kuiagiza Serikali yao juu ya mambo ya ustawi na maendeleo ambayo wanataka serikali isimamie kwa ukamilifu wake, na kuwa na sauti juu ya mipango na sera za Serikali.

Pia wananchi wa Ireland walitaka viongozi na Serikali wasiwe mabwana na badala yake wawe ni watumishi wa umma.

Katiba nyingine zenye misingi mikuu ni Ghana, India, Nigeria, Papua New Guinea, Uganda na pia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar ya 1984.

**Ibara ya 11: Utekelezaji wa Malengo ya Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya katiba inaelekeza namna Malengo ya kitaifa yatakavyo tekelezwa na inasema wazi kuwa Malengo Makuu na muongozo kwa Serikali na taasisi zake katika utekelezaji wa sheria na sera kwa madhumuni ya kujenga jamii iliyo bora, huru na makini. Aidha, inaitaka Serikali kutoa taarifa kwa wananchi kupitia Bunge lao angalau mara moja kwa mwaka juu ya namna malengo hayo yalivyosimamiwa na kutekelezwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na Malengo haya ya Taifa ni kuhakikisha kuwa Serikali na mamalaka zake zimepewa mwongozo wa kisera na mwelekeo wa kiutendaji ambao itabidi kusimamia kwa niaba ya wananchi na kutoa fursa kwa wananchi kuweza kuipima serikali yao.

Pia, ni kuweka mwongozo wa dhamira ya malengo ya taifa yaliowekwa katika katiba hii.

Halikadhalika, vyama vya siasa vitakavyoshika madaraka vitawajibika kufuata bila kujali sera na ilani ya chama binafsi bali kuongozwa na malengo haya makuu ambayo yatakuwa ni ya kitaifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuwepo kwa Ibara hii katika Katiba ni kujaribu kujenga umoja, maridhiano na mwafaka wa kitaifa juu ya malengo makuu ya jamii na sera za nchi ili kuepusha mkanganyo na ushindani wa ilani na mikakati ya vyama na sera za kitaifa katika utendaji wa Serikali.

Kuwepo kwa sharti la Kikatiba la Serikali kutoa taarifa kila mwaka ni kuhakikisha kuwa haipuuzi wajibu huo na haiwanyimi wananchi haki ya kujua maeneo hayo makuu, ambayo ni msingi wa taifa, yamesimamiwa vipi mwaka hadi mwaka.

Kuhakikisha kwamba malengo haya yanakuwa ndiyo mwongozo kwa Serikali, mamlaka nyingine zote na wananchi kwa ujumla katika kutekeleza maamuzi yaliyo makini kwa lengo la kujenga jamii iliyo bora.

Ibara hivi vimekuwemo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977 na kuwa ya mwanzo kufanya hivyo kwa nchi za Afrika Mashariki. Katiba za nchi nyingine zenye Ibara kama hivi ni Philipines, Uganda, Sudan Kusini, Ghana, Kenya na Namibia.

**Ibara ya 12: Sera ya Mambo ya Nje**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka msingi wa kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa wenye tija kwa taifa na raia wake. Nguzo za sera hii ni kuimarisha umoja wa kikanda, wa Afrika, kutofungamana na upande wowote na kuheshimu sheria na mikataba ya kimataifa na pia kukuza haki za binadamu na uhuru wa watu. Halidhalika azma ni kukuza amani katika dunia.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuweka bayana misingi mikuu ya Sera ya Mambo ya Nje na falsafa yake na kuwapa nafasi wananchi kuelewa namna nchi yao inavyojihusha katika mambo ya nje na ushirikiano na mataifa mengine.

Kulinda maslahi ya kitaifa na yale ya dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutambua nafasi, msimamo na wajibu wa taifa katika mahusiano yetu na taasisi na nchi tunazoshirikiana au kuhusiana nazo.

Vile vile kukuza umoja wa Afrika na kujenga utangamano katika Bara la Afrika kuwa ni msingi mkuu wa sera yetu ya mambo ya nje.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kwakuwa palikua na ombwe juu ya Tanzania inavyoshirikiana na mataifa mengine palionekana kuwa na haja ya Ibara hii kwa mara ya kwanza katika Katiba ya Tanzania. Tanzania imekuwa ikiingia katika mahusiano ya makundi na jumuiya mbalimbali na wakati mwingine kujitoa bila ya wananchi kujua msingi wa uamuzi kama huo.

Pia, ni kuweka wazi suala la Mambo ya Nje kuwa ni suala la Muungano kwa kupewa hadhi yake katika katiba na kuwawezesha Nchi Washirika kujua nafasi zao katika suala hili la Mambo ya Nje ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatekeleza kwa niaba yao. Sababu nyingine ni kudhihirisha mamlaka kamili ya dola katika medani ya kimataifa.

Mifano ya nchi ambazo zimeweka suala la Sera ya Mambo ya Nje katika Katiba zao ni:, Ghana, Kenya, Siera Leone, Sudan Kusini, Switzerland, Uganda and Venezuela.

# SURA YA TATU

# MAADILI NA MIIKO YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA

## SEHEMU YA KWANZA

## MAADILI YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA

### Ibara ya 13: Dhamana ya Uongozi wa Umma

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inasisitiza kuwa uongozi ni dhamana ambayo kiongozi amepewa na wananchi ili awatumikie. Kwa maana hiyo kiongozi ana wajibu wa kuheshimu wananchi, kukuza imani ya wananchi na kulinda ofisi ya umma.

Ibara inaweka vigezo vya kuteuliwa na kuchaguliwa kwa viongozi wa umma kuwa ni pamoja na mwenendo wa mtu na uwezo. Halikadhalika sifa nyingine za kiongozi katika utendaji wake ni kutokuwa na upendeleo wa ukabila, udini na kuwa muwazi, mkweli, muadilifu na mwenye kujituma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii imewekwa ili kuwawezesha watu wanaotaka kugombea au ambao watapata fursa ya kuteuliwa kujua masharti ya Utumishi au Uongozi wa umma ambayo wataingia na wananchi wanaotaka kuwatumikia.

Kufanya marekebisho, kuinua hadhi, taswira na sifa ya ofisi ya umma kwa kuweka misingi bora ya viwango, vigezo na uadilifu katika kutumikia umma. Pia kuweka wazi vigezo ambavyo kila anayetaka kujiunga au kuchaguliwa katika utumishi wa umma atapaswa kuvimiza kwa ukamilifu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu moja wapo ya kuweka Ibara hii ni kurudisha, kuyahuisha na kuyapa nguvu ya kikatiba maadili ya uongozi yaliyokuwa katika Azimio la Arusha na Ahadi za TANU kama ambavyo wananchi wengi walivyotaka wakati wa utoaji wa maoni ya wananchi na katika Mabaraza ya Katiba.

Eneo hili ni jipya katika Katiba ya Tanzania ingawa tumekuwa na miongozo, sheria, Tume ya Maadili ya Viongozi na Sekretariati ya Maadili ya Viongozi. Utekelezaji wa yote haya umekuwa dhaifu kwa kukosa nguvu za kikatiba.

Wananchi wengi walilalamikia na kuchukizwa na mmomonyoko wa maadili ya umma uliokithiri, rushwa na ufisadi. Watu walizungumzia juu ya haja ya kudhibiti wizi, ufisadi, umangimeza, uzembe, kuweka mbele maslahi binafsi, utumiaji mbaya wa madaraka na kiburi kwa viongozi na watumishi wa umma. Kwa hali hiyo, Tume ikaona haja ya kukisikiliza kilio cha wananchi.

Katiba ya Phililipines ya mwaka 1987 iliweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma kama njia ya kuzuia rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Katiba hiyo imeainisha misingi ya maadili ya uongozi na uwajibikaji. Halikadhalika, Katiba ya Afrika Kusini ya mwaka 1994 ina misingi ambayo inawafanya viongozi wa umma kuwajibika katika kuwatumikia wananchi waliokuwa na matumaini makubwa kwa serikali katika kuboresha maisha yao baada ya miongo kadhaa chini ya Serikali ya kibaguzi.

Vilevile Katiba ya Nigeria inaeleza:

> " *A public officer shall not put himself in a position where his personal interests conflict with his duties and responsibilities*."
>
> Mtumishi wa Umma hatakiwi kujiweka kwenye nafasi ambayo maslahi yake binafsi yatagongana na majukumu yake ya kazi

Katiba hiyo inakwenda mbali zaidi kwa kueleza:

> "*Without prejudice with the foregoing paragraph a public officer shall not receive or be paid the emolument of any public office the same time as he receives or is paid the emulments of any other public office*."
>
> Bila ya kuathiri ibara iliyotangulia Mtumishi wa Umma hatapokea au kulipwa malipo ya mishahara na marupurupu mengine yanayoambatana na mishahara kutoka katika ofisi nyingine ya Umma kwa wakati mmoja.

**Ibara ya 14: Kanuni za Uongozi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inasisitiza wajibu wa kiongozi au mtumishi wa umma kuweka mbele maslahi ya umma badala ya kuweka maslahi yake binafsi ili kuepuka mgongano wa maslahi, kuhalalisha maslahi ya umma na kujihusisha na vitendo vya ofisi anayoifanyia kazi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara inakusudia kutenganisha maslahi ya umma na yale ya binafsi, kutunza hadhi na heshima ya ofisi ya umma na kuweka vigezo na viwango vya utumishi juu ya mwenendo wa utumishi wa umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu moja wapo ya kuwekwa Ibara hii ni kuweka utumishi wa umma wenye heshima na hadhi stahiki. Vile vile kuondoa rushwa, ufisadi na mgongano wa maslahi ambao kwa sasa umejaa katika mfumo wa utawala.

Kwa sababu hiyo Tume imependekeza maadili ya viongozi wa umma na miiko ya viongozi wa umma yawekwe katika katiba mpya. Aidha, Sekretairieti ya Maadili ya Viongozi ibadilishwe kuwa Tume kamili yenye mamlaka ya uwezo wa kusimamia maadili ya viongozi.

Rasimu hii inapendekeza kuwepo kwa Tume ya Maadili na Uwajibikaji ili kusimamia suala la maadili ya uongozi.

**Ibara ya 15: Zawadi katika Utumishi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka misingi ya utaratibu wa kushughulikia na kusimamia zawadi wanazopewa viongozi wanapotekeleza shughuli za kiserikali. Zawadi itakuwa ni kitu chochote chenye thamani atakachopewa kiongozi wa umma anapokuwa katika shughuli za umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inaweka namna ya kushughulikia zawadi hizo na njia bora zaidi ya kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi kwa kujipatia zawadi kupitia ofisi ya umma na ambapo hiyo itamfanya kiongozi kuweza kutenganisha dhima binafsi na dhima ya umma kuhusiana na zawadi anazopewa akiwa mtumishi wa umma.

Kujenga utamaduni wa viongozi wetu wa kupeleka zawadi kutunzwa ili ziweze kuhifadhiwa katika sehemu za makumbusho kwa faida ya vizazi vya leo na vijavyo na namna ya kutumia zawadi ambazo zinaweza kuharibika haraka kwa asili yake kwa maslahi ya umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kujenga utamaduni wa kuhifadhi zawadi zinazotolewa kwa viongozi ili zihifadhiwe kama vile Makumbusho ya Butiama ambayo yametunza zawadi zote alizopewa Mwalimu Nyerere lakini pakiwa na upungufu mkubwa wa taarifa juu ya zawadi walizopewa viongozi wetu wakuu wengine.

Kupunguza ushawishi wa kudai au kupewa zawadi viongozi au watendaji na kuathiri maamuzi yao yalalie zaidi ya maslahi ya taifa kwa kuweka maslahi yao binafsi mbele.

Tabia ya baadhi ya viongozi kudai zawadi kwa wananchi imekera watu wengi na kutolewa maoni na watu kadhaa wa kadhaa wakati wa kukusanya maoni ya Katiba.

Baadhi ya nchi ambazo zimeweka ibara kama hizo katika Katiba zao ni Nigeria ambapo ibara 6 (3) inaeleza:

> " *A public officer shall not put himself in a position where his personal interests conflict with his duties and responsibilities*."
>
> *Zawadi yoyote itakayotolewa kwa mtumishi wa Umma akiwa katika shughuli au Sherehe ya Kiserikali itachukuliwa kuwa zawadi iliyotolewa kwa taasisi ambayo mtumishi wa umma husika anaiwakilisha.*

## Ibara ya 16: Akaunti Nje ya Nchi na Mikopo

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inakataza kiongozi wa umma kufungua au kumiliki akaunti ya benki nje ya nchi kinyume na sheria na pia inakataza kiongozi wa umma kuomba au kupokea mikopo au faida yoyote inayoshusha hadhi na heshima ya utumishi wa umma.

### b. Madhumuni na Lengo

Ibara hii inakusudia kusisitiza uadilifu na uzalendo katika utumishi wa umma; kupunguza uwezekano wa kutorosha na kuficha fedha nje ya nchi, kupiga vita ufisadi, ubadhirifu na kulinda hadhi ya ofisi ya umma.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu ya mapendekezo ya ibara hii ni kuzuwia Viongozi na Watumishi Waandamizi wa Umma kufungua Akaunti nje ya nchi na hasa katika mfumo wa Benki za maficho zilizopo katika nchi za Switzerland Jersey Island na Isle of Man zijulikanazo kama Offshore Accounts.

Hali hiyo huashilia Viongozi au Watumishi hao Waandamizi wa Umma kuwa wamejipatia fedha hizo kwa njia zisizo halali na pia, husababisha kudhoofika kwa vyombo vya nchini vya fedha na kudhihirisha Viongozi na Watumishi Waandamizi wa Umma kutokuaminiwa na wananchi.

Uzoefu wa nchi nyingine Venezuela zimeweka ibara kama hizo kwenye Katiba kuzuwia Viongozi na Watumishi Waandamizi wa Umma kufungua Akunti nje ya nchi kwa kificho.

## Ibara ya 17: Wajibu wa Kutangaza Mali na Madeni

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inawataka viongozi wa umma kutangaza mali na madeni yao kwa Tume ya Maadili ya Viongozi kabla ya kuchukua na kuacha uongozi wa umma na zoezi hilo kufanyika kila mwaka mara moja.

Kwa masharti ya Ibara hii viongozi wa umma maana yake ni mtu binafsi, mwenza wake na watoto wake walio chini ya umri wa miaka 18.

### b. Madhumuni na Lengo

Ibara hii itasimamia utekelezaji wa tunu ya uwazi na uadilifu; na kuhimiza uaminifu katika jamii na uongozi na pia kuwezesha wananchi kujenga imani kwa viongozi wao.

Kuondoa uwezekano wa viongozi wa umma kujilimbikizia mali kinyume cha sheria.

### c. Sababu za Mapendekezo

Ibara hii imelazimika kuingizwa kwenye Rasimu ya Katiba kwa sababu ya uzoefu wa wazi wa matukio kadhaa ambapo viongozi wameonekana kutajirika kwa njia zisizo halali mara tu wanapoingia madarakani na bila ya kuwepo taratibu za kuwawajibisha.

Wananchi walitoa maoni kuwa matukio kama ya EPA, Richmond, taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na taarifa za kibunge, tume zilizoundwa pamoja na kesi zilizo mahakamani ni ushahidi wa madai hayo.

Katika uzoefu kwenye eneo hili kuna Katiba kadhaa ambazo zimeweka wajibu huu wa kutangaza mali na ni pamoja na Philipines ambapo kwenye Ibara ya 12:

> "*Without prejudice with the foregoing paragraph a public officer shall not receive or be paid the emolument of any public office the same time as he receives or is paid the emulments of any other public office*."
>
> *Wajumbe wote wa Bunge la Mabwanyenye (Senate) na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Watalazimika kutoa tamko la fedha wanazomiliki na biashara wanazofanya mara tu watakapoanza kazi.*

**Ibara ya 18: Mgongano wa Maslahi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kuzuia au kukataza kiongozi yeyote wa umma kushiriki katika uamuzi wa jambo au shughuli yoyote ambayo yeye ana maslahi nayo; au kuzungumzia kitu chochote ambacho ana maslahi nacho ya moja kwa moja. Kiongozi atapaswa kutoa taarifa ya mgongano huo kabla hajashiriki katika taratibu au kikao cha kufanya uamuzi.

Pia, kiongozi hatafaidika na uamuzi ambao kuna maslahi yanayomuhusu ambayo atayafanyia maamuzi. Na kuwa hatashika nafasi zaidi ya moja ya madaraka au kutumikia mihimili zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inakusudia kuwazuia viongozi wa umma kujinufaisha kwa namna yoyote wakati wa utumishi wao na kupiga vita ubinafsi na upendeleo kwa kutumia nafasi zao. Aidha, inasisitiza utii, uadilifu na umakini katika kazi anayoitumikia na kuepusha kutokea mgongano wa maslahi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Tume imependekeza kuwepo kwa Ibara hii ili kupigana na tabia inayoota mizizi ya viongozi kujiongezea maslahi na marupurupu, hasa wale wa kisiasa wakiwemo Wabunge.

Uzoefu unaonesha kuwa nchi nyingine, zikiwemo Namibia na Nigeria zina ibara kama hizi. Ibara ya 42(1)(2) ya Katiba ya Namibia inakataza viongozi wa umma kutumia nafasi zao kujinufaisha na kujitengenezea maslahi yao na kutumia nafasi au taarifa wanazozipata ili kujinufaisha kibiashara.

**Ibara ya 19: Matumizi ya Mali ya Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaeleza kuwa kiongozi wa umma hataruhusiwa kutumia au kuruhusu kutumika mali za umma zikiwemo zilizokodishwa kwa serikali kwa madhumuni ya kujipatia yeye binafsi au kumpatia mtu mwingine manufaa yoyote**.**

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inakusudia kudhibiti matumizi mabaya na haramu ya mali ya umma kwa manufaa binafsi. Pia kujenga tabia, nidhamu na utamaduni wa kuheshimu, kuhifadhi na kutunza mali ya umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kumejitokeza matumizi mabaya ya mali za serikali na watu kujiuzia rasilmali za umma kama vile nyumba, viwanda, migodi, mashamba makubwa na mali nyingine. Jambo hili wananchi walilizungumzia sana. Wakati mwingine uuzaji huo wa rasilmali na mali umesababisha migogoro mikubwa.

Vilevile mali za serikali zimekuwa zikikodishwa nje ya utaratibu na hivyo siyo tu kuikosesha serikali mapato lakini pia kuitia hasara kwa kulipa huduma ambayo haitolewi kwa mfano ukodishaji wa mitambo na kuwapangia hoteli viongozi wa umma.

Ibara hii inatakiwa isomwe pamoja na ibara za 7, 49 na 51 za Rasimu hii.

**Ibara ya 20: Utekelezaji wa Masharti ya Maadili**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza Bunge kutunga sheria kuhusu utaratibu wa utwaaji wa mali zilizopatikana kinyume cha sheria, utaratibu wa kumwajibisha kiongozi aliyekiuka wajibu na miiko. Pia inazungumzia uanzishwaji wa mitaala kuhusu Katiba na maadili katika taasisi za elimu na umma kwa ujumla.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuifanya sehemu ya Maadili ya Viongozi kuwa na meno ya kisheria na kukaziwa kikatiba. Pia sehemu hii inakusudia kuwadhibiti na kuwawajibisha viongozi wa umma wanaokiuka maadili na miiko ya uongozi.

Kujenga utamaduni na misingi ya uelewa na wajibu wa vijana katika masuala ya kikatiba na kimaadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ibara hii imevuka daraja ambalo halikuweza kuvukwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za kusimamia maadili zilizokuwepo. Hii inaifanya Serikali na vyombo vya kutunga sheria kulazimika kutunga sheria za usimamizi na urasimishaji wa jambo hili na kama vile Rasimu hii ilivyotangulia kuweka Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.

Sababu nyingine ni kuzuia vitendo vya kujitwalia mali na rasilmali za umma na kupiga vita uroho na uporaji wa mali hizo.

**Ibara ya 21: Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaorodhesha miiko ya uongozi. Miiko hiyo inajumuisha makatazo na wajibu wa kisheria. Pia inaweka masharti ya uwajibikaji wa kiongozi kwa makosa ya kimaadili.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii ipo kwa ajili ya kuainisha maadili na makatazo yanayohusu viongozi wa umma. Pia kuainisha uwajibishwaji wa viongozi hao ikiwa ni pamoja na kusimamishwa uongozi watakapokabiliwa na shutuma za kukiuka au kuvunja maadili.

Halikadhalika kuweka misingi imara ya kutenganisha biashara na shughuli binafsi na uongozi ili kuepuka mgongano wa maslahi na ukiukwaji wa maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sehemu hii imekuja kuitikia kilio cha wananchi wengi waliosema kuwa hawaoni hatua imara za kisheria kuchukuliwa dhidi ya viongozi wanaokiuka maadili. Wananchi walidai vitendo vya hujuma ya mali ya umma, kufanya biashara wakiwa katika uongozi vimekithiri na wakataka katiba ilisimamie hilo na sheria ziende mbali kudhibiti vitendo hivyo.

Hivyo, umeonekana umuhimu wa kujenga utamaduni wa uongozi na uwajibikaji wa pamoja na kupiga vita utumiaji wa nafasi ya uongozi kufanya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia au wa aina nyingine yoyote.

Aidha, sababu nyingine ni kuzuia viongozi wa umma kutumia nafasi zao kujinufaisha wao binafsi.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 52(3)(4) na (5) na Ibara 102 ya Rasimu inayozungumzia uwajibikaji wa pamoja wa Baraza la Mawaziri.

**Ibara ya 22: Marufuku ya Baadhi ya Vitendo**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kwa watumishi wa umma walio katika ajira ya kudumu kutoruhusiwa kuingia ajira nyingine ya kudumu yenye mshahara; kugombea, kuchaguliwa au kushika madaraka katika chama cha siasa au nafasi nyingine ya madaraka chini ya Katiba hii.

Pia, inaweka masharti iwapo mtumishi ataamua kugombea au kuridhia kuchaguliwa kushika nafasi ya madaraka ya kisiasa au ngazi ya uongozi katika chama cha kisiasa. Ibara inakusudia kutenganisha utumishi wa umma na siasa na kumpa hiyari mtumishi kubaki au kutobaki katika nafasi aliyoajiriwa na serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara inataka kutenganishwa utumishi wa umma na siasa. Pia inaweka masharti ya kikatiba kuzuia mtumishi wa umma kufanya ajira nje ya ajira ya Serikali na kupata mshahara. Hii inakusudia kuzuia mgongano wa maslahi kwa mtumishi wa umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Watoa maoni wengi walitaka watumishi wa umma wanaotaka kugombea nafasi za kisiasa kwanza wasite katika utumishi wao wa umma ili kuepuka kufanya upendeleo katika kujitengenezea mazingira ya kushika nafasi hizo za kisaisa.

Halidhalika, kumekuwa na tabia yakuchanganya shughuli za kisiasa na za umma kama vile mawaziri kuwa na nafasi za juu katika chama cha siasa.

Kuwepo kwa ibara hii kutasaidia kudhibiti uwajibikaji na hivyo kuongeza ufanisi.

Ibara hii isomwe na Ibara ya 125 cha Rasimu hii.

## SURA YA NNE

## HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI

## SEHEMU YA KWANZA

## HAKI ZA BINADAMU

### Ibara ya 23: Uhuru, Utu, Usawa wa Binadamu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatamka binadamu wote ni sawa na huzaliwa huru na kwamba kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake. Hii ndiyo haki ya msingi wa haki zote za binadamu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo ni kuweka haki ya msingi ya kutambuliwa, kuheshiwa na kuthaminiwa utu wa mwanadamu katika Katiba. Pia ni kusisitiza uhuru, utu na usawa wa kila mwanadamu. Haki hii ambayo inahusu uhai, inajenga msingi wa kudai haki nyinginezo ambazo zitakuwa zinakiukwa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ni muhimu kwa Katiba kutambua na kulinda utu wa mwanadamu ambao ni chemchemu, kiini, kitivo na ndiyo msingi wa haki zote za binadamu. Haki hii inayohusu utu haiwezi kuondolewa kwa hali yoyote ile.

Pia Ibara hii inatekeleza masharti ya mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu haki za binadamu. Ieleweke kwamba nchi ya kwanza duniani kufanya utu wa binadamu kuwa ni haki inayolindwa kikatiba ni Ujerumani. Kwa Bara la Afrika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ilikuwa ya kwanza kulinda haki ya utu wa mwanadamu

### Ibara ya 24: Haki ya Kuishi

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya uhai ya kila mtu kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika Serikali na jamii.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inaweka masharti ya kulinda na kuthamini uhai wa mwanadamu na usiondolewe kinyume na masharti ya kikatiba na sheria za nchi.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu ya msingi ni kuhakikisha kuwa hakuna mtu wala chombo chenye mamlaka ya kutoa uhai wa mtu mwingine na hivyo kulindwa kikatiba. Halikadhalika Ibara hii inapanua maana ya uhai na hivyo kuweka msingi wa namna uhai huo unavyoweza kuwekewa mazingira ya kila mtu kuishi na kufaidi kikamilifu haki hii.

Mahakama za Tanzania zimekwenda mbali zaidi kupanua dhana hiyo ya haki ya kuishi ikiwa ni pamoja na kuishi katika mazingira safi na salama. Kesi hizo ni pamoja na *Joseph D. Kessy and Others v. City Council of Dar es Salaam. High Court of Tanzania,* Dar es Salaam, *9 September 1991* (**Lugakingira J**) na pia ile ya *Festo Balegele and 794 others (Applicants) v. DSM City Council (Respondent) High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Misc. Civil Cause No. 90 of 1991*. (**Rubama J**).

## Ibara ya 25: Marufuku ya Ubaguzi

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatamka kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria na inapiga marufuku aina zote za ubaguzi na kuhakikisha kuwa watu wote wanalindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Ibara hii inaweka msingi wa haki ya kila mtu kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu anapokabiliwa na mashtaka au tuhuma na inakataza vitendo au adhabu ya kudhalilisha, kutwezwa na kumtesa mwanadamu.

### b. Madhumuni na Lengo

Ibara inalenga kuhakikisha usawa mbele ya sheria ili kuakisi dhamira ya taifa ya kujenga jamii yenye usawa. Pia ni kuweka katazo la kubagua raia katika hali yoyote. Inaweka haki ya kusikilizwa na kujitetea na kuondoa hali ya mtu kutumia nafasi yake kumkomoa mtu mwingine.

Ibara pia inakusudia kuzuia vitendo vya ubaguzi kwa kutumia tofauti za watu kama kigezo cha kuwadunisha au kuwanyima haki au fursa. Kuchukua hatua za upendeleo maalum kwa kutoa nafuu kwa makundi au watu kutokana na kutengwa kwao.

### c. Sababu za Mapendekezo

Ni kupiga marufuku ubaguzi na vitendo vyote vya kutesa na kutweza binadamu. Vilevile ni kutekeleza wajibu unayowekwa na mikataba mbali mbali ya kimataifa na sera za kibaguzi zinazolenga kuzuia utesaji wa binadamu za ndani ya nchi. Inajenga pia wajibu chanya kwa serikali kusimamia haki hii kuhifadhi na kutekeleza haki.

## Ibara ya 26: Haki ya Kutokuwa Mtumwa

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inazuia mtu kutendewa au kutumikishwa kama mtumwa kwa kufanyishwa kazi za kulazimishwa au kutwezwa. Upande mwingine ni kutumiwa kwa kusafirishwa na kufanyiwa biashara kwa faida ya mtu mwingine.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara inapiga marufuku na kukomesha biashara haramu ya kusafirisha binadamu. Inakusudia kutukuza na kulinda utu wa kila mtu na kuhakikisha kuwa sheria zinasimamia haki ya mtu kutotiwa katika utumwa.

**c. Sababu za mapendekezo**

Ibara hii inazuia ajira za kutweza na za mateso ambazo zipo katika sekta mbali mbali za ajira ndani na nje ya nchi. Pia inazuia utumwa mambo leo ambao umekuwa ukiripotiwa katika vyombo vya habari na katika taarifa za taasisi zinazosimamia haki za binadamu. Ibara hii pia inazuia watu kuchukuliwa na kutiwa katika biashara haramu ya binadamu ndani au nje ya nchi.

**Ibara ya 27: Uhuru wa Mtu Binafsi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii Rasimu ya Katiba inalinda na kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na hivyo kupiga marufuku kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kuchukuliwa uhuru wake kinyume na masharti yaliyowekwa na Katiba hii na sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuweka msingi kwa Serikali na vyombo vyake kuheshimu uhuru wa mtu binafsi na mtu ambaye haki yake imechukuliwa kinyume na utaratibu kuweza kudai fidia**.** Pia kuzuia maamuzi ya Serikali na vyombo vyake kuingilia au kuchukua uhuru wa mtu kinyume cha masharti ya Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Pamoja na kuwepo na sheria na taratibu zinazoongoza Serikali na vyombo vyake kujali matakwa ya demokrasia na mipaka inayokubalika katika jamii na kimataifa kuingilia uhuru wa mtu binafsi, lakini bado tatizo la kukamatwa watu nje ya utaratibu limekuwa likijitokeza.

Sababu nyingine ni kuzuia vitendo vya kuhamishwa wananchi kwa sababu mbali mbali na hata kukamatwa, kushtakiwa kwa mashtaka bandia kunakotokea sehemu mbali mbali za nchi yetu**.**

**Ibara ya 28: Haki ya Faragha na Usalama wa Mtu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya faragha na usalama wa mtu na pia kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na makaazi yake. Haki hii ni pamoja na kuheshimiwa mawasiliano yake binafsi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara inalinda na kuheshimu faragha, usalama na mawasiliano ya mtu.

**c. Sababu ya Mapendekezo**

Ibara hii imeingizwa katika Katiba ili kuheshimu faragha na mawasiliano binafsi ya mtu kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa. Ibara inamwezesha mwananchi kulindwa dhidi ya vyombo vya dola na taasisi nyingine kuingilia mawasiliano yake kwa kutumia vyombo vya kisasa vya kiteknolojia na kutumia taarifa hizo dhidi yake bila ya utaratibu wa sheria.

**Ibara ya 29: Uhuru wa Kwenda Mtu Anakotaka**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka msingi kwamba kila raia anaweza kwenda na kuishi popote ndani ya Jamhuri ya Muungano na kutoshurutishwa kuhama ndani ya nchi. Inatoa haki ya kutoka na kurudi ndani ya nchi. Pia inaainisha mipaka ya uhuru huo inayokubalika kikatiba ikiwa ni pamoja na kutekeleza hukumu au amri ya mahakama na kulinda maslahi ya umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ni kutambua na kuweka masharti na haki ambayo inamuwezesha kutekeleza haki nyingine kama ya kazi, kuabudu na kujumuika. Lengo pia ni kujenga utaifa na utangamano ili kila raia awe na haki ya kuishi popote ndani ya Jamhuri ya Muungano

**c. Sababu za Mapendekezo**

Hii ni katika kuendelea kudumisha kikatiba uhuru wa raia katika maeneo mbali mbali na kuwawezesha kwenda watakapo.

**Ibara ya 30: Uhuru wa Maoni**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka uhuru wa mtu kuwa na maoni na kueleza fikra zake; kutoingiliwa katika mawasiliano yake; kufanya ugunduzi, ubunifu na utafiti wa sanaa na mapokeo ya asili. Pia, Ibara hii inatoa haki ya mtu kupewa taarifa zozote kwa wakati wowote.

Ibara pia inaelezea mazingira ambayo haki hii inaweza kupunguzwa katika hali ya vita au machafuko ya kisiasa katika kuzuia propaganda za vita au matumizi ya taarifa hasi ya uhuru huu kwa kuchochea vita au chuki, rangi, ukabila, udini, itikadi au suala lolote linaloweza kuleta madhara kwa taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kutambua umuhimu wa uhuru wa maoni kama suala la amani, demokrasia na maendeleo. Pia ni kutambua uhalali wa kutoa maoni na kupata taarifa. Aidha, lengo jingine ni kujenga tabia ya watu kujiona huru, kujieleza, kusikilizwa na kuchangia katika mijadala ya kuchochea maendeleo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Moja ya sababu ya Ibara hii ni kuhamasisha watu kujieleza kwa uhuru, uwazi na ukweli bila ya wasiwasi wa kuchukuliwa hatua za kisheria kinyume cha misingi ya haki za binadamu. Pia inawezesha watu kushiriki katika majadiliano yanayojenga utashi wa kisiasa, maridhiano na mwafaka wa kitaifa juu ya masuala mbalimbali.

**Ibara ya 31: Uhuru wa Habari na Vyombo vya Habari**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki na uhuru wa kila mtu kutafuta, kupata, kutumia, kusambaza habari na taarifa; na kuanzisha vyombo vya habari bila ya kujali mipaka ya nchi. Pamoja na ibara hii kutambua uhuru na haki kwa vyombo vya habari kupata, kutumia na kusambaza habari lakini pia inaweka wajibu kwa vyombo hivyo kuambaza habari kwa wananchi. Katika kutimiza wajibu wao huo, vinatakiwa kuheshimu na kulinda utu, heshima na staha ya kila mtu. Ibara hii vile vile inaweka wajibu kwa serikali na taasisi zake, taasisi za kiraia na watu binafsi kutoa habari kwa umma juu ya shughuli zao na utekelezaji wa shughuli hizo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kulinda uhuru wa habari na vyombo vya habari. Pia ina lengo la kubainisha uhuru na wajibu wa vyombo vya habari kwa jamii. Lengo jingine la Ibara hii ni kuhamasisha ukuaji wa vyombo vya habari na kuweka mazingira bora ya uanzishaji na uendeshaji wa vyombo vya habari vilivyo huru na vyenye uwajibikaji kwa wananchi na taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuimarisha uhuru wa habari ambao ni muhimu kwa ustawi wa mtu binafsi, jamii na taifa. Kujenga mazingira na utamaduni wa serikali na taasisi zake kutoa taarifa kwa umma na hivyo kuwezesha wananchi kushiriki na kujua kinachoendelea katika serikali yao.

Pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa na kukidhi viwango na vigezo vya kimataifa vinavyohusu uhuru wa habari na vyombo vya habari.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka haki ya mtu kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu ya maisha na shughuli za wananchi na masuala muhimu kwa jamii. Rasimu hii inakwenda mbali zaidi kwa kuweka uhuru kwa vyombo vya habari na wajibu wake kwa wanachi na jamii na pia kujali utu, heshima na staha ya mtu.

**Ibara ya 32: Uhuru wa Imani ya Dini**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua uhuru wa kuamini au kutokuwa na imani ya dini, kubadili dini, kutangaza dini, na kufanya ibada. Ibara hii inatamka kuwa masuala ya uenezaji na uendeshaji wa shughuli za dini yatakuwa nje ya serikali na

yataendeshwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ili kulinda amani, usalama na umoja wa jamii na taifa. Kwa hivyo Ibara hii marufuku mtu au kikundi au taasisi ya dini kutumia uhuru wa kutangaza dini kwa namna ambayo italeta uvunjifu wa amani, kujenga chuki au kuchochea vurugu na ghasia. Kwa maana hiyo dini na imani ya dini haitatumika kwa namna yoyote itakayowagawa wananchi, kuleta uhasama au kuharibu amani miongoni mwa wananchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kulinda uhuru na hiari ya mtu kuwa au kutokuwa na imani ya dini na uhuru wa ibada maana suala hili ni la binafsi na siyo la dola wala shuruti yoyote ile. Pia lengo jingine ni kuweka mazingira yatakayowezesha dini zote kutumia uhuru kwa Amani, heshima, uvumilivu na staha kwa dini nyingine ili kulinda umoja na mshikamano katika jamii na taifa.

**c. Sababu ya Mapendekezo**

Katika miaka ya karibuni kumekuwa na matukio, migogoro na mivutano ya kidini kati ya dini moja na dini nyingine au madhehebu kwa madhehebu ndani ya dini moja au makundi ndani ya madhehebu moja. Jambo hili lilizungumzwa na wananchi wengi. Pia wananchi hao walizungumzia sana juu ya kuachia hali itakayopelekea kuingia katika migogoro na mivutano ya kidini kama inavyoonekana katika nchi nyingine.

Kwa hivyo Ibara hii inazuia utumiaji wa uhuru wa kutangaza na kueneza dini kufanywa ndiyo sababu na chanzo cha mtafaruku wa kidini. Sababu nyingine ni kuepuka matumizi ya dini kupata manufaa na kutimiza malengo ya kisiasa. Katazo hili ndilo suala jipya katika uhuru wa imani ya dini katika Rasimu hii ikilinganishwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977

**Ibara ya 33: Uhuru wa Mtu Kujumuika na Kushirikiana na Wengine**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa haki ya uhuru wa mtu kujumuika na kushirikiana kwa hiari na watu wengine ikiwa ni pamoja na kutoa maoni hadharani, kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kihalali.

**b. Madumuni na Lengo**

Kuendeleza uhuru wa raia kujumuika na kushirikiana na wengine katika mambo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Uhuru huu unamwezesha mtu kutekeleza uhuru wake wa maoni na wajibu wake wa kushiriki katika kuchangia mawazo ya kuleta maendeleo na ustawi wa jamii. Pia, kuweza kufuatilia kupitia makundi hayo maamuzi mbalimbali ya serikali.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka msingi wa kikatiba wa wananchi kuanzisha na kuendesha vyama vya siasa, vyama vya ushirika, vyama vya kijamii na makundi yenye malengo yanayofanana. Pia sababu ya kuwa na Ibara hii ni kuweka mazingira ya amani na utulivu ili kuwawezesha wananchi kutumia haki hii bila kuingiliwa kinyume cha Katiba na misingi ya

kidemokrasia. Ibara hii ni mwendelezo wa Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ibara ya 34: Uhuru wa Kushiriki Shughuli za Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya uhuru wa mwananchi kushiriki katika utawala na maamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuwawezesha raia kutekeleza na kutumia mamlaka yao juu ya serikali na mambo yote yanayohusu maisha yao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Haki hii inamhakikishia mtu kujiona anahusika na kujisikia ni sehemu ya jamii kwa kuwa na uhuru wa kushiriki katika maamuzi ikiwa ni pamoja na kuchagua na kuchaguliwa kuwa kiongozi. Pia ni kutoa fursa ya kutoa maoni yao juu ya uendeshaji wa serikali na mikakati ya kuleta maendeleo.

**Ibara ya 35: Haki ya Kufanya Kazi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya kila mtu kufanya kazi ya kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe na pia kupata fursa sawa katika kushika nafasi yoyote ya kazi au shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kumwezesha raia kupata kipato halali kwa kufanya kazi ili kuweza kujikimu yeye pamoja na familia yake. Pia ni kutoa fursa sawa na kuepusha ubaguzi katika upatikanaji wa ajira kwa mujibu wa sifa ya kazi inayohusika. Kutambua kuwa kazi ndiyo inayompa mtu heshima na utu wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kusisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za makusudi kujenga mazingira na kutoa fursa ya kupatikana kwa ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri. Mapendekezo haya pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa ikiwemo ile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

Haki ya kufanya kazi ipo katika Ibara ya 22 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Ibara ya 36: Haki za Wafanyakazi na Waajiri**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya kufanya kazi na kupata ujira wa haki, haki ya wafanyakazi kuanzisha vyama vya wafanyakazi na kufanya majadiliano kati ya

serikali, mwajiri na wafanyakazi. Pia Ibara hii inatambua haki ya waajiri kuunda chama chao na kushiriki katika mapatano na kuingia mikataba na wafanyakazi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua na kulinda haki za wafanyakazi na waajiri na kujenga mazingira ya kuondoa mifarakano na kujenga maelewano kati ya wafanyakazi na waajiri. Hii itasaidia sana kuondoa migogoro ya wafanyakazi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka misingi ya wafanyakazi na waajiri katika kujenga uchumi wa nchi. Aidha, sababu nyingine ni kuondoa uonevu, udhalilishaji na unyonyaji kazini. Pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa ikiwemo ile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO)

**Ibara ya 37: Haki ya Kumiliki Mali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua haki ya kila mtu kumiliki mali isipokuwa mali itakayothibika kwamba haikupatikana kihalali. Pia Ibara hii inazuia kutaifishwa au kuchukuliwa mali ya mtu, na ikiwa ni lazima ichukuliwe mwenye mali atalipwa fidia kwa kiwango cha soko kwa wakati husika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka haki ya kumiliki mali halali na kulipwa fidia stahiki na kwa wakati inapochukuliwa kwa madhumuni yoyote.

**c. Sababu ya Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha mali za watu hazitaifishwi bila fidia na hivyo kujenga mazingira ya uhakika wa kuchuma na kumiliki mali kihalali. hii itatoa motisha wa kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi. Ibara hii inapendekezwa ili kujenga mazingira ya kujenga imani na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje nchini

**Ibara ya 38: Haki ya Uraia**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa haki ya raia kutambuliwa uraia wake na kupewa hati ya kuzaliwa na kitambulisho cha uraia, na pale inapohitajika kupata nyaraka za kumwezesha kusafiri.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuifanya kuwa haki kwa raia kupewa hati ya kuwatambulisha uraia wao kwa madhumuni ya kufaidi haki za kiraia.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo ya Ibara hii ni kutoa haki hii muhimu kwa raia. Kwa kuwa ibara ya 29 ya Rasimu hii inapendekeza haki ya raia kwenda anakotaka, ibara hii

imewekwa kwaajili ya kuwezesha uhuru huo kutimizwa. Pia ni kuipa serikali wajibu wa kutambua na kulinda raia wake.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 56, 57, 58 na 59 za Rasimu ya Katiba.

**Ibara ya 39: Haki ya Mtuhumiwa na Mfungwa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa haki mtuhumiwa kuelezwa makosa kwa namna ambayo ataelewa na kupewa nafasi ya kutoa maelezo yake juu ya shauri linalomhusu au kukataa kutoa maelezo. Haki hii inamwezesha mtuhumiwa kupata msaada wa kisheria na kupelekwa Mahakamani mapema iwezekanavyo. Pia mamlaka inatakiwa kutunga sheria ambayo, pamoja na mambo mengine, itajumuisha mtuhumiwa kupata nakala ya mashitaka na kumbukumbu ya mwenendo wa mashitaka kwa lugha ambayo anaielewa ili kumuwezesha kuchukua hatua za kisheria zinazofuata.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua utu, heshima na haki ya mtuhumiwa na mfungwa. Pia ni kuipa wajibu Serikali kuzingatia utu wa watuhumiwa na wafungwa juu ya ubinadamu wao na kuwatendea haki za kibinadamu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutekeleza mikataba ya kimataifa juu ya haki za watuhumiwa na wafungwa kwa kuzingatia ubinadamu wao ambao hauondosheki. Haki hii imewekwa kwa mara ya kwanza katika Rasimu hii ya Katiba.

**Ibara ya 40: Haki ya Watu Walio Chini ya Ulinzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaweka utaratibu ambapo haki za kikatiba hazipotei kwa mtu ambaye amewekwa kizuizini na kwamba mtu huyu hatapoteza haki ya kuiomba mahakama kueleza sababu ya kuwekwa chini ya ulinzi. Aidha, inaweka zuio kwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusishwa na taratibu za kisheria nje ya mipaka ya Tanzania isipokuwa tu katika kutekeleza matakwa ya mikataba ya kimataifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutunza usalama wa taifa bila ya kuathiri haki za msingi, heshima na utu wa mtu aliyewekwa kizuizini au chini ya ulinzi. Lengo jingine ni kumlinda raia wa Tanzania asipelekwe nje kwa mashitaka kwa shinikizo la mataifa mengine nje ya matakwa ya mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya inaiwezesha Serikali kulinda usalama wa nchi na jamii katika misingi inayoheshimu haki za binadamu. Pia kulinda raia wake wasichukuliwe na kupelekwa kushitakiwa nje ya nchi isipokuwa inapokuwa ni kutekeleza matakwa ya sheria za kimataifa. Haki hii imewekwa kwa mara ya kwanza katika Rasimu hii.

**Ibara ya 41: Uhuru na Haki ya Mazingira Safi na Salama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inahusu haki ya kuishi katika mazingira safi na salama. Aidha, Ibara hii inatoa haki kwa kila mtu kutumia maeneo ya umma yaliyotengwa kwa madhumuni ya burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na shughuli za kiuchumi na wajibu wa kutunza na kuendeleza mazingira.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inalenga kukuza kiwango bora cha afya na ustawi wa kila raia na kuhakikisha kuwa mazingira yanahifadhiwa na kutumika kwa njia ambazo zitadumisha usafi, usalama na afya njema za jamii. Aidha, inalenga pia kuhamasisha utunzwaji wa mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vya baadaye.

**c. Sababu za Mapendezo**

Haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya afya haikuwekwa bayana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Hata hivyo mahakama Kuu katika maamuzi yake ilitafsiri kwamba haki ya kuishi maana yake ni pia kuishi katika mazingira safi, salama na ya afya. Aidha, sheria ya usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, imeweka kifungu kinachotambua haki hii. Kwahiyo ibara hii inatekeleza maamuzi hayo ya Mahakama na kuipa nguvu Sheria ya Mazingira, Sura 191.

Pia, umuhimu wa kuwa na nguvu za kikatiba umekuja kwa sababu ya matukio ya kidunia kama vile mabadiliko ya tabia nchi kunakopelekea mvua zisizo na mpango na kiangazi cha muda mrefu kinachosababisha majangwa. Hali kadhalika kumekuwa na athari za kimazingira kutokana na maendeleo kupitia viwanda na makazi na kuchafua mazingira na baionuai na mara nyingine kushindwa kurejesha mazingira katika hali ya asili.

Vile vile kumekuwa na mtindo ulioenea wa katiba nyingi kuweka angalau viwango vya msingi vya kimazingira kwa mujibu wa matakwa ya mikataba ya kimataifa. Kwa mfano katiba zenye vifungu vya kulinda na kuhimiza utunzanji wa mazingira ni pamoja na Afrika Kusini, Kenya, Namibia na Uganda.

**Ibara ya 42: Haki ya Elimu na Kujifunza**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inahusika na haki ya kupata fursa ya kupata elimu bora bila ya vikwazo. Inataja elimu ya msingi iliyo bora na inayoweza kupatikana bila ya malipo. Ibara pia inataka kuwekwa mazingira ya kumuwezesha kijana kupata elimu ndani na nje ya mfumo rasmi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara inakusudia kutambua umuhimu wa elimu bora na fursa sawa kwa gharama zilizo nafuu. Utoaji huo wa elimu kwa mapana yake na unafuu pia kusaidie kujenga jamii

iliyoelimika na iliyo makini katika maamuzi na utekelezaji wa shughuli zake katika dunia hii ya utandawazi, teknolojia na ubunifu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Moja ya sababu ya kuwekwa kwa haki ya elimu na kujifunza ni kutambua kuwa elimu haina mwisho na ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira na kutoa fursa kwa raia wake kupata elimu na kujifunza kwa gharama nafuu.

Watoa maoni wengi walilalamikia kuongezeka kwa tofauti baina ya walio nacho na wasio nacho na kunavyoathiri fursa na uwezo wa watu wa kipato cha chini kupata elimu. Kumekuwa na tofauti kubwa ya ubora wa elimu kwa shule za vijijini na zile za mijini, na tofauti kubwa zaidi baina ya shule za Serikali na shule za binafsi.

Wananchi pia, walizungumzia kuwa watoto wa viongozi na wenye uwezo wanapata fursa na elimu bora zaidi kuliko watoto wa wakulima na wafanyakazi. Kumekuwa na malalamiko pia kuwa mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara yameleta hasara badala ya faida katika jamii.

Tume imetambua hali mbaya ya elimu katika nchi yetu katika nyanja zake zote kama vile walimu, mitaala, vifaa, majengo na kadhalika na ndiyo sababu ya kuweka kipengele hiki. Hii ni mara ya kwanza haki ya elimu na kujifunza kutambulika katika Katiba.

**Ibara ya 43: Haki ya Mtoto**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelezea, pamoja na mambo mengine, haki ya mtoto kupewa jina na uraia, kutoa mawazo, kusikilizwa na kulindwa dhidi ya uonevu na udhalilishaji.

Pia haki ya mtoto kucheza, kupata elimu bora, malezi bora na ya kimaadili, na ulinzi kutoka kwa wazazi, walezi na mamlaka ya nchi bila ya kubaguliwa kwa njia yoyote**.**

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kuainisha haki za msingi za mtoto na kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha utekelezaji na usimamizi wa haki hizo. Ibara kinaweka wajibu wa moja kwa moja wa wazazi, walezi, jamii na mamlaka za nchi kuona haki hizo kwa ujumla wake zinalindwa na zinatekelezwa kikamilifu.

Kuweka mazingira ya kuelekeza kuwepo kwa kizazi chema zaidi kimaadili na kinachoweza kujua wajibu wake ili kukabili mabadiliko ya ndani na nje na kuweza kuchukua nafasi zao katika uchumi na ustawi wa taifa lao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ibara hii inatekeleza mkataba wa kimataifa na mkataba wa Afrika juu ya haki ya mtoto na sheria na sera za kitaifa. Kumekuwa na kiwango kikubwa cha unyanyasaji wa watoto nchini, matendo ambayo wakati mwingine yakinasibishwa na Imani za kichawi na kuchangiwa pia na ukosefu wa uwelewa katika jamii. Hivyo kumeonekana umuhimu wa kuweka Ibara hii kwa mara ya kwanza katika Katiba ili wazazi, walezi na jamii kwa

ujumla wajue wajibu wao na kujenga hamasa ya kujenga kizazi kinachoepukana na makovu ya manyanyaso.

**Ibara ya 44: Haki na Wajibu wa Vijana**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inahusu haki na wajibu wa vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za Serikali na jamii kwa jumla. Kwa hivyo Serikali inatakiwa kuwawekea mazingira bora ya kuwawezesha kuwa raia wema na kuwapatia fursa za kushiriki kikamilifu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo kuu la Ibara hii ni kutambua nafasi na umuhimu wa vijana kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa lao.

Pia ni kuwatayarisha kuwa viongozi na raia wema, kushika uchumi wa nchi yao, kuwa wazazi bora na wana jamii bora kwa ujumla.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kwa mujibu wa Sensa ya Tanzania iliyofanyika 2012 imeonesha kuwa vijana ndiyo kundi kubwa zaidi la Watanzania kwa asilimia 60 lakini hapajakuwa na kifungu cha katiba kinachotambua nguvu kazi hii.

Kwa hivyo Tume imeona haja na umuhimu wa kuweka Ibara hiyo kwa mara ya kwanza ili taifa lijielekeze katika kuhakikisha kwamba nguvu kazi hiyo inatumika kwa njia chanya kwa faida yao na ile ya taifa kwa vijana hao kujua wajibu wao, na kuona na kutumia fursa zilizopo.

Pia ulazima wa kuwepo Ibara hii ni kujaribu kama taifa kuwaelekeza vijana katika fikra za kisasa za kiuchumi na kimaendeleo ambazo zinaendana na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia ili wasiachwe nyuma kuweza kujiajiri au kufanya kazi na kuweza kujiepusha na vitendo vya ukosefu wa maadili na kupoteza utamaduni, silka na mila za Kitanzania.

Haki hii inawekwa ndani ya Katiba kwa mara ya kwanza.

**Ibara ya 45: Haki za Watu Wenye Ulemavu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba ambayo ni mpya inakusudia kuweka msingi wa kuheshimu utu na haki mbalimbali za watu wenye ulemavu zikiwemo kuwapatia elimu kwa kutumia vifaa stahiki,kuwekewa miundo mbinu na mazingira mwafaka na kutumia lugha maalum inapohitajika. Pia ni kuweza kushiriki katika shughuli za kijamii, kupata ajira na kugombea nyadhifa za uongozi bila ya kubaguliwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua kundi hili ambalo ni asilimia 10 ya wananchi wa Tanzania na kujali upekee wa hali zao. Pia ni kutambua kuwa ni kundi linaloweza kutoa

mchango mkubwa katika Taifa na hivyo kuhakikisha serikali inatoa mahitaji maalum na miundo mbinu stahiki ya kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za jamii kwa mfano elimu, usafiri, uzalishaji, burudani na kadhalika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya kupendekeza haki hii ambayo ni mpya katika Katiba ni kutekeleza mikataba na maazimio ya kimataifa pamoja na sheria na sera za nchi zinazotambua na kulinda haki watu wenye ulemavu.

Kwa kiasi kikubwa kundi hili halijapewa umuhimu na jicho linalostahiki na hivyo kuonekana haliwezi kutoa mchango wowote katika jamii. Mapendekezo ya Rasimu hii ni kuweka nguvu za kikatiba ili hali hiyo irekebishwe. Imeonekana wazi kuwa pale kundi hili linapowezeshwa linaweza kutoa mchango mkubwa katika nyanja mbalimbali.

Pia, ni kujenga mazingira ya kundi hili kujiamini na kuona kuwa jamii na taifa linawathamini na hivyo kujitokeza kuchukua fursa ambazo zinaweza kupatikana kwa kutengeneza ustawi wao, familia zao na kutoa mchango maridhawa kwa taifa.

**Ibara ya 46: Makundi Madogo Madogo katika Jamii**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inazungumzia kuyawezesha makundi madogo madogo kushiriki katika uongozi kupatiwa fursa maalum za elimu, fursa za kujiendeleza kiuchumi na ajira; na pia kutengewa maeneo ya ardhi ambayo kwa desturi huyatumia kuishi na kupata riziki ya chakula.

Ibara inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kuendeleza shughuli zao za kiuchumi, makazi, elimu na afya ili kukidhi mahitaji ya leo na kesho ya watu katika makundi hayo. Ibara hii ya Rasimu pia inatoa tafsiri ya makundi madogo madogo kuwa ni watu wanaoishi kwa kutegemea uoto wa asili kwa mazingira yanayowazunguka kwa ajili ya chakula, makazi na mahitaji mengine ya maisha.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii ni mpya na inalenga kuitambulisha jamii ya Kitanzania, hasa jamii ambazo zinazunguka makundi hayo, ili kujua namna ya kuishi na makundi hayo na kutambua haki zao.

Lengo la kuwa na Ibara hii ni kutambua kuwepo kwa makundi hayo na haja ya kuhifadhi maisha na mazingira yao kwa ajili ya maendeleo yao. Ibara pia inataka kudumisha utambulisho wao lakini bila ya kuyaacha makundi hayo nyuma kimandeleo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Maoni mbalimbali yalielezea juu ya makundi madogo madogo kuachwa nyuma katika kasi ya maendeleo na mengi yakibakia kuishi katika mazingira ya asili na kuonekana kutengwa. Ibara inataka kubadilisha mtazamo wa Watanzania juu ya makundi hayo kuwafanya watambue kwamba yanaweza kuishi yakiwa na utambulisho wao lakini pia wakajumuishwa katika maisha, mazingira na utamaduni mpana wa Mtanzania. Sababu

nyingine ni kukubali ukweli wa upana wa jamii ya Kitanzania na aina za maisha za makundi mbalimbali.

**Ibara ya 47: Haki za Wanawake**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka heshima na utu kwa kila mwanamke, kuwa salama dhidi ya unyonyaji na ukatili, kushiriki bila ubaguzi katika nafasi za maamuzi, kupata fursa na ujira sawa na mwanamme katika kazi zinazofanana. Pia inatoa haki ya kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu na mila zenye madhara, kulindwa ajira yake wakati wa ujauzito na kupata huduma bora ya afya.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo ni kutambua na kurekebisha mtazamo hasi dhidi ya wanawake juu ya mchango wao na nafasi yao katika jamii. Kuizindua jamii kuwa katika ajira na elimu raia wote wana haki sawa bila kujali jinsi zao, na kwamba kwa kuwa kila mtu hulipwa kwa jasho lake basi mwanamke alipwe sawa na mwanamme kwenye ajira yenye sifa sawa.

Aidha, Ibara inalenga kuwalinda wanawake dhidi ya ubaguzi na uonevu na mila zenye madhara. Muhimu zaidi ni kuweka msingi wa Kikatiba kuhakikisha kuwa wanawake wanalindwa katika jukumu lao la uzazi na kuwekewa msingi wa kikatiba wa upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa ustawi wao na wa watoto.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Wanawawake ni kundi muhimu katika jamii na lina mahitaji maalum ambayo upatikanaji wake ndiyo uhai wa taifa. Kwa kiasi kikubwa wamekuwa hawana sauti katika vikao vya maamuzi na hali hiyo inapaswa kurekebishwa kwa kutoa fursa ya wanawake kugombea na kushika nafasi kama hizo.

Kwa kuwa jamii ya Tanzania bado haina usawa, Ibara hii imewekwa ili kuondoa ubaguzi, ukatili na unyonyaji dhidi ya wanawake.

Pia mapendezo haya yanakuja kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa juu ya haki mbalimbali za wanawake, kwa mfano Convention on Elimination of Discrimination Against Women (CEDAW) na Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Right of Women in Africa, ambayo Tanzania imeridhia. Haki hizo ni pamoja na kuwa na kiwango cha asilimia 50-50 katika ngazi za uwakilishi na maamuzi. Ibara hii pia inazipa nguvu ya kikatiba haki za wanawake ambazo zimetambuliwa katika sheria na sera mbalimbali za nchi.

Nchi ambazo zina vifungu vya kulinda haki za wanawake ni nyingi na kwa kweli Tanzania ilikuwa inaonekana iko nyuma kwa mujibu wa namna ambavyo demokrasia yake imekuwa na kupanuka.

**Ibara ya 48: Haki za Wazee**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya katiba ni mpya na inatambua kuwepo wa wazee, likiwa ni kundi maalum, na kujali mchango wao walioutoa katika ujana wao kwenye ujenzi wa taifa. Ibara inatoa fursa kwa wazee kushiriki katika shughuli za kijamii, kutodharauliwa na kupata mahitaji ya msingi kutoka familia, jamii na mamlaka ya nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuwatambua wazee kuwa ni kundi ambalo lina mahitaji maalum lakini pia wakiwa na uzoefu na ujuzi ambao wanaweza kuutumia kwa faida ya jamii na taifa.

Lengo pia ni kuwawezesha wazee kushiriki katika shughuli wanazoweza kufanya, kuheshimiwa na kupatiwa haki zao kama raia.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kumekuwa na hali ya kuwatenga na kuwadharau wazee, hasa wanawake, katika jamii ya Kitanzania na hata kufikia kuuawa. Wazee wameonekana ni kundi ambalo halina msaada na ni tegemezi. Hivyo Ibara hii inataka kurekebisha muonekano na mtazamo huo.

Maoni mengi ya wananchi yalilalamikia kuwa hali ya wazee hasa vijijini ni ya kutisha na inayohitaji hatua za makusudi katika maeneo ya afya, lishe na malazi kwa vile kunakosekana hifadhi ya kinga ya jamii katika ngazi ya taifa.

Ibara hii pia inakidhi mahitaji ya mikataba ya kimataifa kama vile African Charter of Human and People's Rights ya kuwatunza na kuwalinda wazee na kwa hivyo jukumu lianze kwa mtoto na jamii inayomzunguka.

## SEHEMU YA PILI

## WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA YA NCHI NA HAKI ZA BINADAMU

### Ibara ya 49: Wajibu wa Raia

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inataja wajibu wa raia kuwa ni pamoja na kulinda na kutetea katiba na sheria; tunu na urithi wa taifa; kulipa kodi; kuheshimu haki, uhuru na maslahi ya watu wengine; kulinda na kuheshimu utamaduni na maadili ya taifa na kuilinda Tanzania. Pia Ibara hii inaweka wajibu wa kulinda na kutunza mazingira.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu wajibu wa raia kwa taifa, jamii, watu wengine na mazingira. Aidha, ni kujenga utamaduni wa wananchi kuwajibika na kuchangia katika shughuli zinazohusu maendeleo ya nchi; na kusimamia, kuheshimu na kulinda haki za watu wengine**.**

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina Ibara inayohusu wajibu wa raia lakini Rasimu ya katiba imeongeza wajibu wa kulipa kodi, kulinda na kutunza mazingira.

Ibara hii ni kutekeleza masharti ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (African Charter of Human and Peoples' Rights) pamoja na maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania (DPP v. Daudi Pete, Criminal Appeal No. 28 of 1990) ambayo inataka kila raia ajue wajibu wake katika suala la haki za binadamu na watu ambazo msimamizi wake mkuu ni dola**.**

### Ibara ya 50: Wajibu wa Kushiriki Kazi

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaeleza kuwa kila raia ana wajibu wa kushiriki kazi kwa kujituma, uaminifu na kwa nidhamu. Ibara pia inapiga marufuku kazi yoyote ya shuruti, kikatili au kutweza.

Hata hivyo Ibara inaweka wazi kuwa tafsiri ya kazi za shuruti haijumuishi zile zinazohusu kutekeleza hukumu au amri ya mahakama, kazi ya askari wa jeshi na kazi wakati wa hali ya hatari na ujenzi wa taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi na kutumia nguvu kazi yake kwa faida yake na taifa. Aidha Ibara inalenga kupiga marufuku kazi za shuruti, ukatili na kutweza bila ya kuathiri kazi za dharura na zile za lazima kwa mujibu wa sheria na maslahi ya nchi.

### c. Sababu na mapendekezo

Ibara hii inalenga kuwafanya watu waone kuwa kufanya kazi ndio chimbuko pekee la kipato na kujitegemea, na ni msingi wa utu wa binadamu.

Aidha, ni kujenga mazingira ya wananchi kushiriki katika kazi za kujitolea katika suala la ujenzi wa taifa, kazi za dharura wakati wa hali ya hatari au kuokoa maisha ya watu yanapotokea maafa.

Maudhui ya Ibara hii yanalingana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya 25 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Ibara ya 51: Ulinzi wa Mali ya Umma

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa wajibu kwa raia kulinda mali asili ya taifa, mali ya mamlaka ya nchi ama mali yoyote inayomilikiwa na wananchi pamoja na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu.

### b. Madhumuni na Lengo

Ibara hii ina madhumuni na lengo la kuweka masharti kuwa mali ya asili ya mamlaka ya nchi na rasilmali zinalindwa na kuheshimiwa. Aidha, inalenga kujenga moyo wa Watanzania kukataa na kupiga vita uharibu na ubadhirifu.

### c. Sababu za Mapendekezo

Ibara hii imewekwa ili kuhimiza tabia ya kuheshumu na kujali mali na rasilimali zinazomilikiwa kwa pamoja na umma zikiwemo ardhi na maliasili ambayo ndiyo rasilimali kuu ya taifa. Sababu nyingine ni kumfanya kila mtu kujiona kuwa yeye ni mdhamini wa ardhi na maliasili kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mabadiliko ya kiuchumi duniani na nchini yamesababisha kujengeka katika mamlaka za nchi na jamii tabia ya ubinafsi, uroho, uvamizi na uchotaji wa rasilmali. Hivyo, Ibara hii itasimamia eneo hilo ipasavyo kwa kujenga uelewa na uzalendo zaidi ili kudhibiti madhara hayo.

Ibara hii ya Rasimu ni mwendelezo wa maudhui ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## Ibara ya 52: Haki na Wajibu Muhimu

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa kila raia haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu zinazowekwa kwenye Katiba bila ya kupendelewa au kubaguliwa kwa misingi ya nasaba au jadi.

Ibara inaweka wajibu kwa kila mtu kutenda na kuendesha shughuli zake bila ya kuingilia haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kuhakikisha haki na wajibu sawa kwa wote. Lengo jingine ni kuziba njia ambapo mtu anapata kazi au cheo kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi wake.

Pia kunawekwa wajibu wa mtu mmoja mmoja kuheshimu uhuru na haki za watu wengine.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Utekelezaji wa haki za binadamu ulilalamikiwa sana na wananchi na walisema kuwa katika hali halisi kumekuwa na upendeleo na matabaka katika suala la utoaji wa haki.

Kwahiyo, moja ya sababu ya kuwepo Ibara hii ni kujenga uelewa katika jamii kwamba dhana ya kuheshimu haki za binadamu ni pana na hivyo sio tu wajibu wa Serikali, bali unamhusu kila mtu. Dhana hii pana inawezesha kuwa na jamii ambayo inajali ustawi, haki na maisha ya raia wake.

Sababu nyingine ni kuhamasisha na kujenga utamaduni wa raia wa kuchukua hatua pindi katiba inavunjwa na kuendeleza utamaduni huo kwa vizazi vijavyo.

Ibara hii inafanana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya 29 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Ibara ya 53: Hifadhi ya Haki za Binadamu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka wajibu kwa serikali na mamlaka zake kuzingatia na kuhifadhi haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba, mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia. Hapa ndipo wajibu wa Serikali kulinda, kusimamia na kutekeleza haki za binadamu unapowekwa. Pia inatoa wajibu kwa mamlaka na wananchi kuhifadhi haki za wengine.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuhakikisha kuwa serikali na mamlaka zake zinahifadhi na kulinda haki za binadamu kwa upana wake. Pia ni kujenga tabia ya wananchi kutambua, kudai na kutetea haki zao, za wenzao na za jamii kwa ujumla.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Wananchi wengi walizungumzia juu ya kushuka kiwango cha utekelezaji wa haki za binadamu na kujionyesha sana watendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali hasa ngazi za chini kwa kuwa na kiburi katika kutumia nafasi zao.

Sababu moja wapo ni kutekeleza masharti ya mikataba ya kimataifa inayotoa wajibu kwa mamlaka ya dola kulinda, kuheshimu na kuendeleza haki za binadamu.

Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Ibara ya 54: Usimamizi wa Haki za Binadamu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza Mahakama au chombo chochote cha kufanya maamuzi kuzingatia mambo makuu kuhusu haki na usawa, utu na uhuru wa mtu binafsi, sheria za kimataifa za haki za binadamu na haki za jamii na maslahi ya jamii kwa ujumla**.**

Ibara hii vilevile inampa kila mtu haki ya kufungua shauri mahakamani kwa ajili ya kudai haki yake au ya mtu mwingine. Ibara pia inaweka wigo mpana wa kuwasilisha na kufungua shauri mahakamani juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa aliyeathirika au mtu anayetaka kumuwakilisha.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo ni kutoa nguvu za kisheria kwa mtu binafsi, muakilishi wake au kundi kuweza kufungua shauri la haki za binadamu mahakamani.

Kuipa wajibu mahakama wa kusimamia na kulinda katiba na kuwa mlinzi na msimamizi mkuu wa haki za binadamu. Mahakama pia inapewa uwezo wa kikatiba wa kubatilisha sheria yoyote iwapo imekwenda kinyume na Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mapendekezo haya yanatokana na hukumu mbalimbali za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ya Tanzania zilizotafsiri kwa upana na kukazia mashauri mbalimbali ya haki za binadamu. Moja ya hukumu hizo za Mahakama Kuu ni ile ya *W. K. Butambala v. Attorney General (Mwalusanya J)*. Hata hivyo, hukumu hizo na mapendekezo yake hazikuzingatiwa katika mabadiliko ya Katiba ya awali.

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwepo mkanganyiko kuhusu uwezo wa kufungua mashauri mahakamani kudai haki za binadamu kati ya sheria mbali mbali za uendeshaji wa mashauri na katiba.

Sababu nyengine ni kuendana na mabadiliko yanayotokea duniani juu ya namna ya kusimamia mashauri ya haki za binadamu ili wananchi wafaidi haki mbali mbali kwa uhakika, uwazi na uhuru.

Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Ibara ya 55: Mipaka ya Haki za Binadamu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka mipaka ya haki za binadamu inayokubalika katika jamii, inayo heshimu uwazi na demokrasia kwa kuzingatia utu, usawa, uhuru na vigezo ambavyo havififishi au kuondoa kabisa haki ya msingi.

Vigezo hivyo vya kuzingatiwa ni aina ya haki; umuhimu na sababu za kuweka mipaka; asili na ukubwa wa mipaka husika; uhusiano baina ya mpaka husika na sababu yake; njia nyepesi ya kufikia madhumuni ya mpaka husika na umuhimu wa kulinda usalama wa nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo mojawapo ni kuainisha kikatiba na kuiwekea masharti mipaka ya haki za binadamu itakayokuwa ya wazi na kidemokrasia. Hii ina maana kuwa amri ya zuio au masharti yoyote ya kuzuia haki za binadamu pia yawe na mipaka yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maamuzi ya mahakama juu ya haja ya katiba kuweka mipaka kuhusu masuala ya haki za binadamu. Kwa maana kuwa kila hatua ya kuzuia uhuru lazima itoe sababu na kueleza mipaka ya uzuiaji huo**.** Moja ya hukumu hizo za Mahakama ya Rufani ya Tanzania ni katika shauri la *Kukutia ole Pumbun & Another v. Attorney General and Another* [1993] TLR. 159. Pamoja na shauri la *Attorney General v. Lohay Akonaay and Joseph Lohay, Court of Appeal of Tanzania, Civil Appeal No. 31 of 1994,* (**Nyalali C.J., Makame and Kisanga JJA**.).

Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## SURA YA TANO

## URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

### Ibara ya 56: Uraia wa Jamhuri ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Katiba ya Sheria inatambua aina mbili za uraia katika Jamhuri ya Muungano kuwa ni wa kuzaliwa na kujiandikisha. Aidha, Ibara inatamka kuwa aliyekuwa raia kabla ya kupitishwa kwa Katiba hii ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka uraia wa Jamhuri ya Muungano kuwa ni mmoja na kutoruhusu raia wa Tanzania awe wa kuzaliwa au wakuandikishwa kuwa raia wa nchi nyingine. Aidha madhumuni ya Ibara hii ni kumpa raia haki ya kutambuliwa, kulindwa, na kupata huduma mbalimbali anazostahili kupata raia. Lengo jingine ni kuepusha kuwa na uraia wa nchi mbili katika Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Moja ya sababu za mapendekezo haya ni kwamba mamlaka makuu ya kidola (*Sovereign functions*) ni uraia ambalo limewekwa kuwa suala la Muungano. Uraia ni msingi wa utambulisho (*identity*) unaompa hadhi aliyenao kulindwa na nchi yake ikiwa ni pamoja na haki zake za binadamu za asili na zisizoondosheka (*inherent and inalienable rights*) kama zilivyotambuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa.

Msingi wa kuweka uraia wa nchi moja ni kuepuka kuwabagua au kuwatenga raia wa Tanzania katika matabaka na madaraja yanayotokana na utofauti wa hali na fursa zao.

Ibara hii imezingatia maoni ya wananchi wengi na hasa wa maeneo ya mipakani waliokataa uraia wa nchi mbili kwa sababu za kiusalama, kiuchumi, kimaadili na matumizi mabaya ya rasilimali ya ardhi na uharibifu wa mazingira.

Ibara hii ni mpya katika katiba ingawa ipo sheria ya uraia yenye maudhui yanayofanana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya Rasimu hii.Ibara hii pia isomwe pamoja na Ibara ya 57,58,59 na 235 ya Rasimu hii.

### Ibara ya 57: Uraia wa Kuzaliwa

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mtu ambaye wakati wa kuzaliwa mama au baba yake ni au alikuwa raia wa Tanzania. Raia wa kuzaliwa ni pamoja na mtu aliyezaliwa nje ya Tanzania kuanzia tarehe ya kuzaliwa kwake ikiwa mama au baba yake ni raia wa Jamhuri ya Muungano. Aidha, Ibara hii inamtambua mtoto mwenye umri wa chini ya miaka saba aliyekutwa

ndani ya eneo la Jamhuri ya Muungano katika mazingira ambayo wazazi wake hawajulikani atachukuliwa kuwa raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano na atapoteza uraia huo wa kuzaliwa ikibainika kuwa wazazi wake sio raia wa Tanzania.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua na kuthamini uraia wa kuzaliwa na haki zake na pia kuupa wajibu na dhamana kubwa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Uraia wa kuzaliwa umejengwa katika msingi wa uzalendo usiotiliwa shaka (*patriotism*) unaompa raia wajibu wa kuitetea, kuilinda na kuifia nchi yake bila ya tashwishi au shaka. Kwa hiyo uraia ndiyo kigezo na sifa ya kupewa dhamana ya uongozi wa taifa na kuwa katika vyombo na mifumno ya ulinzi na usalama. Madhumuni mengine ni kukiri uwepo wa Watanzania walio nje ya nchi na kuzaa, kuzaliwa na kutambua uzao wa raia wa Tanzania walio nje kuwa ni raia wa kuzaliwa na sio wa kurithi ingawa wamezaliwa nje ya nchi.

**Ibara ya 58: Uraia wa Kuandikishwa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaweka masharti ya kuwa raia wa kundikishwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Masharti hayo ni pamoja na mtu aliyefunga ndoa na raia wa Tanzania na amedumu katika ndoa hiyo kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo na kutimiza masharti yaliyoainishwa katika Katiba na mtoto aliyeasiliwa na raia wa Jamhuri ya Muungano aliye chini ya miaka kumi na nane ambaye wazazi wake siyo raia wa Tanzania atakuwa raia wa Tanzania wa kuandikishwa. Uraia wa kuandikishwa pia unaweza kutolewa kwa mtu ambaye amekuwa mkazi wa Jamhuri ya Muugano na ametimiza masharti yote ya sheria za nchi ikiwa ni pamoja na kukana uraia wa nchi aliyotoka.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuwatambua watu ambao wamekuwa wakaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wana sifa za kisheria za kuomba uraia wa kuandikishwa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa raia wa nchi nyingine ambao wapo tayari kuukana uraia wa nchi zao na kuchukua uraia wa Tanzania baada ya kuwa wameishi Tanzania kwa muda maalum uliowekwa na Katiba au sheria, wameoa au kuolewa na raia wa Tanzania na watoto walioasiliwa na raia wa Tanzania kuweza kuomba uraia wa kuandikishwa.

**Ibara ya 59: Hadhi ya Watu wenye Asili au Nasaba ya Tanzania**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inawatambua na kuwapa hadhi maalum watu wenye asili au nasaba ya Tanzania na ambao wameacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kupata uraia wa nchi nyingine wanapokuja Tanzania kwa masharti yatakayoainishwa na sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuwapa hadhi maalum watu walioacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano tofauti na raia wa nchi nyingine ambao hawana asili au nasaba ya Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwawezesha watu waliokuwa raia wa Tanzania waliopoteza uraia kwa namna yoyote ile kuwa na hadhi maalum wanapokuwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadhi hiyo itawaondolea usumbufu wanaporejea Tanzania na kuwapa fursa mbalimbali za kushiriki katika maendeleo ya nchi, jamii na familia zao zilizobaki Tanzania. Mapendekezo haya yalizingatia kuwa nchi itakapotambua uraia wa nchi mbili haitakuwa na msingi wa kikatiba na kisheria wa kuwazuia raia wa nchi nyingine kubaki na uraia wao wanapokuwa raia wa kuandikishwa wa Tanzania kwa kuzingatia kuwa Jamhuri ya Muungano inapakana na nchi nane na italeta changamoto ya usalama na ulinzi.

Uzoefu wa nchi ya India na Ethiopia ambazo hazina na zimesita kutoa uraia wa nchi mbili kwa sababu za kiulinzi na usalama lakini zimetoa hadhi maalum kwa watu wenye asili na nasaba ya nchi hizo ambao wameacha kuwa raia wa nchi hizo. Katika Katiba ya India watu hao wanaitwa "Persons of Indian Origin" na wana hadhi maalum.

Kwa mujibu wa sheria za India, mtu mwenye asili au nasaba ya India hadi kizazi cha nne atapata hadhi ya "*Person of Indian Origin (PIO)"* isipokuwa kwa raia wa nchi za Afghanistan, Bangladesh, Bhutan, China, Iran, Nepal, Pakistan na Sri-Lanka. Watu hao wenye hadhi ya PIO wanaweza kupata fursa zifuatazo;

i. Kupata kadi ya kitambulisho cha PIO.
ii. Hahitaji viza ya kuingia na kutoka India.
iii. Anaweza kukaa miezi sita nchini India mfululizo bila kulazimika kujiandikisha uhamiaji.
iv. Wana haki sawa ya kupata huduma za kiuchumi, kifedha na elimu kama ilivyo kwa raia.
v. Wana haki ya kununua, kumiliki, kuhamisha, kuuza mali isiyohamishika isipokuwa kwa mashamba makubwa ya kilimo.
vi. Watoto wao wanahaki ya kudahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu nchini India.
vii. Wana haki ya kupata makazi katika utaratibu unaosimamiwa na Serikali au wakala wake.

Hata hivyo hawana haki zifuatazo;

i. Hawaruhusiwi kupiga kura.
ii. Hawaruhusiwi kugombea nafasi yoyote ya kisiasa wala kushika madaraka ya utawala.

## SURA YA SITA

## MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO

### Ibara ya 60 Muundo wa Muungano

#### a. Maudhui ya Ibara

Ibara ya Rasimu ya Katiba inaainisha muundo wa Muungano wa Shirikisho la Serikali tatu, ambazo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia inaiinisha mihimili mikuu ya dola ambayo ni Serikali, Bunge na Mahkama ya Jamhuri ya Jamhuri ya Muungano.

Aidha inazungumzia utekelezaji na usimamizi wa shughuli za Jamhuri ya Muungano. Ibara hii pia inatambua kwamba mambo mengine ya kiutendaji yasio ya Muungano yataainishwa katika Katiba za Nchi Washirika.

#### b. Madhumuni na Lengo

Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kutambua mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ni Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano, Mamlaka yasio ya Muungano ya Tanganyika na mamlaka yasio ya Muungano ya Zanzibar.

Aidha, kuipa kila mamlaka kuwa na Serikali yake kusimamia maeneo yake yaliotajwa katika Katiba hii ikiwa ni pamoja na vyombo vyake vya utekelezaji na kwa hivyo kutenganisha mamlaka hizo au kuziweka bayana.

Hali kadhalika madhumuni na lengo ya Ibara hii kuweka masharti ya Kikatiba ya kutambua kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano. Vilevile lengo jengine ni kuimarisha na kudumisha Muungano wa hiari wa pande mbili zinazohusika.

Lengo jingine ni kutunza utambulisho wa kihistoria na kiutamaduni wa nchi Washirika wa Muungano zilizoamua kuungana kwa hiari. Hiyo itaondoa hofu ya Zanzibar kumezwa na Tanganyika lakini pia, itahifadhi utambulisho wa Tanganyika na kuondoa taswira kwamba ndiyo imevaa hadhi ya Serikali ya Muungano.

#### c. Sababu ya Mapendekezo

Sababau ya mapendekezo haya ni kutambua kuwa, kwa kawaida panapokuwa na muungano wa hiari wa nchi mbili huru na yakaainishwa mamlaka ya mambo ya muungano na mamlaka ya mambo yasio ya muungano, na yakatenganishwa mamlaka ya Mambo ya Muungano na mamlaka mambo yasiyo ya Muungano, muundo huo unapaswa kuwa ni muundo wa shirikisho la Serikali Tatu.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 katika Ibara za **4, 34, 64** na **102** inatambua mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano. Kwa upande wa Katiba ya Zanzibar, 1984 katika ibara za **5A na 99** inatambua mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano. Mamlaka hizo tatu ni mamlaka ya Mambo ya Muungano, mamlaka ya mambo yasiyo ya Muungano ya Tanganyika na mamlaka ya mambo yasiyo ya Muungano ya Zanzibar.

Pia, kuwepo kwa mamlaka hizo kumefafanuliwa na Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha *"Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania"* katika ukurasa wa 15, kwamba:

> *"Nchi mbili zinapoungana na kuwa Nchi Moja mifumo ya kawaida mifumo ya miundo ya Katiba ni miwili: Kwa mfumo wa kwanza kila nchi itafuta serikali yake, na Nchi mpya inayozaliwa itakuwa ni nchi moja yenye serikali moja. Katika mfumo wa pili kila nchi itajivua madaraka Fulani ambayo yatashikwa na serikali ya shirikisho, na itakuwa na serikali ambayo itakuwa na mamlaka juu ya mambo yaliobaki. Mambo yatakayoshikwa na serikali ya shirikisho ni yale ambayo yakibaki katika mamlaka ya nchi zilizoungana, basi kwa kweli nchi hizo zitakuwa hazikuungana kuwa nchi moja, bali zinaendelea kuwa nchi mbili zenye ushirikiano mkubwa katika mambo fulani fulani.Shirikisho halisi la nchi mbili litakuwa ni nchi moja yenye serikali tatu, Serikali ya shirikisho na serikali mbili za zile nchi mbili za awali zilizoungana kuzaa nchi mpya moja."*

Pia Mwalimu alifafanua zaidi kuhusu jitihada za kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki alisema:

> *"Kama jambo hilo lingetokea, nina hakika kabisa kwamba mfumo wa nchi mpya ambayo ingezaliwa ungekuwa ni wa Shirikisho; ama shirikisho la Nchi Tatu zenye serikali nne, au Shirikisho la Nchi Nne lenye Serikali Tano. Kwa kweli hata kesho nchi za Afrika Mashariki zikiamua kuungana na Tanzania ikawa ni mshiriki, naamini kuwa ni rahisi zaidi kushirikisha Tanzania yenye Serikali Mbili- ya Zanzibar na Tanganyika- kuliko Tanzania yenye Serikali Mbili, ya Tanzania na ya Zanzibar."*

Hata hivyo, tangu mwaka 1964 hadi mwaka 2014, mamlaka ya Mambo ya Muungano na mambo ya Tanganyika yasiyo ya Muungano yaliwekwa katika Katiba moja na Serikali moja yaani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mamlaka ya mambo ya Zanzibar yasiyo ya Muungano yaliwekwa katika Katiba ya Zanzibar na yanasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Muundo wa Muungano unaelezewa katika Ibara ya 60 ya Rasimu ya Katiba, unazingatia matakwa ya kifungu cha 9(2) (a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yaliyoielekeza Tume pamoja na mambo mengine kuzingatia kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kudumisha Muungano.

Rasimu imependekeza muundo wa Serikali tatu baada ya kufanyika uchambuzi wa takwimu na kuchanganua sababu zilizotolewa na makundi mbalimbali inapendekeza muundo wa Seikali tatu ili: kuitambua Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano, kuendelea kuitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuondoa kero za muda mrefu zinazotokana na muundo uliopo wa Serikali mbili na kuthamini mapendekezo yaliyotolewa na Tume na Kamati mbalimbali zilizoundwa hapo awali kuhusu mfumo wa Serikali.

Muundo huo uliochanganya Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano ya Tanganyika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kimantiki umeshindwa kueleweka

kwa wananchi. Aidha muundo huo ndio chimbuko kuu la ubishi, migogoro mivutano (zinazojulikana kama kero) kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kiuhalisia, katika utekelezaji wa Mambo ya Muungano, Serikali zote ama kwa kukubaliana au kujiamulia zenyewe zimebadili taswira ya muundo wa Muungano katika utendaji wake ambao umekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

Utata na mkanganyiko unaouzonga Muungano unatokana na kuwepo kwa malalamiko kutoka kila upande wa Muungano. Kwa upande wa Zanzibar baadhi ya malalamiko yao kuhusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano ni:

1. Serikali ya Tanganyika imevaa taswira/koti la Serikali ya Muungano ambalo linaisaidia Tanganyika zaidi kuliko Zanzibar. Taswira hiyo imeifanya Tanganyika kuwa ndiyo Tanzania na Watanganyika ndiyo wamekuwa Watanzania; na Wazanzibari wamebaki kuwa Wazanzibari.
2. Mambo ya Muungano yamekuwa yakizidi kuongezeka na hivyo kuathiri uhuru wa Zanzibar (Autonomy) na kufifisha hadhi ya Zanzibar (Identity).
3. Kuvunjwa kwa makubaliano ya Hati ya Muungano kwa kuificha sura ya Tanganyika katika Muundo wa Serikali ya Muungano.
4. Kumuondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
5. Kutokuwepo kwa uwazi wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali ya Muungano.
6. Kutokuanzishwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja.
7. Kuwepo kwa mkanganyiko wa ugawaji wa mapato na jinsi ya kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za Muungano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar.
8. Kuwepo kwa chumi mbili tofauti zinazoshindana katika nchi moja.
9. Zanzibar kutoshirikishwa kikamilifu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika masuala ya kupata misaada na mikopo kutoka nje ya nchi.
10. Malalamiko kuwa viongozi wakuu wa Zanzibar wanachaguliwa Dodoma na sio Zanzibar kwenyewe.
11. Zanzibar inalalamika kuwa kuna baadhi ya mambo yamefanywa kuwa ya Muungano kupitia kutungwa kwa sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa mambo yasio ya Muungano na baada ya hapo mambo hayo kupata hadhi ya Muungano.

Malalamiko haya ya Zanzibar kwa kiwango kikubwa yanatokana na muundo wenyewe wa Muungano. Kuyaweka mambo ya Tanganyika chini ya Serikali ya Muungano, kumesababisha Serikali ya Muungano kujishughulisha zaidi na mambo ya Tanganyika, hasa mambo ya maendeleo.

Kwa mfano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inashughulikia sana mambo ya kilimo, viwanda na biashara, ujenzi, uchukuzi, mawasiliano, nishati na madini, maji, elimu,

huduma za afya na maliasili na utalii kwa upande wa Tanzania Bara ambayo siyo Mambo ya Muungano.

Ingawa Bunge ni la Mungano na kinadharia kutarajiwa kushughulikia mambo ya Muungnao kwa kiasi kikubwa lakini linashughulikia mambo yaliotajwa hapo juu ambayo ni ya Tanganyika kwa uzito mkubwa.

Kwa hali hiyo inavyotokea ni kuwa Wabunge kutoka Zanzibar kwenye Bunge la Muungano huwa hawashiriki katika mijadala kwa mambo ya Tanganyika lakini pia huonekana ni kuwapotezea muda Wabunge hao kutoka Zanzibar katika Bunge ambalo linajadili mambo yanayowahusu kwa uchache sana.

Wakati wa kikao cha bajeti mambo yanayohusu Tanganyika ndiyo mambo yanayotengewa siku mbili au tatu za majadiliano; wakati Mambo ya Muungano kama vile: ulinzi, mambo ya ndani na mambo ya nje yanatengewa siku moja au nusu siku. Aidha, hata ziara za Kamati za Bunge la Jamhuri ya Muungano kukagua shughuli za maendeleo zinafanywa Tanzania Bara tu. Mambo haya bungeni yanasimamiwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye, kihalisia hana mamlaka wala madaraka yoyote kuhusu Zanzibar.

Muundo uliopo sasa wa Serikali mbili pia umesababisha kuwepo kwa wizara au taasisi zenye sura au zinazotekeleza mambo ya Muungano pekee; mambo ya Tanzania Bara na mambo ya mchanganyiko; kwa maana ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano hali ambayo inapelekea ugumu wa kutofautisha gharama za muungano na zisizo za muungano katika wizara au taasisi hizo. Hakuna njia ya kubadili hali hii kwa sababu Serikali ya Muungano haina mamlaka juu ya mambo ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar. Mawaziri katika Serikali ya Muungano wamelazimika kufanya mipango na kutafuta rasilimali kwa ajili ya Tanganyika tu. Zanzibar inalazimika kufanya mipango yake wenyewe na ili kupata rasilimali kama vile misaada na mikopo ni lazima ipitie Serikali ya Muungano, jambo ambalo utekelezaji wake una matatizo mengi. Njia pekee ambayo ingefanya mambo ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar yapewe uzito sawa na Serikali ya Muungano ingekuwa ni kuyaweka mambo hayo chini ya Serikali ya Muungano, yaani hiyo ingekuwa Serikali Moja badala ya mbili; lakini hilo lingefanyika, Zanzibar ingekuwa imemezwa na Tanganyika.

Kwa upande wa Tanzania Bara, baadhi ya malalamiko kuhusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano ni haya yafuatayo:

1. Zanzibar imekuwa nchi huru, ina bendera yake, ina wimbo wake wa Taifa, ina Serikali yake na imebadili Katiba yake ili kujitambua kuwa ni nchi.
2. Zanzibar imebadili masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inasema Sheria za Muungano zinazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano zitumike sehemu zote za Muungano, badala yake Katiba ya Zanzibar inaelekeza kuwa ili Sheria itumike Zanzibar ni sharti ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi. Maana yake ni kuwa, Katiba ya Zanzibar ipo juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

3. Zanzibar imetunga sheria kuhusu fedha ambalo ni suala lililo kwenye madaraka ya Muungano.
4. Zanzibar imetunga Katiba ambayo imechukua madaraka ya Rais yaliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano yanayoeleza kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano ana madaraka ya kugawa nchi katika maeneo ya kiutawala. Marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 yameitambua Zanzibar kuwa ni nchi na yanampa mamlaka Rais wa Zanzibar kuigawa nchi katika maeneo ya kiutawala.
5. Katiba ya Zanzibar inasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni wa nchi mbili lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kwamba, Tanzania ni nchi moja.
6. Masharti ya Kikatiba yaliyowekwa na Katiba ya Zanzibar kuhusu mchango wa Zanzibar katika uendeshaji wa Mambo ya Muungano yanapingana na masharti ya Katiba ya Muungano. Mifano kwenye Katiba ya Zanzibar
7. Muundo wa Muungano uliopo umepoteza utambulisho wa kihistoria wa Tanganyika na fursa ya watu wa Tanganyika kutetea maslahi yao ndani ya Muungano.
8. Wananchi wa Tanzania Bara kutokuwa na haki ya kumiliki ardhi Zanzibar wakati wenzao wa upande wa Zanzibar wana haki hiyo Tanzania Bara.
9. Pia Wabunge wa Tanganyika kulalamika kuwa Wabunge wa Zanzibar huchangia mijadala kwa mambo yasio ya Muungano na ambayo kwa uhakika wake ni mambo ya Tanganyika na kwamba Wabunge wa Tanganyika hawana nafasi ya kuchangia katika Baraza la Wawakilishi kwa mambo yasio ya Muungano na yanayohusu Zanzibar.
10. Kwa mujibu wa Sheria ya Mzanzibari, 1985 Watanzania ambao ni wa Watanganyika hutakiwa kutimiza sifa maalum ili kuweza kupata haki za kiraia huko Zanzibar ilhali Mzanzibari huweza kupata haki ya kiraia wakati wowote na popote katika ardhi ya Tanganyika. Haki hizo za kiraia ni pamoja na kugombea uongozi na kupiga kura.

Tangu mwanzo wa Muungano ilikubalika kwamba, Zanzibar ibaki na hadhi yake *(identity)* na iwe na uhuru wa maamuzi kuhusu mambo yasiyo ya Muungano *(autonomy).* Katika utekelezaji, Zanzibar imechukua hatua za kuimarisha hadhi yake: kwa maana ya kuwa na Bendera, Wimbo wa Taifa, Nembo na Ukuu wa nchi kamili. Pili kwa makubaliano na Serikali ya Muungano, baadhi ya Mambo ya Muungano yamebadilishwa kwa kiwango kikubwa ili kuipa Zanzibar uhuru wa kuamua *(Autonomy).*

Hivi sasa mambo mengi ya Muungano hayatekelezwi kikamilifu kimuungano. Mambo hayo ni pamoja na kodi, bandari, leseni za viwanda, usafiri na usafirishaji wa anga, utafiti, takwimu, posta na simu, gesi na Mahakama ya Rufani.. Baadhi ya mabadiliko yaliyofanywa yameleta mgongano kati ya Katiba ya Muungano na Katiba ya Zanzibar, hasa kwenye vipengele vinavyohusu kodi, Madaraka ya Bunge kutunga Sheria, Madaraka ya Rais kuigawa Nchi, tafsiri ya nchi na uraia.

Mambo haya yamebadilishwa bila kubadili Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na kwa maana hiyo mabadiliko hayo yamevunja Katiba.

Kuna njia mbili za kurekebisha mambo hayo. Njia ya kwanza ni kuyarudisha chini ya Muungano mambo yote yaliyobadilishwa. Kiuhalisia jambo hili haliwezekani. Serikali zote mbili zilifikia makubaliano kuondoa mgongano wa Katiba kwa mambo fulani, kama vile Madaraka ya Bunge, Uraia na kodi, lakini utekelezaji wake ulishindikana kupitia Taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu jitihada za kuondoa mambo ambayo ni vikwazo katika kutekeleza shughuli za Muungano ( Taarifa ya Kamati ya Shelukindo.

Hata hivyo miaka kadhaa baadae Ripoti ya Shelukindo imeshindwa kutekelezwa kwa ukamilifu wake na kubakisha hali ya mivutano na mizozano ndani ya Muungano, kama ambavyo imekuwa kwa Tume nyengine nyingi ambapo inaonekana zaidi mtizamo wa Tume hizo ni kuiridhisha zaidi Zanzibar ibakie ndani ya Muungano kuliko kutafuta suluhu ya kudumu ya kero za Muungano na kuwa na maslahi kwa pande zote mbili za Muungano.

Hali inakuwa ngumu zaidi kwa sababu baadhi ya mabadiliko yatahitaji kura ya maoni kwa upande wa Zanzibar. Na hata kama ingewezekana kuyarudisha kwenye Mamlaka ya Muungano, matatizo na kero za Muungano zisingemalizika bali zingeongezeka.

Njia ya pili ni kuyakubali mabadiliko yaliyofanywa na kuongeza mengine ambayo yataipa Zanzibar uhuru wa kuamua *(Autonomy)* mambo yake ya uchumi. Hili linawezekana lakini likitokea ni lazima Tanganyika nayo ipate uhuru wa kuamua *(Autonomy).* Kwa maana hiyo kutakuwa na Serikali tatu na Serikali ya Muungano itabaki na mambo ambayo itakuwa na madaraka nayo kamili.

Kutokana na malalamiko yanayotolewa na wananchi wa pande zote mbili ambayo Serikali zote mbili zimeshindwa kuyapatia ufumbuzi wa kudumu kwa muda mrefu, baadhi ya wananchi wa Zanzibar wanauona Muungano kuwa ni kero na baadhi ya wananchi wa Tanzania Bara wanauona Muungano kuwa ni mzigo.

Aidha, wananchi wa Tanzania kwa kutumia Tume mbalimbali zilizoundwa kwa mfano Tume ya Nyalali na Kamati ya Kisanga walipendekeza Muungano wa Serikali tatu. Maoni hayo ya wananchi yamependekezwa tena mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Pamoja na maoni hayo, Tume pia, ilipitia taarifa mbalimbali za utafiti na uzoefu wa nchi nyingine zenye changamoto za muungano. Katika kutoa mapendekezo hayo yenye lengo madhubuti la kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ilizingatia ya wananchi yanayoakisi matakwa na matarajio yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tume nayo ilifanya utafiti na kuandaa ripoti juu ya Muungano inayopatikana katika ripoti za utafiti kuhusu Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tatizo la msingi kabisa kwa Muungano wa Tanzania ni la muundo wenyewe wa Muungano wa Serikali mbili badala ya tatu ambao umetoholewa kutoka mifano ya miungano ambayo imeundwa kutokana na chimbuko la ukoloni kama ilivyokuwa kwa

United Kingdom of Great Britain na Northern Ireland pengine kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Tanganyika wakati huo alikuwa ni Rolland Brown ambaye ni Mwingereza.

Hali kadhalika, Muungano kama huo ulindwa Shirikisho la Malaysia ambalo lilijumuisha nchi ya Singapore ambayo baada ya muda mfupi ilijitoa.

Takwimu za Tume zimeonyesha kwamba kwa upande wa Tanzania Bara, 13% walipendelea Serikali moja, 24% walipendekeza Serikali mbili na 61% walipendekeza Serikali tatu. Kwa upande wa Zanzibar, 34% walipendekeza Serikali mbili na 60% walipendekeza Muungano wa mkataba na 0.1% (watu 25) walipendekeza Serikali moja.

Aidha, taasisi nyingi kama vyama vya siasa kwa mfano Chadema, CUF, NCCR Mageuzi;asasi za kiraia kwa mfano Legal and Human Rights Centre; - jumuiya za kidini kama Baraza la Maaskofu Tanzania, BAKWATA, Pentecost Council of Tanzania, Christian Professionals of Tanzania, Shuraa ya Maimamu, Baraza la Maimamu Zanzibar; , jumuia za wanasheria kama Zanzibar Law Society na Tanganyika Law Society, Law Academics; jumuia za wasomi; jumuia za wafanyakazi Zanzibar Trade Union ZATU, na Tanzania Union TUCTA, zilipendekeza muundo wa Serikali tatu.

Baadhi ya taasisi za kiserikali ama moja kwa moja au kwa tafsiri ya mapendekezo yao, pia zilipendekeza serikali tatu.

Kwa mfano, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lilipendekeza kuwepo kwa mamlaka huru ya Zanzibar, Mamlaka huru ya Tanganyika na Mamlaka ya Muungano na iwekwe wazi maeneo, uwezo, nguvu, utendaji na mipaka ya kila mamlaka; kwa upande wa Makatibu Wakuu wa Zanzibar hali kadhalika kwa tafsiri ya mapendekezo hayo pia yalijitokeza kama vile lilivyoona Baraza la Wawakilishi.

Aidha, maoni yaliyotolewa na Ofisi ya Makamu Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zimependekeza mfumo wa Serikali tatu ili kuondoa kero za Muungano. Aidha, mamlaka ya Mapato Tanzania imependekeza kuwepo kwa Serikali tatu ili kutoa majibu ya kero zilizopo na kuleta utulivu zaidi ilimradi upangiliwe vizuri.

Hivyo, muundo unaopendekezwa umezingatia kwamba: unaeleweka kwa urahisi katika ugawanyaji wa madaraka kati ya Mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa kila Mamlaka kuwa na Serikali yake; unawezesha nchi Washirika kubaki na utambulisho wao wa kihistoria na kiutamaduni, na hivyo, kuondoa hisia ya Zanzibar kumezwa na Tanganyika ndani ya Muungano na Tanganyika kupoteza utambulisho na uwepo wake; unasaidia kila upande wa Muungano kuendesha mambo yake yasiyo ya Muungano kwa kadri inavyoona inafaa kwa maslahi ya maendeleo na ustawi wa watu katika eneo lake na hivyo kuondoa visingizio dhidi ya muungano; unaleta uwajibikaji kwa kila Serikali ya Nchi Mshirika na kuchochea kasi ya maendeleo na kukuza maslahi ya watu katika eneo husika na unapanua zaidi demokrasia kwa kupeleka madaraka kwa wananchi kujiamulia mambo yao.

Rasimu hii inaweka vyombo na mfumo wa utatuzi wa mambo ya muungano na pia kuwepo na utaratibu wa kikatiba wa ushirikiano wa mambo yasio ya Muungano. Pia Rasimu inaweka dhahiri dhamana na majukumu na kujua nani mwenye dhamana gani

na mamlaka gani na kwa mipaka gani. Hivyo maamuzi yoyote yanaweza kuwa ya kutabirika na sio ya kushtukiza kama ilivyo hivi sasa na kuongeza tija na ufanisi jambo ambalo litaimarisha Muungano.

Kwa mujibu wa maoni wananchi wengi waliopendekeza Muungano wa Serikali moja, walisema isipowezekana basi iwe ni Serikali tatu.

**Ibara ya 61: Vyombo vya Utendaji vya Jamhuri ya Muungano.**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inabainisha kuwepo kwa mihimili mikuu ya dola ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama na majukumu na wajibu wa kila mhimili. Vyombo hivyo vinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa kufuata masharti yaliyomo katika Katiba hii.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kutambua kikatiba kuwepo kwa mihimili mitatu ya dola na mamlaka zao za kiutendaji ndani ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, madhumuni mengine ni kutenganisha majukumu na mamlaka ya kila mhimili ili kuimarisha misingi ya udhibiti na urari wa madaraka (*checks and balances).*

Lengo lingine ni kuviweka vyombo hivi chini ya Katiba kwa kufuata masharti yaliyomo ndani yake.

**c. Sababu ya Mapendekezo**

Dhana ya mgawanyo wa madaraka ni moja ya misingi muhimu ya kikatiba na ukatiba wa nchi inayoheshimu misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji wa serikali kwa raia. Hivyo, Ibara hii inaimarisha dhana hiyo ili kujenga taifa linaloongozwa kwa misingi ya uwajibikaji kwa wananchi na kuheshimu haki za binadamu. Vile vile kuifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa imara kisiasa na yenye mfumo wa utawala unaoeleweka na kutabirika.

Dhana hii imekuwepo katika katiba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ingawa wakati wa kipindi cha utawala wa chama kimoja (1965-1992) mihimili yote hii iliwekwa chini ya mamlaka ya chama tawala na kutekeleza maamuzi ya chama hata kama yalikuwa hayaendani na matakwa ya Katiba.

Na baina ya mihimili mitatu hiyo ya dola, mhimili wa utendaji ulipewa mamlaka makubwa zaidi kuliko mihimili mengine miwili iliyobakia.

**Ibara ya 62: Mamlaka ya Serikali ya Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaipa Serikali ya Jamhuri ya Muungano mamlaka kamili juu ya usimamizi na utekelezaji wa mambo yote ya Muungano iliyokabidhiwa chini ya Katiba hii.

Ibara hii inatoa nafasi kwa Serikali ya Muungano kutekeleza mambo yasiyo ya Muungano itakayokabidhiwa na Nchi Mshirika kwa hiyari na makubaliano kwa masharti

maalum. Katika utekelezaji wa shughuli zake kwa Mambo ya Muungano au yasiyo ya muungano, Serikali ya Muungano italazimika kufuata masharti ya Katiba hii.

**b. Madhumuni na lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya Kikatiba kwa Serikali ya Muungano katika kutekeleza Mambo ya Muungano. Pia kuweka fursa ya kikatiba kwa Nchi Washirika kuweza kukasimu mamlaka yake kutekelezwa na Serikali ya Muungano kwenye mambo yasiyo ya Muungano.

Kuiwezesha Serikali ya Shirikisho kutekeleza majukumu yake kiufanisi katika Mambo ya Muungano. Vile vile ni kuweka msingi wa Serikali kutii Katiba katika utendaji na shughuli zake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ibara hii imezingatia kuwa katika miundo ya muungano inayotenganisha mambo ya muungano na mambo yasiyo ya muungano, huyaweka mamlaka yote ya mambo ya muungano kwenye serikali ya muungano. Katika usimamizi na utekelezaji wake mamlaka hayo hayaruhusiwi kukasimiwa au kuingiliwa na mshirika yoyote wa muungano. Huo ndio ukuu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano na Serikali yake katika mamlaka ya Muungano.

Sababu nyingine ni kuweka msingi kwa Jamhuri ya Muungano kusimamia kikamilifu wajibu wake katika Muungano.

Kwa mara ya kwanza Rasimu hii inajenga msingi wa ushirikiano (*cooperation*), mshikamano (*solidarity*) na kufikia kina cha ufanisi (*subsidiarity*) kwa kuweka kipengele cha Nchi Mshirika kuwa na fursa ya kuiomba Serikali ya Muungano kutekeleza mamlaka yaliyo chini yake kuweza kufikia malengo na matakwa yake kwa manufaa na ustawi wa wananchi.

Dhana hii inasaidia zaidi kujenga muungano kwa vile inaweka mkazo kwa Serikali Jamhuri ya Muungano kutafuta kila njia kufanya kazi na Serikali za Nchi Washirika, na pia Serikali za Nchi Washirika kuwa karibu zaidi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia kujenga na kudumisha utamaduni wa Nchi Washirika kuweza kushirikiana baina yao.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Rasimu ya Katiba mamlaka ya Serikali ya Tanganyika au Serikali ya Zanzibar ni kwa mambo yasiyo ya Muungano tu na siyo vinginevyo.

## Ibara ya 63: Mambo ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Katiba inaainisha mambo saba (7) ya Muungano kama ifuatavyo:

1. Katiba na Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2. Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
3. Uraia na Uhamiaji.

4. Sarafu na Benki Kuu.
5. Mambo ya Nje.
6. Usajili wa Vyama vya Siasa.
7. Ushuru wa Bidhaa na Mapato yasiyo ya Kodi yatokanayo na Mambo ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha na kutofautisha Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano ili kuleta ufanisi wa utekelezaji. Kwa kupunguza mambo ya Muungano kunaondoa kero zilizotokana na kuongezeka kwa Mambo mengi ya Muungano.

Kurudi kwenye mambo ya msingi ya muungano yenye sifa ya kutambulisha mamlaka ya dola (*Sovereign Functions*) na kwenye dhana ya asili ya Waasisi wa Muungano kama yalivyoainishwa kwenye Hati ya Muungano ya 1964. Muhimu zaidi ni kuweka mipaka ya kikatiba kwa mamlaka ya muungano ambayo hayastahiki kuchezewa au kuingiliwa kuepukana na uvunjifu wa katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kwa mujibu wa Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, Mambo ya Muungano yaliyopendekezwa ni saba badala ya 22 yaliyoorodheshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mambo mengine yaliyozingatiwa katika Rasimu hii ni kuhakikisha mambo makuu ya kidola (*Sovereign Functions*) yanabaki chini ya Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano. Mambo hayo ndiyo yanayoitambulisha nchi katika medani za sheria na mahusiano ya kimataifa na ndani ya nchi hayana budi yawe ya Muungano.

Rasimu hii imezingatia mambo 11 ya awali yaliyokuwemo katika Hati ya Makubaliano ya Muungano na Katiba ya awali ya Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo, masuala ya Bandari na Usafiri wa Anga ambayo ni Mambo ya awali ya Muungano yameachwa katika orodha mpya ya Mambo ya Muungano kwa sababu hayajawahi kutekelezwa kimuungano kwa makubaliano ya Serikali mbili. Mambo mengine ya Muungano yaliyoachwa ni yale 11 yaliyoongezwa baadaye ambayo ndio yamekuwa chanzo cha malalamiko na kero za Muungano.

Kigezo kilichotumika katika kuamua Mambo ya Muungano katika Rasimu hii ni pamoja na kuhalalisha makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kwa hatua zilizochukuliwa na upande mmoja wa Muungano kutekeleza au kutokutekeleza Mambo ya Muungano bila ya kubadilisha Katiba.

Mapendekezo haya yanakidhi haja ya wananchi walio wengi waliotoa maoni yao ya kutaka kuondoa kero za Muungano ambazo kwa kiasi kikubwa zimetokana na muundo wa Serikali mbili kwa kukosekana kwa mipaka iliyo wazi baina ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano.

Jumla ya maoni 2,452 yalitolewa katika pande zote mbili za Muungano juu ya Orodha ya Mambo ya Muungano. Maoni 6 katika kila 10 (61.9 asilimia) yalitaka mambo ya Muungano yapunguzwe hasa kutoka Tanzania Zanzibar. Waliotaka mambo yapunguzwe kutoka Tanzania Zanzibar ni asilimia 79.3 na kutoka Tanzania Bara ni asilimia 44.

Rasimu inapendekeza katika hali mpya ya kuwa na mambo machache ya Muungano ambayo yataweka mipaka baina ya Serikali zote tatu

**Ibara ya 64: Nchi Washirika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua kikatiba Nchi Washirika wa Muungano kuwa ni Tanganyika na Zanzibar.  Pia inaweka mamlaka zao za utekelezaji kwa mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Nchi Washirika katika serikali zao kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba zao.

Vile vile ibara  inaainisha hadhi na haki sawa za Nchi Washirika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara ni kutambua kuwepo kwa Nchi Washirika zinazounda na kuipa uhalali wa Jamhuri ya Muungano.

Lengo la Ibara hii pia ni kuainisha hadhi na haki ya kila Nchi Mshirika ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia usawa na ukweli kwamba Muungano huu ni wa hiari. Hadhi na haki inayotajwa hapa siyo ya usawa wa mahitaji na kuchangia bali ya usawa na uhuru kwa maana kuwa kila moja ilikuwa nchi kamili ilipojiunga na Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua Nchi Washirika katika Ibara ya 4, 34, 64, 102. Aidha Ibara ya 151 inatamka kuwa Tanzania Bara maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika na Tanzania Zanzibar maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa ni eneo la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Hivyo moja ya sababu ya Ibara hii ni kuendeleza dhana hii ya kihistoria.

Sababu nyingine ni kuweka wajibu wa msingi wa kuleta maendeleo na usatwi wa watu wa kila upande wa Muungano chini ya mamlaka ya Nchi Mshirika husika. Aidha, sababu ya Ibara hii pia ni kuitikia madai ya wananchi kutaka utambulisho rasmi na wa wazi kwa kila Nchi Mshirika katika Muungano. Takwimu za maoni ya wananchi kuhusu suala hili zimo katika Ripoti ya Tume, "Takwimu za Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi Kuhusu Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania", Sura ya Nne, Eneo la Muungano, hoja 4.2.2, Hadhi za Washirika wa Muungano kwa Sehemu Mbili za Muungano.

**Ibara ya 65: Mamlaka ya Nchi Washirika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua Mamlaka ya Nchi Washirika katika utekelezaji wa mambo yote yasiyo ya Muungano yaliyo chini ya mamlaka zao. Ibara inabainisha kuwa katika utekelezaji wa mamlaka hayo, Nchi Mshirika itazingatia misingi ya ushirikiano baina yao. Aidha, Ibara inaelekeza kuwa Nchi Washirika zinaweza kuanzisha mahusiano au mashirikiano yoyote ya kikanda au kimataifa kwa mambo yasiyo ya

Muungano na zinaweza kuomba ushirikiano kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kufanikisha suala hilo.

Ibara vile vile inaeleza kuwa katika kutimiza mamlaka ya Nchi Washirika kwenye masuala ya kikanda na kimataifa kila moja peke yake au kwa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano, zitafuata utaratibu uliowekwa kwenye Katiba kupitia vyombo vilivyomo ndani ya Katiba hii. Vyombo hivyo ni Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali na Mawaziri Wakaazi, pamoja na sheria itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa madhumuni hayo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuainisha mamlaka na haki ya kila Nchi Mshirika wa Muungano ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano; kuziwezesha Nchi Washirika kusimamia na kutekeleza mambo yasiyo ya Muungano katika maeneo yao; pia kuziwezesha kikatiba Nchi Washirika wa Muungano kutekeleza masuala ya ushirikiano wa kimataifa katika maeneo yasiyo ya Muungano na kuepusha migongano inayoweza kutokea kati ya Nchi Washirika na Jamhuri ya Muungano au Washirika wa Muungano wenyewe kwa wenyewe.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katiba hii inabainisha kuwa Nchi Washirika wa Muungano zitakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yasiyo ya muungano yanayohusu Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa juu ya mambo yote yasiyo ya muungano yanayohusu Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, Nchi Washirika wa Muungano zitakuwa na mamlaka kamili ya kutekeleza mambo yote yasiyo ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuanzisha ushirikiano na jumuiya au taasisi yoyote ya kikanda au kimataifa kuhusiana na mambo hayo kwa mujibu wa Katiba. Aidha, Rasimu inapendekeza Nchi Washirika kuruhusiwa kuomba ushirikiano kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kufanikisha suala hili. Jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika suala hili ni kufanikisha utekelezaji wake.

Mapendekezo haya yamezingatia kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni taifa moja lenye dola moja. Aidha, yanatambua hadhi na haki sawa za Nchi Washirika wa Muungano na kuweka utaratibu utakaorahisisha na kuharakisha juhudi za kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi katika Jamhuri ya Muungano. Mapendekezo haya pia yanaweka msingi wa mshikamano (*Solidarity Principle*) baina ya Nchi Washirika.

Moja ya sababu za mapendekezo haya ni hoja kwamba Zanzibar inastahili kuwa na mamlaka ya kujihusisha na masuala ya kimataifa ili kukuza maslahi yake. Inadaiwa kuwa hali ya sasa ambapo masuala yote ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa ni masuala ya Muungano, Zanzibar inapungukiwa na fursa za kujistawisha kimaendeleo. Hivyo, imeonekana haja ya kutenganisha masuala ya mambo ya nje (*International Relations*) nay ale ya ushirikiano wa kimataifa (*International Co operation*) ili kutoa fursa pana kwa Nchi Washirika kushughulikia ustawi wa kimaendeleo wa maeneo yao.

Sababu nyingine ni kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitakuwa ya kwanza duniani kuruhusu washirika wake kuwa na mashirikiano ya kimataifa. Nchi za Marekani,

Ujerumani, Canada, Austria na Uswisi zimeruhusu washirika wao wa Muungano kujihusisha na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwa njia mbalimbali kama vile kwenye masuala ya mikataba, kufanya ziara, kutafuta na kutoa misaada na kuwasiliana na wadau mbalimbali wa kimataifa.

Washirika wa Muungano wamekuwa wakiendesha shughuli za uhusiano wa kimataifa moja kwa moja kwa hadhi zao kama Washirika wa Muungano kwa mambo yaliyopo kwenye mamlaka zao na siyo shughuli za asili za nchi huru kama vile ulinzi na usalama (*strategic and security matters*). Mara nyingi masuala hayo yamekuwa yakihusiana na masuala yanayo wakabili katika maeneo yao ya utawala kama vile utamaduni, mazingira, biashara na masuala ya maendeleo kwa jumla.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 66 na 67.

**Ibara ya 66: Mahusiano kati ya Nchi Washirika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka misingi ya ushirikiano na mashauriano baina ya Nchi Washirika wenyewe kwa wenyewe au kati yao na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika utekelezaji wa shughuli zao kwa lengo la kukuza na kulinda maslahi ya taifa na maendeleo ya wananchi.

Ushirikiano na mashauriano hayo ni katika mambo ya uongozi, utawala, vyombo vya uwakilishi na mahakama, na yatekelezwa kwa kuzingatia na kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inalenga kuweka utaratibu wa kikatiba utakaowezesha usimamizi na ushirikiano baina ya Nchi Washirika wenyewe, na kati yao na Jamhuri ya Muungano.

Lengo jingine ni kukuza umoja na mtangamano wa kitaifa kwa kuzingatia maslahi ya taifa na ustawi wa wananchi.

Kuwezesha Nchi Washirika kutambua na kuhamasisha wananchi wao kutumia fursa zilizopo katika pande zote mbili za Muungano na shughuli hizo zikifanywa na wananchi wenyewe.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katika nchi yenye mfumo wa shirikisho au Muungano, Nchi Washirika na Serikali ya Muungano zinawajibika kushirikiana na kushauriana ili kuweka misingi ya kuwahudumia wananchi wote kwa usawa, haki, ulinganifu na uwiano katika masuala ya ustawi wa jamii na maendeleo. Kwa mujibu wa Rasimu hii, vyombo vya kushughulikia suala hili ni pamoja na Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali na Mawaziri Wakaazi.

Sababu ya mapendekezo haya ni kuepusha migongano katika uendeshaji wa shughuli za dola na serikali kwa kuwa na vyombo na taasisi vinavyosimamia na kuratibu uhusiano na ushirikiano wa pande husika.

Sababu nyingine ni kukuza na kulinda maslahi na ustawi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano kwa ujumla wao lakini bila ya serikali za Nchi Washirika kuingiliana.

**Ibara ya 67: Mawaziri Wakaazi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha nafasi za Mawaziri Wakaazi watakaoteuliwa na nchi zao na kua na ofisi makao makuu ya Muungano. Ibara pia inaainisha majukumu yao ambayo ni kushughulikia mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu ushirikiano au mahusiano ya kimataifa; na kuwa kiungo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika na baina ya Nchi Washirika wenyewe kwa mambo ya Muungano na yale yasiyokuwa ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka chombo cha kikatiba chenye dhamana ya kushughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano ili kuunganisha, kuratibu na kusimamia shughuli za kila siku. Ibara pia inalenga kujenga utamaduni wa kiutawala utakaoleta ukaribu na ushirikiano katika Jamhuri ya Muungano na hivyo kujenga imani juu ya maamuzi yanayofanywa katika ngazi hiyo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Moja ya sababu za mapendekezo haya ni kurahisisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Nchi Washirika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Vilevile ni kufuata uzoefu wa baadhi ya nchi zenye muundo wa shirikisho wa kuwa na Mawaziri Wakaazi au Ofisi za Uwakilishi wa kila Nchi Mshirika wanaoratibu na kusimamia mambo ya shirikisho na maslahi ya Nchi Washirika ndani ya Muungano. Mfano wa nchi hizo ni Ujerumani na Canada. Jumuia ya Umoja wa Ulaya nayo pia ina utaratibu kama huo. Aidha, sababu nyingine ni kuendeleza utaratibu ulioanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuwa na Ofisi Jijini Dar-es-Salaam ambayo ni Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**Ibara ya 68: Mamlaka ya Wananchi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inasema kuwa wananchi ndio chimbuko kuu la mamlaka ya nchi. Hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itapata mamlaka yake kutoka kwa wananchi kupitia uchaguzi wa kidemokrasia utakaoendeshwa na kusimamiwa na chombo kitakachopewa mamlaka na Katiba. Aidha, Nchi Washirika zitapata mamlaka kupitia uchaguzi wa kidemokrasia utakaoendeshwa na kusimamiwa na vyombo vitakavyopewa mamlaka chini ya Katiba zao. Serikali za Nchi Washirika, katika kutekeleza mamlaka yao, zitawajibika kustawisha mamlaka ya wananchi kwa kugatua madaraka kwa Serikali za Mitaa zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba zao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua ukuu wa wananchi kikatiba na kuziwajibisha mamlaka zote kwa wananchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kuwa mamlaka kuu ya dola na nchi ni wananchi na sio watawala au vyombo vya serikali na vyote hivyo viko chini ya wananchi kwa mujibu wa katiba.

Katika historia ya nchi nyingi za Kiafrika dhana ya ukuu wa wananchi ilififishwa na badala yake ikakuzwa dhana ya ukuu wa utawala na vyombo vya serikali. Mapendekezo haya ni kurudisha dhana ya ukuu wa wananchi katika uendeshaji wa nchi. Ili kuweza kutekeleza dhana ya Mamlaka ya wananchi ni vyema Katiba ikaanisha vyombo vya kikatiba kama uwepo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambavyo ndivyo vyenye uwakilishi wa wananchi moja kwa moja na ndivyo vyenye wajibu wa kutoa huduma moja kwa moja kwa wananchi.

Sababu ya mapendekezo ni kuendeleza maudhui ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Ibara ya 9 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 zinazotambua mamlaka ya wananchi ingawa katika utekelezaji bado mwelekeo umekuwa zaidi kwenye mamlaka ya watawala na vyombo vya serikali.

Muhimu zaidi mapendekezo haya ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka Katiba ionyeshe wazi kuwa Mamlaka ya nchi yanatokana na wananchi wenyewe na kwamba, vyombo vya Serikali vimewekwa na wananchi kwa lengo la kuwatumikia.

**Ibara ya 69: Wajibu wa Kuulinda Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, inaweka wajibu kwa kila raia, viongozi wakuu wenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano wakiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha Muungano. Kwa hiyo kila kiongozi Mkuu kabla ya kushika madaraka yake ataapa kuutetea na kuudumisha Muungano.

Aidha, Ibara pia inaainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa atakayeshindwa kutekeleza wajibu huu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutambulisha kuwepo kwa Muungano katika maisha ya taifa letu na kujenga uzalendo na mshikamano; na hivyo, kuuthamini, kuulinda na kuutetea Muungano huo wa hiari baina ya raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia umoja wao, udugu, urafiki na mahusiano yao ambayo yana uhusiano ya muda mrefu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za kuwepo kwa Ibara hii ni kusisitiza wajibu wa viongozi wenye dhamana ya juu ya uongozi wa nchi kuuheshimu na kuusimamia Muungano kwa kila hali ili kuuendeleza, kuuhuisha na kuudumisha.

Vilevile ni kutambua kuwa Muungano huu wa hiari ni wa wananchi wenyewe na viongozi wao lazima wautii na wauheshimu. Uzoefu umeonyesha kuwepo kwa uvunjaji

wa Katiba kwa viongozi kukubaliana masuala kadhaa bila ya kuwashirikisha wananchi kwa makusudi au vinginevyo.

# SURA YA SABA

## SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

## SEHEMU YA KWANZA

## SERIKALI, RAIS, MAKAMU WA RAIS NA BARAZA LA MAWAZIRI

### *(a) Serikali*

### Ibara ya 70: Serikali ya Jamhuri ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelezea kuwepo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakayoundwa na Rais, Makamu wa Rais na Mawaziri ambao watahusika na utekelezaji wa Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hifadhi ya Katiba. Aidha, inampa uwezo Rais wa kutekeleza majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yeye mwenyewe au kwa kukasimu madaraka hayo kwa Makamu wa Rais au watu wenye madaraka kwenye utumishi wa Serikali ya Jamhuri kama ilivyoruhusiwa na Katiba.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka mhimili wa utendaji (*The Executive*) katika mfumo wa dola. Pia kutambua mamlaka ya Mkuu wa Serikali katika kutekeleza mambo ya utendaji yeye mwenyewe au kwa kukasimu madaraka yake.

Ibara hii pia inatambua mamlaka ya mihimili mingine ya dola yaani Bunge na Mahakama katika uwezo wao wa kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria kwa watu au mamlaka nyingine yoyote ambayo si Rais.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza msingi wa kikatiba wa mgawanyo wa madaraka kwa kutambua na kuanzisha ndani ya katiba mhimili wa utekelezaji wa shughuli za dola, na kuweka wazi kwamba mhimili huu unaundwa na Rais, Baraza la Mawaziri na Utumishi wa Serikali. Vile vile ni kutambua mipaka ya kila mhimili wa dola katika kutekeleza majukumu yake.

Rasimu hii ya Katiba kwa mara ya kwanza inauweka Utumishi wa Umma kuwa ni sehemu muhimu ya mhimili wa dola na siyo kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuwa mhimili wa utendaji ni Rais na Baraza la Mawaziri.

Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuendelea kuwepo kwa mfumo wa Jamhuri inayoongozwa na Rais Mtendaji ambaye ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Amiri Jeshi Mkuu. Pia, ni kuzingatia matakwa ya kifungu cha 9(2)(b) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 yaliyoitaka Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuzingatia kuwepo kwa Serikali.

### *(b) Rais*

**Ibara ya 71: Rais wa Jamhuri ya Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kikatiba kuwepo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni alama na taswira ya Jamhuri ya Muungano na watu wake, alama ya umoja na uhuru wa nchi na mamlaka yake; na atakuwa na dhamana ya kukuza na kuhifadhi umoja wa kitaifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha kikatiba kuwepo kwa Rais mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia, ni kubainisha na kuyaweka wazi mamlaka yake akiwa Mkuu wa Nchi, mamlaka yake akiwa ni Amiri Jeshi Mkuu na mamlaka yake akiwa ni Mkuu wa Serikali. Madhumuni mengine ni kutofautisha mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mamlaka ya Wakuu wa Nchi Washirika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mfumo wa nchi yetu ni wa Jamhuri na siyo wa Kifalme au vinginevyo na kwa hivyo ni lazima uongozwe na Rais wa kuchaguliwa. Aidha, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inataja mfumo wa kiutawala wa kijamhuri kuwa ni moja ya misingi muhimu ya kuzingatiwa na kuboreshwa katika Katiba Mpya.

Sababu ya kupendekeza kuendelea mfumo huo wa kuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye mamlaka kamili yasiyogawika kwa mwingine ambayo ni ya Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na pia Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye Mamlaka kamili kwa mambo yote yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano, wakati marais wa Nchi Washirika watakuwa wakuu wenye mamlaka kamili kwa Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar kwa mambo yasiyo ya Muungano. Mfumo huu wa Rais kuwa Mkuu wa Serikali unafuatwa na nchi kadhaa duniani ikiwemo Brazil, Marekani, Mexico, Nigeria, Ujerumani na Venezuela.

Sababu nyingine ni kufafanua utekelezaji wa madaraka ya Rais akiwa katika nafasi zake tatu za Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

**Ibara ya 72: Madaraka na Mjukumu ya Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba imefafanua kwa upana madaraka na majukumu ya Rais katika nafasi zake tatu; akiwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Amiri Jeshi Mkuu. Aidha, Ibara hii inaweka masharti kwa Rais kuepuka kujinasibisha kwa namna yoyote na chama chochote cha siasa au kundi lolote la jamii kwa namna ambayo itaathiri umoja wa wananchi wakati akiwa madarakani.

## b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka wazi na kuainisha kwa kina mipaka ya madaraka na majukumu ya Rais katika nafasi zake tatu tofauti katika utekelezaji wa kazi zake.

Lengo jingine ni kuweka masharti yanayomzuia Rais wa Jamhuri ya Muungano kujinasibisha na chama chochote cha siasa au kundi lolote kwa namna ambayo itaathiri umoja wa wananchi.

## c. Sababu za Mapendekezo

Sababu moja ya mapendekezo haya ni kuendana na Katiba nyingine duniani ambazo zinatambua nafasi hizo tatu tofauti za mamlaka ya kiongozi wa nchi na zinatenganisha shughuli hizo kwa kufanywa na watu mbali mbali au kuwekwa chini ya mtu mmoja lakini kila nafasi ikiwa na mipaka inayoeleweka.

Kwa hali hiyo, Mkuu wa Nchi dhamana yake ni alama ya umoja wa taifa na wananchi wake; Amiri Jeshi Mkuu dhamana yake ni ulinzi na usalama wa nchi, watu na mali zao; na Kiongozi wa Serikali dhamana yake ni usimamizi na uendeshaji wa kila siku wa shughuli za Serikali.

Aidha, Ibara hii ni kuzingatia na maoni ya wananchi ambao walitaka kutenganishwa kwa shughuli za Serikali na zile za chama, Rais kutotumia rasilimali za Serikali kwa shughuli za chama na pia kuondoa uwezekano wa Rais kuegemea upande wa chama chake katika kufanya maamuzi na hivyo kuwagawa wananchi katika makundi.

## Ibara ya 73: Utekelezaji wa Madaraka ya Rais

## a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua utekelezaji wa madaraka ya Rais ya uteuzi wa nafasi mbalimbali za Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali ambao utathibitishwa na Bunge. Pia Ibara inaeleza kuwa katika kuanzisha au kufuta nafasi za madaraka, Rais atapaswa kuzingatia ushauri wa Mamlaka za Serikali, Bunge au Mahakama.

## b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa utekelezaji wa madaraka ya Rais ya uteuzi wa nafasi mbalimbali katika Utumishi wa Umma na kuainisha vyombo vya kikatiba vitakavyomsaidia katika uteuzi wa nafasi hizo. Aidha, madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu kwamba, viongozi na watumishi wa umma watakaoteuliwa na Rais watokane na mapendekezo ya tume au kamati mahsusi za uteuzi za kikatiba na kuthibitishwa na Bunge ambalo ndicho chombo kinachowawakilisha wananchi wote.

## c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuruhusu kikatiba kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali Amiri Jeshi Mkuu aendelee kuwa na madaraka ya uteuzi wa viongozi wa ngazi za juu Serikalini lakini ashauriwe na taasisi na vyombo vyengine mahsusi vya umma na baadhi ya viongozi anaowateua wathibitishwe na Bunge kabla ya kushika madaraka.

Sababu nyingine ni kuondoa changamoto mbalimbali zinazotokana na mfumo wa sasa ambapo Rais ana mamlaka yasiyo na udhibiti ya kuteua Viongozi mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Changamoto za mfumo huu ni pamoja na:

1. Uwezekano wa uteuzi kufanyika kwa upendeleo na rushwa bila kuzingatia uwezo na sifa stahili. Kwa mfano, kwa sababu ya mfumo huu, Rais wa zamani wa Marekani, James A. Garfield, aliuawa mwaka 1881 na mtu ambaye alitegemea kuteuliwa lakini akanyimwa nafasi kinyume cha matarajio yake kutokana na upendeleo na rushwa. Baada ya tukio hilo sheria ilitungwa ili kumpunguzia Rais madaraka ya uteuzi na kumbakishia nafasi chache kwa ajili ya viongozi wa ngazi za juu tu.
2. Uwezekano kwa Rais kufanya uteuzi kwa kupotoshwa na washauri wake hasa kukiwa na idadi kubwa ya wateule.
3. Uwezekano wa Rais kutumia muda mwingi kwenye uteuzi badala ya kufanya kazi nyingine muhimu.
4. Uwezekano wa wateuliwa kutowajibika kwa kujinasibisha kuwa wote ni wateule wa Rais.
5. Uwezekano wa kushusha ufanisi katika utendaji wa kazi kwa kuwa Rais hayupo karibu na wateule wake wengi kuweza kuwasimamia kinidhamu na kuwawajibisha.

Mapendekezo haya pia yamezingatia maoni ya wananchi yaliyotaka Rais awekewe udhibiti katika utekelezaji wa madaraka yake ya uteuzi.

Kwa mujibu wa Katiba ya Ufaransa, Rais amepewa madaraka ya uteuzi wa mabalozi, viongozi wa juu wa majeshi, wakurugenzi mbalimbali wa idara za serikali, wakuu wa taasisi za elimu, wakaguzi wa mahesabu ya serikali na wakuu wa mikoa. Uteuzi huo lazima uthibitishwe na Bunge. Vilevile, mamlaka ya uteuzi ya Rais yanafanyika kwa kushauriana na kamati husika za Bunge. Rais hatafanya uteuzi ikiwa theluthi mbili ya kura za kamati za Bunge zinazohusika zitakataa.

Katika Katiba ya Finland, Rais anamteua Waziri Mkuu, na uteuzi huo huthibitishwa na Bunge. Rais pia anateua Mawaziri wengine kwa ushauri wa Waziri Mkuu. Rais anateua Makatibu Wakuu wa wizara, Mabalozi na viongozi wengine ambao Katiba na sheria zinaona kuwa zinahitaji kuteuliwa na mamlaka ya kipekee ya Rais kama Mkuu na Amiri Jeshi. Rais pia anateua Maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama. Viongozi na watendaji wa dola wengine wanateuliwa na Serikali kupitia mamlaka mbalimbali za nchi.

### Ibara ya 74: Rais Kuzingatia Ushauri

#### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inazingatia wajibu wa Rais kufuata na kuzingatia ushauri, atakaopewa na Mamlaka za nchi ilimradi ushauri huo haukiuki Katiba au Sheria za nchi na kutoa sababu iwapo hakubaliani na ushauri aliopewa na mamlaka husika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya Kikatiba yatakayomlazimisha Rais kufuata ushauri usiokiuka Katiba au Sheria za Nchi.

Lengo pia ni kujenga mfumo wa kitaasisi ambao una wajibu wa kutoa ushauri na ushauri huo kuheshimika na Rais. Hii pia inakusudia kujenga mfumo wa kutabirika (*certainity and continuity*) katika maamuzi na utekelezaji wa shughuli za Serikali.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya kuweka Ibara ni kumtaka Rais kufuata na kuzingatia ushauri utakaotolewa na mamlaka husika kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi. Ibara hii pia imezingatia mapendekezo ya wananchi ambao walitaka maamuzi ya Rais yasitegemee hekima na busara za mtu mmoja pekee.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika maamuzi ya kuendesha nchi.

**Ibara ya 75: Rais Kushindwa Kumudu Majukumu Yake**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kuthibitisha Rais kushindwa kumudu majukumu yake kutokana na maradhi na kuitangaza nafasi hiyo kuwa wazi. Utaratibu huu unahusisha Baraza la Mawaziri, Jaji Mkuu na bodi ya utabibu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuainisha utaratibu wa kikatiba wa kuthibitisha kwamba Rais ameshindwa kumudu madaraka yake kutokana na maradhi.

Lengo pia ni kuweka masharti ya kikatiba ya kujaza nafasi hii muhimu ili kuondoa uwezekano wa Rais kuendelea kukaa madarakani hata kama hana uwezo wa kumudu majukumu yake.

Vilevile ni kuzuia Baraza la Mawaziri peke yao kufanya maamuzi ya kumuondoa Rais mpaka ithibitishwe na bodi ya utabibu ili kuhakikisha kuwa mfumo wa kuondolewa kwake ni wa haki kwa Rais mwenyewe na wananchi waliomchagua.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu kuu ni kutambua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano amechaguliwa kwa kura na kwa hivyo mchakato wowote wa kumuondoa uwe wa wazi na haki kwa Rais mwenyewe na wananchi waliomchagua na kumpa dhamana ya kuwaongoza.

Sababu ya mapendekezo haya ni kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu utaratibu utakaotumika kutangaza nafasi ya Rais ipo wazi endapo itatokea Rais aliyepo madarakani kushindwa kumudu majukumu yake kutokana na sababu za maradhi.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 76 ya Rasimu ya Katiba.

## Ibara ya 76: Utaratibu wa Kujaza Nafasi ya Rais Kabla ya Kumaliza Muda Wake

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa Makamu wa Rais kujaza nafasi ya Rais inapokuwa wazi kwa sababu ya kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za kuwa Rais, kutomudu kazi zake kutokana na maradhi au kuondolewa kwa kushtakiwa na Bunge. Pia, Ibara inaweka utaratibu wa kupatikana Makamu wa Rais mwingine atayechukua nafasi ya Makamu wa Rais ambaye amekuwa Rais.

Vilevile inaweka utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais itakapokuwa wazi kwa sababu yoyote iliyoainishwa katika Katiba.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba utakaopaswa kuzingatiwa wakati wa kujaza nafasi ya Rais itakapokuwa wazi kwa sababu yoyote iliyoainishwa katika Katiba. Utaratibu huu utasaidia kuondoa mgongano na kuweka uhakika wa kujaza nafasi ya Rais pale inapotokea kuwa wazi.

Hilo pia ni kwa nafasi ya Makamu wa Rais.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu moja ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa nafasi ya Rais, aliye taswira ya dola, ina mtu anayeishikilia wakati wote. Pia ni kumfanya Makamu wa Rais kujaza nafasi ya Rais kwa sababu yeye amechaguliwa kuwa mgombea mwenza na Rais kwa tiketi moja.

Sababu nyingine ni muendelezo mfumo kwa makamu wa Rais kuweza kushika nafasi ya Urais wakati inapotokea dharura kwa Rais kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 80.

## Ibara ya 77: Utekelezaji wa Majukumu ya Rais Akiwa Hayupo

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaeleza utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo. Ibara pia imewataja Makamu Rais na kama yeye hayupo ni Waziri Mwandamizi na kama yeye hayupo basi Waziri mwingine yeyote atakayeteuliwa na Baraza la Mawaziri kuwa wanaweza kutekeleza madaraka hayo.

Pia Ibara hii inaeleza kuwa mtu yeyote atakayekaimu nafasi ya madaraka ya Rais hatakuwa na mamlaka katika maeneo ya uteuzi au kufuta uteuzi au jambo jingine lolote ambalo atazuwiwa kulifanya na Rais katika hati ya kukasimu madaraka yake.

**b. Maudhui na Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kukaimu utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo. Utaratibu huu utasaidia ili kuondoa utata wa utekelezaji wa majukumu ya Rais pale inapotokea Rais hayupo.

Pia kuweka mipaka inayozuia mamlaka ya msingi ya Rais kukasimiwa kwa mtu mwingine yeyote na hivyo Rais kulazimika kutokuwa nje ya nchi kwa muda mwingi zaidi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kwamba, majukumu na kazi za Rais zinaendelea kutekelezwa iwapo Rais mwenyewe hayupo. Pia kumzuia anayekaimu madaraka ya Rais kuyatumia vibaya.

Sababu nyingine ni kuepusha mgogoro au mvutano unaoweza kukwamisha utendaji wa Serikali na kutaja wazi mpangilio wa viongozi wanaoweza kukaimu madaraka ya Rais.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 75 na 88 ya Rasimu.

### ***(c)Uchaguzi wa Rais***

**Ibara ya 78: Uchaguzi wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza kuwa Rais atachaguliwa na wananchi wenyewe na kuainisha utaratibu wa kikatiba kuhusu uchaguzi wa Rais kwa kuzingatia sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka mamlaka ya wananchi ya kumchagua Rais na kumpa dhamana ya uongozi wa nchi na kumfanya awajibike kwao. Pia ni njia ya kutimiza matakwa ya demokrasia ya kubadili uongozi kwa vipindi maalum na kwa njia ya uchaguzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka utaratibu wa kidemokrasia wa wananchi kubadili uongozi kwa vipindi vilivyowekwa na kwa njia ya uchaguzi ili kudhihirisha mamlaka yao ya kumuweka na kumuondoa Mkuu wa nchi.

Mapendekezo haya pia yanaendeleza utaratibu wa uchaguzi wa Rais kwa vipindi vilivyoainishwa kikatiba.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 79 na 80.

**Ibara ya 79: Sifa za Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha na kuweka bayana sifa anazotakiwa kuwa nazo mgombea wa nafasi ya Urais na vigezo vinavyomuondolea mtu sifa ya kugombea nafasi hiyo. Sifa hizo ni za uraia wake wa kuzaliwa; sifa binafsi za akili timamu, umri na elimu; sifa za tabia yaani uadilifu, asiye mbaguzi, anayefuauta maadili, uaminifu na mwenendo usiotiliwa shaka na jamii.

Aidha, Rasimu ya Katiba inaruhusu mgombea huru kwa nafasi ya Urais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka vigezo vitakavyowezesha nchi kupata Rais atakayekidhi matakwa ya wananchi kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

Pia, ni kuweka vigezo vya kumuondolea sifa mtu anaetaka kugombea Urais.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuhakikisha kuwa Urais, ambao ni wadhifa mkubwa katika nchi na ni alama na taswira ya nchi, unashikwa na mtu ambaye ni muadilifu na anayeamika, mzoefu wa uongozi, aliyekomaa kifikra na kiutendaji.

Sababu ya kuweka umri wa miaka 40 ni kwamba mgombea atakuwa amekomaa kifikra na kimatendo na kuweza kubeba jukumu la kuwa kiongozi mkuu. Aidha tafiti zimeonesha kuwa umri wa miaka 40 au zaidi ni sifa iliyo katika katiba za nchi nyingine duniani.

Sababu ya mapendekezo ni kukubaliana na maoni ya wananchi kuwa mtu anayegombea nafasi ya urais lazima wazazi wake wote wawe Raia wa kuzaliwa ili kuondoa uwezekano wa Rais kutumia nafasi yake kutimiza nafasi yake kupendelea upande wa mzazi wake ambaye siyo raia wa kuzaliwa.

Sababu ya kuruhusu mgombea huru katika nafasi ya Urais ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka Katiba ikuze na kupanua wigo wa demokrasia na haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Sababu nyingine ni kupata Rais anayeheshimu haki za Binadamu na asiyekuwa na ubaguzi wa rangi, kabila, jinsi, maumbile au hali zozote katika jamii.

Sababu ya kuweka vigezo vinavyomuondolea mtu sifa ya kugombea Urais ni kumpata Rais ambaye sera zake au za chama chake sio za mrengo wa kuligawa taifa kwa misingi ya ukabila, dini, rangi au jinsi ili kulinda umoja wa kitaifa, amani na utulivu.

**Ibara ya 80: Utaratibu wa Uchaguzi wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa uchaguzi wa Rais ambapo mgombea anaweza kudhaminiwa na chama au kuwa mgombea huru. Ibara inaelekeza taratibu kwa kila mgombea kuwasilisha maombi yake kwenye Tume Huru ya Uchaguzi.

Ibara hii pia inaweka kigezo cha kiwango cha asilimia ya kura ambacho mgombea atahitajika kukifikia ili kushinda kiti hicho. Mgombea anatakiwa apate zaidi ya asilimia 50 ya kura zote halali ili awe mshindi. Ikiwa kiwango hicho hakikufikiwa uchaguzi utarudiwa ndani ya siku 60 kwa washindi wawili wa kwanza.

Aidha, ibara inaeleza utaratibu utakaotumika endapo itatokezea kuwa na mgombea mmoja tu halali kwa nafasi hiyo ya Urais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kumpata Rais mwenye uhalali wa kuongoza kwa kupigiwa kura na kuchaguliwa kwa idadi kubwa ya wananchi. Pia inaruhusu mgombea huru wa nafasi hiyo ili kunapanua wigo wa demokrasia.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kurudisha utaratibu uliokuwepo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 wa mgombea Urais kutakiwa kupata kura kwa zaidi ya asilimia 50, utaratibu ambao uliondolewa kupitia Mabadiliko ya 13 ya Katiba ya mwaka 2000. Pia yamezingatia maoni ya wananchi waliotaka Rais anayechaguliwa apate kura zaidi ya asilimia hamsini ili kuonyesha kukubalika kwake na wananchi walio wengi.

Uzoefu wa baadhi ya nchi nyingi ni kuwa ili mtu atangazwe kuwa Rais katika uchaguzi anatakiwa apate zaidi ya nusu ya kura halali zilizopigwa na wananchi.

Kwa kuwa kupiga kura na kupigiwa kura ni haki ya kila raia wa Tanzania na hivyo si vyema kumlazimisha raia anayetaka kugombea uongozi kuwa mwanachama wa chama cha siasa.

Mapendekezo ya kuwa na mgombea huru yamezingatia msingi wa demokrasia kuwa kupiga kura na kupigiwa kura ni haki ya kila raia. Vilevile ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa mgombea huru katika kiti cha Urais. Pia ni kuridhia maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania yaliyoelekeza Bunge kubadili Katiba ili kuweka haki ya mgombea huru. Aidha, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kupitia kesi ya *Rev. Christopher Mtikila v. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* kwamba iwe ndani ya kipindi cha mwaka mmoja iwe imechukua hatu za kuweka mgombea huru katika Katiba.

**Ibara ya 81: Malalamiko Kuhusu Uhalali wa Uchaguzi wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa haki mtu yeyote aliyegombea nafasi ya Urais na kushindwa anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwenye Mahakama ya Juu kupinga uhalali wa mshindi wa kiti cha Urais. Aidha, Ibara hii imelipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria, pamoja na mambo mengine, kuweka muda na utaratibu wa kupokea na kufanya maamuzi kuhusu suala la kuhojiwa uhalali wa Rais.

Vile vile, Ibara inaelekeza kuwa ni mtu aliyegombea na kushindwa ndiye peke yake ambaye atakuwa na haki ya kwenda Mahakamani kudai uhalali wa mgombea aliyeshinda ili kuepusha utitiri wa kesi katika suala hilo.

Aidha, Ibara hii inaelekeza shauri la kupinga matokeo ya Urais liwe limekwishatolewa uamuzi na Mahakama ya Juu kwa kipindi kisichozidi siku 30. Iwapo matokeo hayo ya urais yatatenguliwa, basi uchaguzi utarudiwa ndani ya siku 60 baada ya uamuzi kutolewa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka msingi wa kikatiba wa kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na Rais aliyechaguliwa kihalali. Hii itasaidia kuondoa malalamiko kuhusiana na uhalali wa ushindi wa Rais aliyechaguliwa. Ibara pia inawapa fursa watu wasioridhika na matokeo ya aliyechaguliwa kuwa Rais kuweza uhoji Mahakamani. Madhumuni mengine ni kujenga utamaduni wa kuendesha chaguzi huru, wa wazi na kuondosha vitendo vya rushwa na udanganyifu kwenye chaguzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mapendekezo haya yamezingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka matokeo ya uchaguzi wa Rais yaweze kuhojiwa Mahakamani. Aidha, hii ni fursa inayotoa haki kwa wagombea wanaodhani kuwa aliyetangazwa kuwa mshindi wa nafasi ya Urais hakuwa mshindi halali.

Utaratibu huu utasaidia kuimarisha demokrasia katika mfumo mzima wa uchaguzi wa Rais kwa kuwa unaruhusu chombo kingine yaani Mahakama ya Juu ambacho ni huru kutathmini na kutolewa uamuzi juu ya suala hilo la uhalali wa mtu aliyeshinda nafasi ya Urais na kutoa kauli ya mwisho ili nchi iendelee katika shughuli zake za kawaida.

**Ibara ya 82: Kiapo cha Rais na Muda wa Kushika Madaraka**

**a. Maudhui ya Ibara.**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kuapishwa na muda wa kushika madaraka kwa Rais mteule. Rais ataapishwa na Jaji Mkuu baada ya siku thelathini tangu siku matokeo kutangazwa au Mahakama ya Juu itakapotoa uamuzi wake kuhusu malalamiko ya matokeo. Aidha, Ibara hii inaweka kipindi cha miaka mitano kwa muhula wa Rais. Pia, inatamka kuwa Rais aliyepo atashika madaraka hadi Rais mwingine atakapoapishwa, au atakapofariki dunia au kujiuzulu au atakapoacha kushika nafasi ya madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba hii.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu kiapo cha Rais cha kulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano; na kufuata utawala wa sheria unaoheshimu haki za binadamu. Aidha, ni kuweka ukomo wa Rais kuwa madarakani na kuwapa fursa wananchi kubadilisha viongozi wao kila baada ya kipindi maalum. Hii ni pamoja na kuwapa wananchi fursa na haki ya kuomba ridhaa ya uongozi kwa kuchaguliwa. Lengo jingine ni kuimarisha msingi wa kuwa uongozi ni dhamana na

hivyo kuepuka watu kuhodhi au kurithisha uongozi kwa ndugu na marafiki zao. Aidha, Ibara hii inajenga utamaduni wa kufuata utaratibu wa kikatiba na vyombo vya kikatiba katika kushughulikia malalamiko yao pale ambapo hawajaridhika na matokeo ya uchaguzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuwekwa utaratibu wa kikatiba wa kumuapisha Rais mteule hataapishwa kabla ya kupita siku thelathini tokea siku ya matokeo yalipotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi au siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu. Sababu ya kupendekeza utaratibu huu ni kutoa muda wa kutosha wa kukabidhiana madaraka kati ya Rais anayemaliza muda wake na Rais anayeingia madarakani.

Sababu nyingine za mapendekezo haya ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliosema kuwa kipindi cha siku thelathini kitatoa fursa kwa wagombea wa uchaguzi wa Rais wasioridhika na matokea waweze kupata haki ya kulalamika Mahakamani.

Aidha sababu nyingine ni kumfanya Rais ailinde na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kuutetea na kuulinda Muungano wa Tanzania.

Uzoefu wa Katiba za nchi nyingine kama Kenya, Marekani ambazo Rais wake huapishwa baada ya kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu.

### Ibara ya 83: Haki ya Kuchaguliwa Tena

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka ukomo wa kushika madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Aidha, Ibara hii inaeleza kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Marais wa Nchi Washirika wanaruhusiwa kugombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu ukomo wa kushika madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Pia, ni kuweka msingi wa kung'atuka, kwamba si suala tu la kuondoka madarakani lakini pia ni dhana ya kupokezana madaraka kwa njia za kikatiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya kwanza ni kuendeleza utaratibu nzuri wa sasa uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 iliyoweka ukomo wa Urais na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi Barani Afrika ambapo marais wamepokezana Urais bila ya mivutano wala misuguano kuanzia 1985.

Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa ukomo wa kushika nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, kujenga utamaduni wa kupokezana madaraka kwa njia ya amani, kutoa fursa kwa Watanzania wengine wenye uwezo na

sifa kushika madaraka ya Rais, na kuepusha uwezekano wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kukaa madarakani bila ukomo.

### *(d) Masharti Mahsusi Kuhusu Mamlaka ya Rais*

**Ibara ya 84: Madaraka ya Kutangaza Vita**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba ni inampa Rais madaraka ya kutangaza vita.

Aidha, inaweka utaratibu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kutangaza vita baada ya kupata idhini ya Bunge au kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa. Ibara inaeleza kuwa iwapo Jamhuri ya Muungano imevamiwa au kundi lolote limeanzisha vita ndani ya Jamhuri, atatangaza hali ya vita na atapaswa kulitaarifu Bunge ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya Tangazo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kumpa Rais madaraka ya kutangaza vita, kulinda amani na usalama wa nchi kwa idhini ya Bunge na ushauri wa Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

Lengo jingine ni kuweka utaratibu wa kumuwezesha Rais kusimamia hali ya ulinzi wakati wa dharura.

Vilevile ni kuweka masharti ya kikatiba ya Rais kushirikisha Bunge na vyombo vingine katika kufikia uamuzi wa kutangaza vita.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Rais anapewa madaraka ya kutangaza vita kwa nafasi yake ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye mwenye madaraka ya kuamuru jeshi kuingia katika vita. Masharti ya kikatiba ya Rais kupata idhini ya Bunge kabla ya kutangaza vita yatawezesha kutoa nafasi kwa Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi kulitafakari jambo hilo kwa sababu suala la kuingiza nchi vitani ni kubwa na athari yake kwa taifa kijamii na kiuchumi ni makubwa.

Rais kutangaza vita baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa inatoa fursa ya kwenda vitani katika hali ya dharura ambapo muda wa kuomba idhini ya Bunge haupo.

Uzoefu wa nchi mbalimbali unaonesha kuwa Rais peke yake hana mamlaka ya kuingiza nchi vitani kabla ya kupata idhini ya mamlaka nyingine au inapolazimika kuingiza nchi vitani atapaswa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa mujibu masharti ya Katiba.

Nchini Uganda, Rais analazimika kutoa tangazo la vita baada ya kupata kibali cha Bunge, na kama hali imelazimisha Rais kutangaza vita kabla ya Bunge kutoa kibali, Rais ataomba kibali baada ya hatua hiyo. Uzoefu uliotofauti na mfumo wa Tanzania ni ule wa Marekani ambapo Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kutangaza vita na siyo Rais.

Ingawa hiyo haimzuii Rais wa nchi hiyo kuchukua hatua za kivita kwa jambo linalohitaji uamuzi wa haraka katika kujilinda.

**Ibara ya 85: Madaraka ya Rais Kutangaza Hali ya Hatari.**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa mamlaka kwa Rais kutangaza hali ya hatari au hali ya kuzingirwa kwa eneo fulani la Jamhuri ya Muungano. Aidha, inaweka utaratibu kwa Rais kutangaza hali ya hatari baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuhakikisha kuwa hali ya amani na usalama katika nchi inaendelea. Aidha, ni kumwekea Rais mipaka ya kutumia madaraka ya kutangaza hali ya hatari au kuzingirwa kwa kutumia madaraka hayo, na kukabiliana na vitisho vya ndani na nje na kudhibiti athari mbalimbali yakiwemo majanga ya kimazingira.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia sheria na mikataba ya kimataifa inayoorodhesha sababu mahsusi za kutangaza hali ya hatari kama vile: wakati kuna vita hasa pale nchi imevamiwa; panapokuwa na uasi au vitendo vingine vinavyolenga kuiangusha Serikali iliyochaguliwa kihalali; panapokuwa na majanga makubwa ya kitaifa kwa mfano matetemeko ya ardhi, mafuriko, milipuko ya volkano au panapokuwa na matatizo makubwa ya kiuchumi kiasi cha kuhatarisha uhai wa Taifa.

Sababu ya kumtaka Rais kushauriana na Baraza la Usalama la Taifa kabla ya kutangaza hali ya hatari ni kuweka utaratibu wa kushirikisha mamlaka nyingine halali ili madaraka hayo yasitumike vibaya au kutumiwa bila sababu ya msingi. Hii ni kwa sababu kutangaza hali ya hatari kunaambatana na athari kubwa kwa Taifa na haki za wananchi. Utangazaji wa hali ya hatari unaidhinisha dola kuchukua hatua zisizo za kawaida ambazo zitaathiri haki za kiraia na za kibinadamu. Hivyo basi, madaraka hayo yanapaswa kudhibitiwa. Kwa mfano, uzoefu wa zaidi ya miaka 200 ya Marekani unaonyesha kuwa kuweka madaraka mengi kwa chombo kimoja kunaweza kuleta hatari kwa nchi. Hivyo, ni muhimu kuweka utaratibu wa kudhibiti utumiaji wa madaraka hayo.

**Ibara ya 86: Mamlaka ya Kutoa Msamaha**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano, katika nafasi yake ya Mkuu wa Nchi, kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mahakamani kwa kosa lolote. Pia, inaelekeza kutungwa kwa sheria zitakazoweka masharti maalum ya utekelezaji wa mamlaka hayo.

Ibara pia inaanzisha kikatiba Kamati ya Taifa ya Ushauri itakayokuwa inamshauri Rais kuhusu kutoa msamaha.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kumpa Rais, kwa nafasi yake ya Mkuu wa Nchi, mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa; na kutambua kuanzishwa chombo na utaratibu wa kumshauri Rais kuhusu kutoa msamaha.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa ni muhimu katika nchi yoyote na kiongozi wa nchi ndiye anayestahili kuwa na mamlaka ya aina hii. Sababu za dhana hii ni pamoja na: kuwasamehe wafungwa kwa sababu za kibinadamu (mfano umri wao, afya mbaya au vigezo vingine vinavyofaa); Kumsamehe mfungwa aliyetiwa hatiani kimakosa; na Kuimarisha mashirikiano na mahusiano na mataifa mengine kwa kumsamehe raia wa nchi nyingine ambaye amefungwa katika Magereza ya Tanzania.

Sababu ya kuanzishwa kwa Kamati ya Taifa ya Ushauri yenye wajibu wa kumshauri Rais kuhusu kutoa msamaha ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka uwepo utaratibu wa wazi wa kikatiba wa kutekeleza mamlaka hayo ya Rais ili kuondoa uwezekano wa matumizi yasiyo mazuri ya madaraka ya aina hii kwa kuwasamehe watu ambao jamii huona hawastahili kusamehewa.

**Ibara ya 87: Kinga ya Mashtaka Dhidi ya Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka kinga yenye ukomo ya mashtaka dhidi ya Rais (*restrictive immunity*) kwa kuzuwia mtu yeyote kumshtaki Rais wakati akiwa madarakani au akiwa amemaliza muda wake kwa makosa aliyotenda akiwa madarakani isipokuwa kama ameshtakiwa na ameondolewa madarakani na Bunge.

Hata hivyo Rais akifanya makosa ya jinai akiwa madarakani utaratibu wa kumuondoa madarakani kwa kushtakiwa na Bunge (*impeachment*) utatumika ili kumvua hadhi ya Urais na aweze kushtakiwa kwa makosa aliyotenda kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 88 ya Rasimu hii.

Aidha, Ibara inakataza kufungua shauri la madai dhidi ya Rais kwa jambo lolote alilotenda au alilokosa kulitenda kama raia, kabla au baada ya kushika madaraka mpaka apewe taarifa angalau siku 30 kabla ya kufunguliwa shauri kama hilo.

**b. Maudhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara ni kulinda hadhi na heshima ya Rais akiwa Mkuu wa Nchi kwa kuwa yeye ni taswira na alama ya umoja wa kitaifa. Vilevile kumuondolea Rais hofu katika kutekeleza majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sheria za kimataifa na sheria za nchi zinawapa viongozi wa nchi kinga dhidi ya kushtakiwa kama ilivyo kwa wana diplomasia.

Kwamantiki hiyo na pia kwa kuzingatia maoni ya wananchi ni muhimu kwa Rais akiwa Mkuu wa Nchi na Taswira ya Umoja wa Taifa abaki na kinga dhidi ya mashtaka akiwa madarakani na anapomaliza muda madaraka yake.

Sababu ya mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa baadhi ya watu kuitumia fursa hiyo vibaya na hivyo kumfanya Rais asijiamini na kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuimarisha utawala wa sheria na uwajibikaji kwa upande wa Mkuu wa Nchi na hivyo kumfanya Rais akiwa Kiongozi Mkuu kuwa mfano kwa wananchi wengine katika kufuata na kutii sheria.

**Ibara ya 88: Bunge Kumshtaki Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inalipa Bunge kwa nafasi yake ya kuwakilisha wananchi mamlaka ya kumshtaki na kumuondoa Rais madarakani kwa makosa mbalimbali yaliyotajwa katika Katiba. Makosa hayo ni pamoja na ukiukwaji mkubwa wa Katiba, makosa makubwa ya jinai, rushwa, uhaini na mwenendo unaodhalilisha nafasi ya Urais, kupuuza au kukataa kutekeleza amri ya mahakama au kufanya kitendo cha kukiuka kanuni za maadili au miiko ya uongozi.

Ibara pia inaweka masharti ya kumshtaki Rais ikiwa ni pamoja na kiwango cha chini cha kura za Wabunge cha kuanzisha mashtaka, kuundwa kwa tume ya kumchunguza na kiwango cha chini cha idadi ya Wabunge kuweza kupitisha hoja ya kumuondosha madarakani.

**b. Maudhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu utakaotumika kumuwajibisha Rais, kujenga tabia na utamaduni wa kutii Katiba na kulinda hadhi ya ofisi ya Rais na heshima ya nchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka utaratibu wa Bunge kumshtaki Rais ambao ni muhimu katika nchi ya kidemokrasia inayofuata utawala wa sheria kama Tanzania. Ni utaratibu unaomkumbusha kiongozi wa nchi kuwa anawajibika kufanya kazi yake ipasavyo, na kuheshimu Katiba na sheria za nchi. Aidha, ni utaratibu unaomkumbusha kiongozi wa nchi kuwa mwenendo wake binafsi unafaa kuwa wenye maadili mema. Rais anatakiwa kuwa ni mfano kwa wananchi wote (*role model*).

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imetoa mamlaka ya kumshtaki Rais kwa Bunge na siyo mhimili wa Mahakama ambao ndiyo wenye jukumu la kutoa haki, kutafsiri sheria na kuilinda Katiba ya nchi. Utaratibu huu umefuata mfumo wa Kiingereza na Kimarekani ambako mhimili wa Bunge ndiyo umepewa mamlaka ya kuwashtaki viongozi wa Serikali. Kihistoria, huko Uingereza Bunge lilihodhi madaraka hayo ili kuonyesha uwezo wake dhidi ya Serikali baada ya

kumshinda Mfalme. Lakini huko Marekani Bunge lilipewa mamlaka hayo kwa sababu tofauti.

Suala la kumuondoa Rais wa nchi ni nyeti kwa hivyo ni muhimu kuweka utaratibu madhubuti ili kuepuka uwezekano wa kuvuruga amani na utulivu wa nchi.

Mfano Katiba ya Marekani iliyotungwa mwaka 1787 na kuanza kutumika mwaka 1789 ililipa Bunge *(Congress)* mamlaka ya kumshtaki na kumuondoa madarakani Rais wa nchi hiyo.

Kuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kumuondoa Rais madarakani kutaepusha uwezekano wa kuvuruga amani na utulivu wa nchi.

**Ibara ya 89: Maslahi ya Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka chombo cha kikatiba kitakachopanga mshahara na maslahi mengine ya Rais, na inampa Rais uhakika wa mshahara na malipo mengine kutopunguzwa wakati akiwa madarakani.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupanga na kulinda maslahi ya Rais.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kikatiba mapato ya Rais ili kuziba mianya ya ubadhirifu, ufisadi na matumizi mabaya kwa ujumla. Vilevile ni kuimarisha dhana kuwa Rais ni mtumishi wa wananchi na kwa hivyo, kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, atatunzwa kwa kazi yake ya kutumikia umma.

Mapendekezo haya pia ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa chombo kitakachokuwa na jukumu la kupanga mishahara na maslahi ya Viongozi na Watumishi wa Umma ili kuweka uwiano wa malipo ya mishahara na maslahi mengine katika Utumishi wa Umma.

## (e) *Makamu wa Rais*

**Ibara ya 90: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara ya Rasimu ya katiba inaweka nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Msaidizi Mkuu wa Rais. Pia Ibara inaainisha majukumu ya kikatiba ya Makamu wa Rais kuwa ni kufanya kazi atakayoagizwa na Rais, kukaimu nafasi ya Rais kwa masharti yaliyotajwa kwenye Katiba na kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni na lengo ni kuainisha kikatiba kuwepo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Rais pamoja na majukumu ya Makamu wa Rais aliyopewa na Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mapendekezo haya ni kuendeleza masharti yaliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 kumtambua Makamu wa Rais kuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais Mtendaji. Aidha, kuwepo kwa nafasi ya Makamu wa Rais kutarahisisha utaratibu wa kukaimisha nafasi ya Rais pindi inapokuwa wazi.

Sababu nyingine ni kwamba Makamu wa Rais atahusika pia na uratibu wa Ushirikiano wa Nchi Washirika wa Muungano katika mambo yasiyo ya Muungano na uhusiano wa Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika. Kwa sababu hiyo, Makamu wa Rais ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Uratibu na Ushirikiano ambayo Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar pia ni wajumbe.

Aidha, inapendekezwa Tume ya Uratibu na Ushirikiano ipeleke taarifa zake Baraza la Ulinzi na Usalama ambalo Mwenyekiti wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar ni wajumbe.

**Ibara ya 91: Upatikanaji wa Makamu wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua utaratibu wa kumpata Makamu wa Rais kwa njia ya uchaguzi wa kidemokrasia akiwa Mgombea mwenza; na kuweka masharti kwamba iwapo mgombea Urais atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano basi Makamu wa Rais atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuainisha upatikanaji wa Makamu wa Rais kwa kupigiwa kura katika Uchaguzi Mkuu wa Rais kwa tiketi moja na Mgombea Urais.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuendelea kuwepo kwa nafasi ya Makamu wa Rais. Pia ni kuonesha kuwepo kwa sura mbili za Nchi Washirika katika uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano.

Pia Ibara hii inaondoa uwezekano wa upande mmoja wa Muungano kutoa nafasi zote mbili za Rais na Makamu wa Rais

**Ibara ya 92: Sifa za Makamu wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza kuwa mtu anayetaka kugombea nafasi ya Makamu wa Rais awe na sifa za kuwa mgombea Urais. Pia Ibara inaelekeza kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano anaweza kumchagua mtu ambaye ni Rais wa Nchi Mshirika kuwa Mgombea Mwenza wake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba sifa na vigezo vitakavyowezesha kumpata Makamu wa Rais. Pia ni kugawa nafasi za uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano kati ya Nchi Washirika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za kupendekeza sifa za Makamu wa Rais ziwe sawa na sifa za Rais ni kuwa yeye ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais, na ndiye atayekaimu au kushika nafasi ya Rais ikiwa Rais atafariki dunia au ataondolewa madarakani kwa mujibu wa mashrti ya Katiba.

**Ibara ya 93: Kiapo cha Makamu wa Rais**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kiapo cha Makamu wa Rais na kuainisha utaratibu wa kikatiba wa kuapishwa kwake. Aidha, Ibara pia inaelekeza kuwa Makamu wa Rais ataapishwa na Jaji Mkuu siku moja na Rais na kwamba hataapishwa kabla ya kupita siku thelathini kutoka siku matokeo yalipotangazwa na Tume au siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ibara hii inalenga kuweka utaratibu wa Makamu wa Rais kula kiapo cha kikatiba kabla ya kushika madaraka yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba uliopo kwa Makamu wa Rais kula kiapo cha utii na uaminifu kabla ya kushika madaraka.

Aidha, ni kuzingatia utaratibu wa kikatiba unaowataka Viongozi Wakuu kuapa kwa mujibu wa Katiba ili waweze kuwajibika na kutekeleza viapo vyao ikiwa ni pamoja na kulinda Muungano.

Uzoefu wa Katiba za nchi nyingine kama Kenya na Marekani ambazo Rais wake huapishwa baada ya kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu na huapishwa pamoja na Makamu wake.

**Ibara ya 94: Wakati wa Makamu wa Rais Kushika Madaraka**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kikatiba wa Makamu wa Rais kushika Madaraka siku moja na Rais. Aidha, Ibara inaweka masharti kuhusu Makamu wa Rais kuacha kushika nafasi hiyo kwa mujibu wa Katiba.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuonesha muda wa kuanza na ukomo wa Makamu wa Rais kushika madaraka kwa mujibu wa Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuendeleza utamaduni wa kuwepo kwa ukomo wa kushika madaraka kwa Viongozi Wakuu wa nchi kwa kutambua kuwa uongozi ni dhamana na siyo haki.

**Ibara ya 95: Bunge Kumshtaki Makamu wa Rais.**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inalipa Bunge mamlaka ya kumshtaki na kumuondoa madarakani Makamu wa Rais kwa utaratibu ambao pia unatumika kumshtaki na kumuondoa madarakani Rais. Tofauti ni kuwa utaratibu wa kumshtaki Makamu wa Rais unaanzishwa na Rais badala ya Wabunge kwa kuwasilisha hati kwa Spika kama inavyoelekeza Ibara ya 88 ya Rasimu ya Katiba.

Ibara hii pia inamuondolea sifa Makamu wa Rais aliyeondolewa madarakani kwa utaratibu huu, kuwa Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kumuwajibisha Makamu wa Rais, kujenga tabia na utamaduni wa kutii Katiba, kulinda hadhi ya ofisi ya Makamu wa Rais na heshima ya nchi.

Lengo pia ni Kulipa Bunge mamlaka, ambacho ni chombo kinachowakilisha wananchi, kuchukua hatua kwa mujibu wa Katiba kumshtaki na kumuondoa madarakani Makamu wa Rais inapothibitika ametenda makosa yaliyoainishwa kwenye Rasimu ya Katiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa Bunge kumshtaki Makamu wa Rais kwa mujibu wa Katiba, ambalo ni suala muhimu katika nchi ya kidemokrasia inayofuata utawala wa sheria.

**Ibara ya 96: Upatikanaji wa Makamu wa Rais Wakati Nafasi Hiyo Inapokuwa Wazi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza utaratibu wa kujaza nafasi ya Makamu wa Rais inapotokea kuwa wazi kutokana na sababu zilizoainishwa kwenye Ibara za 94 na 95 za Rasimu ya Katiba. Aidha, ibara hii pia inampa wajibu Rais kumteua Makamu wa Rais mwingine ndani ya siku 14.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa namna ya kujaza nafasi ya Makamu wa Rais itakapotokea kuwa wazi kabla ya kufika muda wake wa kuondoka madarakani kwa mujibu wa Katiba.

Vile vile ni kulipa Bunge mamlaka ya kumthibitisha Makamu wa Rais, kwa niaba ya wananchi na kumpa kikatiba Makamu wa Rais uhalali wa kisiasa.

## c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kumpata Makamu wa Rais bila ya kusubiri uchaguzi mkuu na kuwezesha majukumu yake kuendelea kutekelezwa na hivyo kuzuia ombwe katika uongozi wa juu.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuendeleza maudhui mazuri ya ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## SEHEMU YA PILI

## BARAZA LA MAWAZIRI LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

### *(a) Baraza la Mawaziri*

### Ibara ya 97: Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano, muundo wake, majukumu na taratibu za uendeshaji wa vikao vyake. Vikao vya Baraza la Mawaziri vitaongozwa na Rais na vitahudhuriwa pia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Aidha, Ibara hii inatambua Baraza la Mawaziri kuwa ndicho chombo kikuu cha kumshauri Rais katika utekelezaji wa madaraka yake na shughuli za serikali. Ibara pia inazuia Bunge au Mahakama kuchunguza ushauri unaotolewa na Baraza la Mawaziri kwa Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha Baraza la Mawaziri na kutambua jukumu lake la msingi la kumshauri kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Pia, ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa Baraza la Mawaziri kufanya kazi yake ya ushauri kwa Rais bila ya hofu wala woga.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuanzisha chombo hiki na kutambua umuhimu wake katika kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977. Sababu nyingine ni kujenga mazingira ya chombo hicho kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa na mihimili mingine ya dola.

### Ibara ya 98: Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya katiba ni inaainisha utaratibu wa uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri na idadi yao. Aidha, inaweka masharti ya uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri ambayo ni pamoja na uteuzi huo kuzingatia uwakilishi wa Nchi Washirika na kuthibitishwa na Bunge. Ibara pia inatamka kuwa idadi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri haitazidi 15.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni pamoja na kuweka ukomo wa idadi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia ni kulipa Bunge mamlaka ya kuwasaili na kuwathibitisha Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa niaba ya wananchi ili

kujenga uadilifu na kuthibitisha uweledi wa wateuliwa ili kukuza uwajibikaji katika uongozi wa taifa.

**c. Sababu za mapendekezo**

Kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka Katiba itamke ukomo wa idadi ya Mawaziri ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Hii pia ni kutekeleza maoni ya wananchi waliotaka madaraka ya Rais ya uteuzi yasimamiwe kwa kulipa Bunge mamlaka ya kuwathibitisha.

Aidha, kutokana na Mambo ya Muungano kupungua hadi kufikia saba na kupunguza ukubwa wa Serikali ya Shirikisho, Rasimu inapendekeza kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wasizidi kumi na tano.

**Ibara ya 99: Waziri Mwandamizi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha nafasi ya Waziri Mwandamizi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano atakayeteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge, sifa za mtu kuwa Waziri Mwandamizi na muda wake wa kushika madaraka.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka nafasi ya Kikatiba ya Waziri Mwandamizi katika utendaji wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa na majukumu yaliyoainishwa katika Ibara ya 100 Rasimu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kwa kuzingatia ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ibara ya 100: Kazi na Mamlaka ya Waziri Mwandamizi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa Waziri Mwandamizi madaraka ya udhibiti na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali za siku hadi siku. Ibara pia intamka kuwa katika utekelezaji wa shughuli zake Waziri Mwandamizi atawajibika kwa Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka Waziri Mwandamizi atakayemsaidia Rais kusimamia Wizara na Mawaziri katika utendaji wao wa shughuli za kila siku za Serikali. Pia lengo la Ibara hii ni kumpa uwezo wa kikatiba Waziri Mwandamizi kukaimu nafasi ya Rais ikiwa Rais na Makamu wa Rais hawapo nchini.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kusimamia na kutekeleza majukumu ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanatekelezwa na yanasimamiwa na Waziri Mkuu. Rasimu ya Katiba inapendekeza kuondoa nafasi ya Waziri Mkuu ambaye kiuhalisia

alikuwa anasimamia mambo yasiyo ya Muungano ya Tanganyika kwasababu majukumu hayo sasa yatakuwa chini ya mamlaka ya Serikali ya Tanganyika.

**Ibara ya 101: Sifa za Mawaziri na Naibu Mawaziri**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua sifa za mtu kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na vigezo vya Kikatiba vinavyomuondolea mtu sifa za kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri. Sifa hizo ni pamoja na kuwa raia wa kuzaliwa na mwenye shahada ya chuo cha elimu ya juu, mwenye weledi na uzoefu. Ibara hii pia inawaondolea sifa Wabunge, wawakilishi wa aina zote au mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa ubadhirifu kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuleta ufanisi wa Serikali kwa kutaja sifa na vigezo mahsusi kwa mtu kuweza kuwa Waziri au Naibu Waziri.

Aidha, Ibara hii inalenga kuweka mfumo wa kikatiba wa kutenganisha madaraka ya mihimili ya dola (*separation of powers*), kupunguza misuguano kati ya Bunge na Mawaziri, na kuondoa uwezekano wa kuwepo mgongano wa kimasilahi unaotokana na majukumu ya Uwaziri na Ubunge au kazi nyingine.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Mfumo unaopendekezwa katika Rasimu hii kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wasitokane na Wabunge na wala wasihudhurie vikao vya Bunge isipokuwa kama watahitajika kutoa ufafanuzi kwenye vikao vya Kamati za Bunge au kwa Bunge zima kuhusu suala lolote lililopo katika madaraka yao ya utendaji ni kuzingatia maoni ya Wananchi waliotaka kutenganishwa kwa utendaji kazi wa Mihimili ya Bunge na Serikali ili kuongeza uwajibikaji wa Bunge katika kuisimamia Serikali. Aidha, mapendekezo haya yataondoa manung'uniko ya wananchi kwamba majimbo yanayoongozwa na Wabunge ambao ni Mawaziri au Naibu Mawaziri yanapendelewa katika huduma za maendeleo.

Sababu ya kupendekeza kuwa uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri, uthibitishwe na Bunge pia ni kuzingatia maoni wananchi walio wengi walisema kuwa Bunge ndicho chombo chenye ridhaa ya wananchi wote, na hivyo kiwe na uhalali wa kudhibiti madaraka ya Rais katika uteuzi huo. Muhimu zaidi matarajio ni kuwa utaratibu huu utaongeza uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

**Ibara ya 102: Kiapo, Muda na Masharti ya Kazi ya Waziri na Naibu Mawaziri**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kiapo, masharti ya kazi na muda wa kushika madaraka ya Waziri au Naibu Waziri. Ibara hii pia inaelekeza kuwa Waziri au Naibu Waziri ataapa kiapo cha uaminifu mbele ya Rais. Aidha, Ibara inatamka kuwa Waziri au Naibu Waziri atawajibika binafsi au kwa pamoja kwa Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya kushika madaraka ya Waziri au Naibu Waziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Vile vile ni kuweka msingi wa uwajibikaji wa Waziri au Naibu Waziri, binafsi au kwa pamoja kwa Rais.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuwepo kwa masharti ya Kikatiba ya kiapo na ya kazi ya Waziri au Naibu Waziri ili kujenga imani kwa wananchi kuwa watatekeleza majukumu yao kwa uaminifu na uadilifu.

Aidha, ni kuzingatia utaratibu unaopendekezwa wa Rais Mtendaji ambapo Mawaziri na Naibu Mawaziri watawajibika, binafsi au kwa pamoja kwa Mkuu wa Serikali aliyewateua. Utaratibu huu unaongeza nidhamu, ufanisi wa utendaji na uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

**Ibara ya 103: Utekelezaji wa Shughuli za Serikali Bungeni**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba kuhusu utaratibu wa Serikali kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zake Bungeni kwa kuainisha namna ambavyo Mawaziri watashiriki katika vikao vya Bunge wakiwa si sehemu ya Bunge. Vile vile, Ibara inampa Waziri fursa ya kuhudhuria vikao vya Kamati za Bunge kila anapohitajika na kutoa maelezo na ufafanuzi wa suala lolote la utendaji. Aidha, Ibara inabainisha kuwa uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali utakua chini ya mamlaka ya Rais akiwa Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kubainisha kikatiba mgawanyo wa madaraka baina ya Mhimili wa Bunge na Mhimili wa Utendaji ambao ni Serikali.

Aidha, lengo jingine ni kuweka utaratibu wa Mawaziri kuhudhuria vikao vya Kamati za Bunge kwa kualikwa.

Pia, ni kuweka msingi wa kuipa Serikali uwezo wa kufanya maamuzi juu ya masuala ya kisera kwa ujumla.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuweka utaratibu wa kuwawezesha Mawaziri ambao si Wabunge kuhudhuria vikao vya Bunge.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kutenganisha mamlaka ya Serikali na Bunge kwa kuweka wazi mipaka ya kiutawala ili kuondoa muingiliano wa majukumu ya mihimili ya dola katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

### *(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**Ibara ya 104: Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kuainisha upatikanaji wake, sifa, majukumu na ukomo wa kushika nafasi hiyo.
Aidha, Ibara inabainisha kuwa Mwanasheria Mkuu ndiye Mshauri Mkuu kuhusu mambo yote ya kisheria kwa Serikali. Mwanasheria Mkuu atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya kisheria ya Serikali, pia kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utaratibu wa uteuzi wake na ukomo wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Katiba wa kuanzisha na kuainisha nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Majukumu yake.

Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali athibitishwe na Bunge kabla ya kuapishwa na Rais.

Vile vile Mwanasheria Mkuu wa Serikali aendelee kushika madaraka hadi Rais atakapomteua Mwanasheria Mkuu mwingine ili nafasi hiyo isiwe wazi. Katiba ya mwaka 1977 iliweka masharti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukoma mara tu baada ya matokeo ya Urais kutangazwa.

### (c ) *Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu*

**Ibara ya 105: Katibu Mkuu Kiongozi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi na kuainisha upatikanaji wake, sifa zake na majukumu yake.
Ibara pia inatamka kuwa Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Katibu wa Baraza la Mawaziri, Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu, Katibu wa Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na Mkuu wa Utumishi wa Umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kumtambua kikatiba Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Mkuu wa Utumishi wa Umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Lengo jingine ni kumpa Katibu Mkuu Kiongozi mamlaka ya kikatiba ya kutoa maelekezo kuhusiana na masuala ya utumishi wa umma.

Aidha, kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Katibu Mkuu Kiongozi na utaratibu wa uteuzi wake kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi wa umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Wadhifa wa Katibu Mkuu Kiongozi ni nafasi muhimu sana katika utendaji wa Serikali, hivyo ni vyema majukumu yake yakaainishwa katika Katiba.

Katika utaratibu wa mgawanyo wa madaraka, Utumishi wa Umma ni chombo muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Katibu Mkuu Kiongozi kwa nafasi yake ya Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma ni kiungo muhimu kati ya Baraza la Mawaziri na Watumishi wa Umma na hivyo ni vyema akawepo kikatiba.

**Ibara ya 106: Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu**

**b. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua kikatiba nafasi ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na kueleza kuwa kila Katibu Mkuu atakuwa ndiye Kiongozi na mtendaji Mkuu wa Wizara. Aidha, Ibara hii inaainisha upatikanaji wa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, sifa zao na majukumu yao.

Ibara pia inaelekeza kuwa Makatibu Wakuu au Naibu Makatibu Wakuu watateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma.

**a. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, na utaratibu wa uteuzi wao. Aidha, lengo jingine ni kuwapa hadhi ya kikatiba viongozi na watendaji wakuu wa Wizara na kuhakikisha kuwa nafasi hizi zinajazwa na watu wenye uweledi na uzoefu katika Utumishi wa Umma na ambao ni waadilifu.

**b. Sababu za Mapendekezo**

Kutambua umuhimu wa Makatibu Wakuu ambao ndiyo Watendaji Wakuu wa Serikali na kuhakikisha kuwa wanapatikana kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Katika mfumo wa Serikali ya Kidemokrasia inayoheshimu utawala wa sheria, katika nchi yenye mfumo wa siasa za vyama vingi ni vyema Katiba ikalinda nafasi ya Katibu Mkuu.

**(d*) Utekelezaji wa Shughuli za Baraza la Mawaziri***

**Ibara ya 107: Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na kuainisha wajibu na majukumu ya Kamati hiyo. Kamati hiyo, itakuwa na majukumu ya kulishauri Baraza la Mawaziri juu ya masuala mbalimbali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuweka kikatiba chombo cha ushauri cha Baraza la Mawaziri, na kutambua umuhimu wa kulinda kikatiba nafasi ya washauri wakuu wa Serikali. Aidha, lengo jingine ni kuweka msingi wa ushauri wao kuzingatiwa na kuheshimiwa na Viongozi wa kisiasa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ni vyema vyombo vyote vya utekelezaji wa majukumu ya nchi vikabainishwa kwenye Katiba ya nchi. Katika mfumo wa nchi unaozingatia utawala bora na wa sheria wenye lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa Serikali ni muhimu kuwa na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*Inter-Ministerial Technical Committee*). Utaratibu huu unaimarisha uelewa wa pamoja katika mwelekeo wa maamuzi ya Serikali .

**Ibara ya 108: Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua kuwepo kikatiba kwa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambayo wajibu na majukumu yake makuu ni kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kutambua kikatiba Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kuwa ndio chombo cha ushauri na uratibu cha Baraza la Mawaziri katika utekekezaji wa majukumu ya Serikali.

Lengo jingine ni kuhakikisha ulingano, mwendelezo na weledi katika maamuzi ya Baraza la Mawaziri na Serikali; na kuweka Kundi la Wataalam Waliobobea katika nyanja zao (*Think Tank*) la Serikali inayofanya utafiti na kutoa ushauri kwa Baraza la Mawaziri na Serikali.

Kuimarisha uratibu wa ushauri wa kitaalam Serikalini.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ni chombo muhimu sana katika usimamizi wa shughuli za Serikali. Katika nchi nyingine za Afrika na hasa zile zilizotawaliwa na Wafaransa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ni chombo muhimu cha kikatiba na kinaongozwa na mtu mwenye hadhi ya Waziri wa Nchi. Chombo hiki ndicho "Think Tank" ya Baraza la Mawaziri na pia, kinachoratibu ushauri wa masuala yote ya Serikali kwa kushirikisha Wizara zote Serikalini. Hivyo, sababu ya mapendekezo haya ni kuanzisha kikatiba kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu chombo hiki muhimu cha kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu

## SURA YA NANE

## UHUSIANO NA URATIBU WA SERIKALI

### Ibara ya 109: Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, kwa mara ya kwanza katika historia ya Jamhuri ya Muungano, inaanzisha chombo cha kikatiba cha uhusiano na uratibu wa Serikali.

Chombo hiki ambacho kitaitwa "Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali" kitakuwa na wajumbe ambao ni; Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakua ni Mwenyekiti; Rais wa Tanganyika; Rais wa Zanzibar; Mawaziri Wakaazi; na Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Nje wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Tume hii ni kiungo muhimu kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuanzisha kikatiba chombo kitakachosimamia uhusiano na uratibu baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; na baina ya Serikali za Nchi Washirika juu ya mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Kuweka utaratibu wa mawasiliano na mashauriano endelevu kati ya Serikali hizo tatu utakaotoa mwelekeo wa kuimarisha na kudumisha Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu wa kikatiba utakaowezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kukutana kwa lengo la kujadiliana na kushauriana katika mambo ya msingi ya maendeleo ya wananchi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, utaratibu huu utasaidia sana kuweka mahusiano mema na kuoanisha sera zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kuwepo kwa Muungano wa zaidi ya Serikali moja katika Jamhuri ya Muungano kunahitaji mfumo madhubuti wa uratibu wa uhusiano na ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za nchi Washirika na baina ya Serikali za nchi washirika zenyewe kwa zenyewe kwa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Moja ya udhaifu wa utaratibu unaotumika sasa ni kukosekana kwa nguvu ya kikatiba ya uratibu wa masuala ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni ya kiutawala na ya hiyari.

Uzoefu wa nchi nyingine zenye mfumo wa Muungano au shirikisho na hata zile zenye Serikali za majimbo zina Tume za aina hii zinazoitwa kwa majina mbalimbali. Nchi nyingi zenye Tume hizi zinaitwa *Inter-Governmental Relations Commission*. Nchi zenye tume hizi katika Katiba zao ni pamoja na India, Canada, Nigeria, Afrika ya Kusini na Kenya.

## Ibara ya 110: Malengo ya Tume

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba yanayoainisha malengo ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali. Malengo hayo ni; kuweka utaratibu bora na endelevu wa kushauriana na kushirikiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; kukuza na kuwezesha uratibu na ushirikiano miongoni mwa Nchi Washirika kuhusu mambo yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuwezesha kufanana kwa kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wote; kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kujadili utekelezaji wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa manufaa na ustawi wa wananchi wote; na kuweka mazingira mazuri ya utatuzi wa migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Nchi Washirika zenyewe.

### b. Madhumuni na Lengo

Kuimarisha kikatiba uratibu, uhusiano na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Nchi Washirika zenyewe kuhusu mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Kujenga utamaduni wa kikatiba wa kutatua migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Nchi Washirika kwa njia ya majadiliano, mashauriano na maridhiano.

### c. Sababu za Mapendekezo

Kuweka utaratibu wa kikatiba utakaoweka mazingira mazuri ya kushauriana na kushirikiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na baina ya Nchi Washirika. Pia kuwezesha uratibu wa ushirikiano miongoni mwa nchi washirika katika mambo yasiyo ya muungano ili kuweka kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wao katika sura inayofanana.

Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali pia itasaidia kuibua na kuyasimamia, kwa manufaa ya nchi, masuala mbalimbali ya Muungano na yasiyo ya Muungano yenye maslahi kwa Taifa kwa lengo la kuleta ustawi wa Taifa na jamii nzima ya Tanzania.

## Ibara ya 111: Majukumu ya Tume

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali katika kuwezesha kutekeleza sera, sheria, mipango na mikakati baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Serikali za Nchi Washirika. Majukumu hayo ya Tume ni pamoja na kushauriana baina ya Serikali ya Muungano na taasisi za kimataifa kwa niaba ya Nchi Washirika. Aidha, Tume itahusika pia, na usuluhishi na utatuzi wa migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na pia baina ya Serikali za Nchi Washirika katika mambo yasiyo ya Muungano. Ibara pia inalipa Bunge mamlaka ya kutunga

Sheria kwa ajili ya kusimamaia uhusiano na uratibu baina ya Serikali za Nchi Washirika na kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika; na kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa Katiba.

Aidha, Ibara inaelekeza kuwa ni pale tu ambapo usuluhishi wa mgogoro umeshindikana ndipo Tume inaweza kulipeleka suala hilo katika Mahakama ya Juu na uamuzi wa Mahakama hiyo utakuwa wa mwisho.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya ibara hii ni kuainisha kikatiba majukumu ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali ili kuipa nguvu kiutekelezaji. Kuimarisha Muungano kwa kuhakikisha kuna uwiano wa sera na sheria za Nchi Washirika katika mambo yasiyo ya Muungano.

Madhumuni mengine ni kuwa na chombo cha kikatiba cha awali kwa ajili ya kuzuia, na inapotokea, kusuluhisha migogoro miongoni mwa Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kabla ya migogoro hiyo kufikishwa kwenye Mahakama ya Juu kwa uamuzi wa mwisho.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kwamba kuna uwiano wa sera na sheria kwa Nchi Washirka katika mambo yasiyo ya muungano, pia kuweka utaratibu wa kusimamia na kukuza masuala yenye maslahi kwa Taifa, na kuweka utaratibu wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Serikali za Nchi Washirika.

Aidha, kuwepo kwa zaidi ya Serikali moja ndani ya Jamhuri moja kunaweza kusababisha tofauti za kisera kwenye masuala ya msingi kama vile elimu, afya n.k baina ya Serikali za Nchi Washirika, hivyo ni muhimu kuwa na chombo maalum kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha kwamba, kunakuwa na ufanani (*harmonisation*) na ulinganifu (*approximation*) wa sera na sheria baina ya Serikali hizo katika mambo yasiyo ya Muungano.

**Ibara ya 112: Sekretarieti ya Tume**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaunda Sekretarieti ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali ambayo itaongozwa na Katibu na Naibu Katibu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuanzisha kikatiba chombo cha kitaalam na kiutendaji cha Tume kitakachokuwa na wataalam wa fani mbalimbali watakaotoa ushauri wa kitaalam juu ya ulinganifu wa sera na sheria, na pia juu ya uhusiano wa kimataifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuwa na chombo cha kutoa ushauri kwa Tume, kurahisisha na kusimamia utekelezaji wa majukumu na shughuli za kila siku za Tume.

Uzoefu wa nchi nyingine kama vile Afrika ya Kusini, India, Kenya na Nigeria Sekretareti kama hizi zina idara za kisekta zenye kongane (*Clusters*) na Kamati za Ufundi (*Technical Committees*) ili kuimarisha usimamizi, uratibu na utendaji wa Tume na Serikali tatu katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo itafaa Sekretarieti inayopendekezwa kuwa na muundo kama huo.

## SURA YA TISA

## BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

## SEHEMU YA KWANZA

## KUUNDWA NA MADARAKA YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

### Ibara ya 113: Kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Bunge la Jamhuri ya Muungano na kutaja aina na idadi ya Wabunge, majimbo ya uchaguzi na utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge. Ibara pia inaelekeza kuwepo kwa majimbo sabini ya uchaguzi ambapo kila jimbo litakuwa na Wabunge wawili mmoja mwanamke na mmoja mwanamme watakaopigiwa kura na wananchi, na wabunge watano watakaoteuliwa na Rais kwa kuzingatia uwakilishi wa Nchi Washirika na jinsi kuwakilisha Watu Wenye Ulemavu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka mamlaka ya nchi itakayohusika na kutunga sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweka aina na utaratibu wa upatikanaji wa wawakilishi wa wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuanzisha chombo cha uwakilishi wa wananchi ambacho ni Bunge la Jamhuri ya Muungano litakalotunga sheria, kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuwajibika kwa wananchi. Aidha, pamoja na sababu hiyo, ni kuweka utaratibu wa kuwapata Wabunge wa kuchaguliwa na Wabunge wa kuteuliwa na Rais kuwakilisha Watu Wenye Ulemavu.

Sababu nyingine ya mapendekezo ni kuweka usawa wa kijinsi katika uwakilishi Bungeni, kuzingatia Mikataba ya kikanda na kimataifa na kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa Bunge dogo ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa shughuli za Bunge.

### Ibara ya 114: Muda wa Bunge

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha maisha ya kila Bunge kuwa ni muda wa miaka mitano ikiwa na maana ya muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge Jipya litaitishwa. Aidha, Ibara hii inaainisha hatma ya Bunge ili kuwezesha uchaguzi mwingine kufanyika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka muda maalum wa kipindi cha Bunge ambao ni miaka mitano na kujenga utamaduni wa Bunge kutimiza malengo na majukumu yake katika muda uliopangwa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka ukomo wa Wabunge ili kuwezesha uchaguzi mwingine kufanyika kila baada ya miaka mitano.

Kutoa nafasi kwa wananchi wengine kushika madaraka ili kuleta mawazo mapya ya kifikra na kimaendeleo katika nchi.

**Ibara ya 115: Madaraka ya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaainisha Bunge kuwa ndiyo chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano chenye madaraka, kwa niaba ya wananchi, ya kusimamia Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote.

Madaraka haya ni pamoja na kutunga sheria, kuishauri Serikali, kuhoji Mawaziri, kujadili na kuidhinisha bajeti na mipango ya Serikali, kujadili na kuridhia mikataba ya kimataifa na ile inayohusisha rasilimali zinazosimamiwa na Serikali.

Kusimamia Serikali kwa kuangalia mwenendo wa utendaji wa Rais, Makamu wa Rais, Mawaziri na Watendaji Wakuu katika Utumishi wa Umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha majukumu ya Bunge kuwa ni chombo chenye madaraka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali, kutunga sheria na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya mambo yote yenye maslahi kwa Taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua Bunge kuwa ni chombo kinachowakilisha wananchi katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na maslahi ya wananchi na Taifa.

Sababu nyingine ni kuendeleza mfumo unaotumika katika nchi za kidemokrasia duniani ambapo kunakuwa na chombo cha aina hii ambacho kazi yake kubwa ni kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi na kuimarisha msingi wa mgawanyo wa madaraka baina ya Bunge, Mahakama na Serikali.

**Ibara ya 116: Mipaka ya Bunge Katika Kutumia Madaraka Yake**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha wajibu wa Bunge kuwa ni kusimamia, kuishauri na kuiwajibisha Serikali bila ya kuingilia shughuli za kiutendaji ambazo kidesturi ni shughuli za Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha masharti juu ya mipaka ya Bunge katika kuiwajibisha Serikali na kubainisha umuhimu wa mipaka ya mamlaka kati ya Mihimili Mikuu ya Dola.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuepusha muingiliano wa majukumu baina ya Bunge na mihimili mingine hasa wa utendaji na kuimarisha misingi ya udhibiti na urari wa madaraka (*Checks and balance*).

**Ibara ya 117: Madaraka ya Bunge Kutunga Sheria**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa madaraka kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutunga sheria zote za Jamhuri kuhusiana na Mambo ya Muungano. Pia Ibara inaainisha kuwa madaraka ya kutunga sheria katika Tanganyika kwa mambo yote yasiyo ya Muungano yatakuwa chini ya Bunge la Tanganyika na madaraka ya kutunga sheria katika Zanzibar kwa mambo yote yasiyo ya Muungano yatakuwa chini ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuainisha kikatiba kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano ndicho chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano. Kuainisha kikatiba kuwa madaraka ya kutunga sheria ya Nchi Washirika kwa mambo yasiyo ya Muungano yamepewa Bunge la Tanganyika na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Ibara hii pia inalenga kubatilisha sheria yoyote itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, Bunge la Tanganyika na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kinyume na masharti ya Katiba hii.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kutofautisha majukumu ya kutunga sheria baina ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na baina ya vyombo vya kutunga sheria vya Nchi Washirika. Pamoja na majukumu hayo, Ibara inaweka mipaka ya kila mamlaka katika kutunga sheria. Mipaka hiyo inalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano litatunga sheria katika Mambo ya Muungano tu na vyombo vya kutunga sheria vya nchi Washirika vitatunga Sheria katika mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu maeneo yao.

**Ibara ya 118: Utaratibu wa Kubadilisha Katiba**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha masharti yatakayoliwezesha Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba na kuelekeza kuwa Muswada wowote wa sheria ya kubadili Katiba ni lazima uungwe mkono na kura za Wabunge zisizopungua theluthi mbili za Wabunge kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa jinsi ya kufanya mapitio ya Katiba pindi itakapolazimu kurekebishwa na kuzuia marekebisho ya Katiba ya mara kwa mara.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kufanya marekebisho ya Katiba yaridhiwe na pande zote mbili za Muungano ili kuimarisha hadhi sawa za Nchi Washirika. Sababu nyingine ni kulipa mamlaka Bunge kufanya mabadiliko ya masharti ya Katiba hii pale itakapoonekana inafaa.

**Ibara ya 119: Utaratibu wa Kubadilisha Masharti Mahsusi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaweka masharti mahsusi ya kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika maeneo ya msingi ambayo ni masharti yaliyomo katika Sura ya Kwanza, Sura ya Pili na Sura ya Nne; masharti ya Ibara ya 60; masharti ya Ibara ya 79; kuongeza au kupunguza jambo lolote la Muungano; uwepo wa Jamhuri ya Muungano; na masharti ya Ibara hii.

Ibara pia inaelekeza kuwa mabadiliko yoyote kuhusu vipengele hivi itabidi yaungwe mkono kwa theluthi mbili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano kutoka kila upande wa Jamhuri kwa kura ya maoni itakayoendeshwa na kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuliwekea Bunge mipaka katika kufanya mabadiliko ya masharti mahsusi ya Katiba. Aidha, kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano na kwamba maeneo ya msingi ya masharti ya Katiba yanabadilishwa kwa ridhaa ya wananchi wenyewe.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwapa nafasi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki moja kwa moja katika kufanya maamuzi kuhusu maeneo muhimu ya Katiba kwa maslahi ya Taifa lao.

**Ibara ya 120: Utaratibu wa Kutunga Sheria**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii inaweka utaratibu kwa Bunge kutumia madaraka yake ya kutunga Sheria kwa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ambao utawekwa saini na Rais. Muswada unaweza kuandikwa na Serikali, Kamati ya Bunge au kikundi cha Wabunge.

Ibara pia inaitaka Serikali kuwashirikisha wananchi kwa ajili ya kupata maoni yao juu ya Muswada husika. Muswada utapitishwa kwa kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili kutoka kila upande wa Muungano. Pia, Bunge litatunga Kanuni za Kudumu za kusimamia utaratibu huu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara ni kuainisha utaratibu utakaotumiwa na Bunge la Muungano katika kutekeleza wajibu wake wa kutunga sheria na Kanuni za Kudumu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo hayo ni kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Bunge na kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa wananchi katika utungaji wa sheria. Kutoa nafasi sawa kwa Wabunge wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika kutunga Sheria na Kanuni. Aidha, ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu mmoja unaofuatwa katika kutunga sheria.

**Ibara ya 121: Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo ya Fedha**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha masharti maalum kuhusu utaratibu na mipaka ya kuzingatiwa na Bunge katika kutunga sheria juu ya mambo ya fedha.

Aidha, Ibara inaainisha mambo ambayo Bunge haliwezi kuyashughulikia isipokuwa kama Rais amependekeza kufanya hivyo na kwamba pendekezo hilo la Rais liwe limewasilishwa Bungeni na Waziri.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka mipaka ya kikatiba kuhusu utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha. Mambo hayo ni pamoja na miswada ya Sheria kuhusu kodi, malipo au matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina au mfuko mwingine wowote wa Serikali na kusamehe au kufuta deni lolote la Serikali.

Lengo jingine ni kuweka mipaka kati ya madaraka ya Serikali na ya Bunge kuhusu masuala ya fedha.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ni kuondoa muingiliano wa madaraka kati ya Serikali na Bunge katika kutekeleza majukumu yao kuhusu masuala ya fedha.

**Ibara ya 122: Madaraka ya Mkuu wa Nchi Kuhusu Muswada wa Sheria**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara ya hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu madaraka ya Mkuu wa Nchi katika kuthibitisha Miswada ya Sheria inayopitishwa na Bunge. Rais atatakiwa kusaini Muswada ndani ya siku zisizozidi 30 tangu muswada uwasilishwe kwake. Rais ana mamlaka ya kukubali au kukataa kusaini Muswada huo na iwapo atakataa Muswada utarudishwa Bungeni kwa majadiliano na kurudishwa tena kwa Rais. Iwapo Rais atakataa tena kusaini Muswada huo basi itahesabika kuwa umepitishwa kuwa Sheria.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua nafasi ya Rais akiwa Mkuu wa Nchi katika utaratibu wa kuidhinisha Miswada ya Bunge kuwa Sheria. Sababu nyingine ni kuweka

udhibiti kwa Bunge katika jukumu lake la kutunga sheria kwa kuhakikisha maslahi ya taifa na maslahi ya wananchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Chini ya mapendekezo ya Rasimu hii, Rais si sehemu ya Bunge, hata hivyo ni muhimu kwake kuidhinisha Miswada ya Serikali kama ilivyo katika nchi nyingine zenye utaratibu huu kwa mfano Marekani na Kenya. Sababu nyingine ni kujenga uhusiano bora na mzuri kati ya Bunge na Serikali na kuepuka uwezekano wa kukwamishana katika utekelezaji wa shughuli zao na kuepuka kuvunja Bunge kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ibara ya 123: Kupitishwa kwa Hoja za Serikali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya utaratibu wa kupitishwa kwa Hoja za Serikali ndani ya Bunge kuhusu bajeti. Bunge limepewa madaraka ya kupitisha Hoja ya Serikali kuhusu bajeti pamoja na mapendekezo ya kurekebisha upungufu utakaobainika baada ya Serikali kufanya marekebisho na kurejesha hoja Bungeni. Endapo Bunge litakataa kwa mara ya pili hoja kuhusu bajeti, basi bajeti ya Serikali itahesabika kuwa imepitishwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuhakikisha kuwa bajeti ya serikali inapitishwa kwa kuzingatia mapendekezo ya Bunge. Lengo jingine ni kuepuka Bunge kukwamisha shughuli za utendaji za nchi na Serikali bila sababu za msingi lakini wakati huo huo kuzuia serikali kuliburuza Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba Serikali ndio yenye jukumu la kukusanya kodi kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kwa ajili ya maendeleo ya Serikali. Sababu nyingine ni kwamba Bunge ndio chombo cha wananchi chenye mamlaka ya kuweka viwango na utozaji wa kodi kutokana na mapendekezo ya Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## WABUNGE

### *(a) Uchaguzi wa Wabunge*

**Ibara ya 124: Uchaguzi wa Wabunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba juu ya uchaguzi wa Wabunge kuwa kila baada ya miaka 5 ukisimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Aidha, Ibara inaelekeza usiwepo uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi ya Mbunge wa Jimbo kwa nafasi itakayoachwa wazi na Mbunge wa Chama cha Siasa na badala yake Tume Huru ya Uchaguzi itajaza nafasi hiyo kwa kuzingatia orodha ya majina iliyowasilishwa awali na chama husika na kwa kushirikiana na chama hicho. Ibara pia inaweka utaratibu wa kufanya uchaguzi mdogo endapo kiti cha Mbunge aliyetokana na Mgombea Huru kitakuwa wazi kwa sababu yoyote.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya kuwa na uchaguzi wa mara kwa mara katika vipindi maalum. Lengo jingine ni kuwapa wananchi mamlaka ya kutoa ridhaa kwa wawakilishi wao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Bunge ndicho chombo cha uwakilishi cha wananchi chenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, ni vyema wabunge wakawa wanathibitishwa kila baada ya kipindi maalum ili waendelee kuwa na ridhaa ya wananchi.

Aidha, sababu nyingine ya mapendekezo ya Ibara hii ni kuepusha gharama za chaguzi ndogo katika mfumo wa uchaguzi nchini.

**Ibara ya 125: Sifa za Kuchaguliwa Kuwa Mbunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge pamoja na kuainisha watu ambao kwa nyadhifa zao hawataweza kuchaguliwa kuwa Wabunge. Watu hao ni pamoja na Rais na Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar na Makamu wao, Spika na Naibu Spika, Waziri na Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na wengine kama itakavyoainishwa kwenye sheria.

Ibara inapendekeza pia kuwepo kwa Mgombea Huru katika nafasi ya Ubunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya sifa za mtu kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge. Vilevile kutambua kikatiba haki ya msingi ya uraia ya kupiga kura na kupigiwa kura bila kuhitaji kuwa mwanachama wa chama cha siasa. Pia kuhakikisha

mgombea atamudu kutekeleza majukumu ya nafasi ya ubunge kwa kiwango kikubwa na kuhakikisha anapatikana Mbunge mwenye uzalendo na maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kwa kuzingatia haki ya msingi ya uraia ya kupiga na kupigiwa kura, ni vyema Katiba ikatoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika maamuzi yenye maslahi kwa Taifa lao. Aidha, kuondoa masharti ya Katiba ya sasa ya kuhitaji mgombea awe mwanachama wa Chama cha Siasa ili kuweza kugombea nafasi ya uongozi. Kuwepo kwa Mgombea Huru kunaimarisha haki ya uraia na kupanua wigo wa demokrasia, kwa kutoa fursa kwa wananchi ambao siyo wanachama wa Vyama vya Siasa kushiriki katika chaguzi mbalimbali.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi kwamba nafasi ya Mgombea Huru iwepo kwa sababu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi kuchagua au kuchaguliwa. Suala la kuwepo kwa Mgombea Huru katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeshaagizwa na uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu iliyoipa Tanzania mwaka mmoja kuwa imetekeleza agizo hilo. Pia Mahakama ya Rufani ya Tanzania imeshalishauri Bunge lirekebishe Katiba na kuruhusu kuwepo kwa Mgombea Huru. Maamuzi haya ya Mahakama yalitokana na shauri la kupinga Mabadiliko ya Kumi na Moja ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yaliyoweka masharti ya mgombea nafasi ya uongozi kulazimika kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa. Mabadilko haya ya Katiba yalifanywa na Bunge ili kufuta uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania ulioruhusu Mgombea Huru.

### Ibara ya 126: Utaratibu wa Uchaguzi wa Wabunge

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba ya utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi na kuelekeza kila anayetaka kugombea nafasi ya Ubunge atalazimika kuwasilisha jina lake kwa Tume Huru ya Uchaguzi kwa utaratibu utakaowekwa na sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka msingi wa hiyari wa mtu kugombea ubunge na kuainisha utaratibu wa uchaguzi unaowezesha kupatikana kwa Wabunge. Lengo jingine ni kuandaa mazingira ya uwazi katika kuwapata wawakilishi wa wananchi Bungeni.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kumfanya mtu anayetaka kugombea ubunge kuthibitisha dhamira na nia yake ya kugombea ubunge kwa hiyari ili awajibike kwa uamuzi wake iwapo atachaguliwa kuwa mwakilishi wa wananchi.

Ubunge ni dhamana na ni vyema kabla ya mtu kuomba ridhaa ya wananchi kuwaongoza awe ametafakari kwa makini na kuthibitisha yeye mwenyewe kwa kuomba.

Sababu nyingine ni kukuza uwazi katika mchakato wa kuwapata wawakilishi wa wananchi bungeni.

**Ibara ya 127: Kiapo na Masharti ya Kazi ya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba ya kiapo cha Mbunge kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Bunge. Aidha, Ibara inaelekeza kuwa mishahara, posho na malipo mengine ya Mbunge yatakuwa kama yatakavyopangwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Aidha, Mbunge atawajibika moja kwa moja kwa wapiga kura wake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka msingi wa uwajibikaji wa Mbunge kwa wapiga kura wake. Pia kuwapa nguvu ya kikatiba wapiga kura kumuwajibisha Mbunge wao. Lengo jingine ni kuweka chombo huru nje ya Bunge kitakachopanga na kusimamia maslahi na posho za Mbunge.

Aidha, kuweka utaratibu wa kuwabana Wabunge kuheshimu, kutii na kulinda Katiba na dhamana yao kwa wapiga kura wao na kuainisha kikatiba masharti ya kushika nafasi ya ubunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ya masharti ya kula kiapo cha uaminifu na uwajibikaji kwa wananchi kunajenga msingi kuwa Mbunge kuwa na dhamana kwa wananchi waliomchagua. Katika baadhi ya nchi za Afrika baada ya uhuru nafasi ya ubunge iligeuzwa kuwa ni mahali pa kuchuma na kujinufaisha binafsi na siyo kuwatumikia wananchi kwa kujitolea.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuzingatia malalamiko ya wananchi wengi kuhusu tabia ya Wabunge kujiongezea posho mara kwa mara bila kujali hali ya maisha ya mwananchi wa kawaida. Ni muhimu kwa chombo cha wawakilishi wa wananchi kuwa na haiba, heshima na imani ya wananchi. Sababu nyingine ni kuashiria mwanzo wa utekelezaji wa madaraka ya Mbunge pamoja na kujenga imani ya wananchi kuwa Mbunge atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, umakini, haki na usawa.

**Ibara ya 128: Kupoteza Sifa za Ubunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya namna Mbunge atakavyopoteza sifa za ubunge. Ibara inaainisha masharti hayo kuwa ni pamoja na kukosa kuhudhuria mikutano ya Bunge miwili mfululizo bila ya ruhusa ya Spika wa Bunge, kuvunja

masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kujiuzulu, kujiondoa kwenye chama cha siasa kwa ridhaa yake, kufukuzwa au kuvuliwa uanachama, kushindwa kufanya kazi za Mbunge kwa muda wa miezi sita mfululizo kutokana na maradhi au kizuizi ndani ya gereza au kufariki dunia.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuhakikisha kwamba Mbunge anahudhuria vikao vyote na kutekeleza wajibu wake ipasavyo ili kuimarisha maadili na uadilifu kama yalivyoainishwa katika sheria za nchi.

Lengo jingine ni kuweka msingi wa mbunge aliyependekezwa na chama kuwajibika kwa vyama vyao vya siasa na kuainisha kikatiba sababu za kupoteza sifa za kuwa Mbunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni wa wananchi walisistiza kuwa na Wabunge wanaowajibika kwa wapiga kura wao, wenye maadili na mwenendo mzuri usio na ubinafsi. Sababu nyingine ni kuweka vigezo vya nidhamu na staha ndani na nje ya Bunge.

**Ibara ya 129: Haki ya Wapiga Kura Kumwajibisha Mbunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti mapya ya kuwapa haki wananchi ya kumuondoa Mbunge endapo atafanya mojawapo au zaidi ya mambo yafuatayo; kuunga mkono sera ambazo zinaenda kinyume na maslahi ya wapiga kura au kinyume na maslahi ya Taifa; kushindwa kuwasilisha au kutetea kwa dhati hoja zinazotokana na kero za wapiga kura wake; kuacha kuishi au kuhamisha makaazi yake kutoka eneo la Jimbo la Uchaguzi kwa zaidi ya miezi sita bila sababu za msingi; au mambo mengine yatakayoainishwa kwenye sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya mapendekezo ni kuwapa wapiga kura haki ya kumuondoa madarakani Mbunge wao kabla ya muda wake kwisha na kuweka vigezo na sababu ya wananchi kumuondoa Mbunge husika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliodai haki yao ya kumuondoa Mbunge wao kabla ya kumaliza muda wake ikiwa hatekelezi wajibu wake ipasavyo. Wananchi walio wengi walilalamika kwamba Wabunge wengi baada ya kuchaguliwa hawakai katika majimbo yao hadi msimu mwingine wa uchaguzi.

Uzoefu wa nchi nyingine zinazosimamia demokrasia shirikishi zikiwemo Uganda, Kenya na Brazili zimetambua haki ya wapiga kura kuwaondoa Wabunge wao.

Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuwalazimisha Wabunge kutekeleza ahadi wanazozitoa wakati wa kampeni na hivyo kuwafanya Wabunge waingie mkataba na wapiga kura wao.

**Ibara ya 130: Uamuzi wa Suala Kama Mtu ni Mbunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara ya hii ya Rasimu ya Katiba inaipa Mahakama Kuu mamlaka ya kusikiliza mashauri kwa ajili ya kutoa uamuzi juu ya suala la uhalali au vinginevyo wa uchaguzi wa Mbunge. Vivyo hivyo, Mahakama Kuu imepewa mamlaka ya kutangaza kama Mbunge amekoma kuwa Mbunge na kama nafasi ya madaraka ya ubunge iko wazi au hapana.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya mapendekezo haya ni kutoa mamlaka kwa Mahakama Kuu ambacho ni chombo cha mhimili mwingine kuamua uhalali wa Ubunge. Lengo jingine ni kuwawezesha wananchi kwenda mahakamani kuhoji uhalali wa Mbunge wao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 juu ya haki ya kufungua shauri Mahakama Kuu kuhoji matokeo ya Ubunge. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kuhalalisha au kubatilisha uchaguzi wa Mbunge pale ambapo imethibitika ulifanyika kinyume na utaratibu wa kisheria. Miongoni mwa haki ambazo wananchi wamezitumia kikamilifu ni ya kuhoji uhalali wa chaguzi wa Wabunge wao mahakamani. Hivyo mapendekezo haya ni kutekeleza maamuzi ya Mahakama Kuu juu ya haki ya wananchi kuhoji matokeo ya uchaguzi wa Mbunge.

**Ibara ya 131: Tamko Rasmi la Wabunge Kuhusu Maadili ya Uongozi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara ya hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kumtaka Mbunge awasilishe kwenye Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji nakala mbili za tamko rasmi akionyesha kuwa hajapoteza sifa za kuwa mbunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kubainisha uadilifu wa Mbunge na jinsi anavyozingatia maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 wa kuwataka Wabunge kutoa Tamko kuhusu maadili ya uongozi. Ibara hii inamtaka kiongozi awasilishe yeye mwenyewe Tamko kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji tofauti na ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ya mwaka 1977 ambapo Mbunge anawasilisha Tamko hilo kwa Spika. Kwa ujumla sababu za mapendekezo haya ni kulinda maadili ya uongozi.

## SEHEMU YA TATU

## UONGOZI WA BUNGE

### *(a) Spika na Naibu Spika*

**Ibara ya 132: Spika na Mamlaka ya Spika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mamlaka ya Spika ambaye atachaguliwa na Wabunge na inaweka masharti ya kikatiba inayowaondolea baadhi ya watu kuweza kuchaguliwa kushika madaraka ya Spika. Ibara hii inapendekeza Spika asitokane na Wabunge.

Pamoja na kuwa ndiye Kiongozi wa Bunge, pia atawakilisha Bunge katika vyombo na vikao vyingine vyote nje ya Bunge.

Watu ambao hawatakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Spika ni Waziri, Naibu Waziri, Mbunge au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yatakayotajwa na sheria za nchi.

Aidha, Spika atatakiwa ndani ya siku 30 tokea kuchaguliwa kwake kuwasilisha kwenye Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji Tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa za kuchaguliwa katika nafasi hiyo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuhakikisha kuwa Spika anatenda na anaonekana kutenda haki na kutoa fursa sawia kwa Wabunge wote. Kumfanya Spika kuwa huru na kumuondoshea Spika shinikizo la kichama katika kusimamia shughuli za Bunge ambacho ni chombo cha uwakilishi wa wananchi wote.

Aidha, ni kuweka msingi wa Spika kuzingatia maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuzingatia maoni ya wananchi kuwa Spika anapotoka kwenye chama inajitokeza kama sehemu ya chama chake na kuwanyima Wabunge wanaotoka nje ya chama chake fursa mbalimbali. Aidha, hutumika kuwadhibiti Wabunge wa chama chake mwenyewe hasa kwa wale ambao wanaonekana wanakengeuka mwelekeo wa chama.

**Ibara ya 133: Ukomo wa Spika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya ukomo wa Spika litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo: atachaguliwa kuwa Mbunge, kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika, lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika, ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa

Azimio la Bunge, atashindwa kuwasilisha tamko rasmi kuhusiana na mali na madeni yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uongo kwa kiapo kinyume cha sheria, itathibitika kuwa amevunja masharti ya Sheria inayohusu Maadili ya Uongozi wa Umma; au kufariki dunia.

Aidha, Ibara inaelekeza kuwa hapatakuwa na shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge kabla ya Spika kushika madaraka yake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka ukomo wa Spika kwa mujibu wa masharti ya Katiba.

Kuweka msingi wa kumuwajibisha Spika

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo ni kujenga uwajibikaji Kwa kuwa Spika kwa kumuwekea masharti ya kikatiba yatakayomfanya aondolewe katika nafasi yake anapokosa sifa za msingi za kuwa Spika au kufanya vitendo vinavyokiuka maadili na uadilifu.

**Ibara ya 134: Naibu Spika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Maudhui ya Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha nafasi ya Naibu Spika wa Bunge. Pia, inaainisha masharti ya sifa za mtu ambaye hataweza kuchaguliwa kuwa Naibu Spika ambayo ni sawa na yale yanayomhusu Spika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuhakikisha kuwa Naibu Spika anatenda na anaonekana kutenda haki na kutoa fursa sawa kwa Wabunge wote. Lengo jingine ni kumfanya Naibu Spika kuwa huru na kumuondoshea shinikizo la kichama katika kusimamia shughuli za Bunge. Aidha, kuweka msingi wa Naibu Spika kuzingatia maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo hayo ni kuwa Naibu Spika ndiye Msaidizi Mkuu wa Spika na ana dhamana inayofanana na Spika katika uongozi wa Bunge.

**Ibara ya 135: Sifa za Mtu Kuchaguliwa Kuwa Spika au Naibu Spika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanisha sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika. Sifa hizo ni pamoja na elimu ya chuo cha elimu ya juu, umri usiopungua miaka arobaini, na awe na sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge.

Aidha, Ibara hii inatoa ufafanuzi kuwa kiongozi yeyote wa juu wa chama cha siasa ambaye ni mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu, naibu katibu mkuu au mjumbe wa chombo chochote cha kitaifa chenye mamlaka katika chama cha siasa hawezi kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka sifa muafaka za mtu kuwa Spika au Naibu Spika wa Bunge. Pia, ni pamoja na kutenganisha ya maslahi ya kichama na uongozi wa shughuli za Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka Spika na Naibu Spika wasitokane na uongozi wa kitaifa wa chama chochote cha siasa kuepusha uwezekano wa mgongano wa kimaslahi au kupendelea chama chake.

Pia kujenga imani katika uongozi wa Bunge na kuweka taswira nzuri ndani na nje ya Bunge.

**Ibara ya 136: Utaratibu wa Uchaguzi na Kiapo cha Spika na Naibu Spika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa uchaguzi wa Spika na Naibu Spika watakaochaguliwa kwa kura za siri, kwa msingi kwamba endapo Spika atatoka upande mmoja wa Muungano, Naibu Spika atoke upande wa pili wa Muungano. Aidha, Ibara hii inaweka utaratibu wa kiapo cha Spika na Naibu Spika kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha utaratibu wa kumpata Spika na Naibu Spika. Pia, Ibara inainisha masharti ya kiapo cha Spika na Naibu Spika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Spika na Naibu Spika wanatii Katiba katika kutimiza wajibu wao na kujenga mazingira ya uaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Sababu ya kuweka nafasi ya Spika na Naibu Spika kutoka pande mbili tofauti za Muungano ni kuupa uongozi wa Bunge kuwa na sura ya Muungano.

***(b) Ofisi ya Bunge***

**Ibara ya 137: Katibu wa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya upatikanaji wa Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na ndiye atakayekuwa Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Katibu wa Bunge akiwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Bunge; na kuweka utaratibu mpya wa kumteua Katibu wa Bunge kwa kushirikisha Tume ya Utumishi wa Umma na vyombo vingine.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu utakaohakikisha kuwa nafasi ya Katibu wa Bunge inajazwa kwa kuzingatia sifa, weledi, uaminifu na uzoefu ndani ya Utumishi wa Umma.

**Ibara ya 138: Sekretarieti ya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza kuwepo kwa Sekretarieti ya Bunge ambayo itaundwa na watumishi kutoka pande mbili za Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia ngazi za utumishi kulingana na mahitaji ya shughuli za Bunge.

Aidha, Ibara hii inaipa Sekretariati ya Bunge wajibu wa kuhakisha utekelezaji bora wa shughuli za Bunge, Wabunge na madaraka ya Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Sekretarieti ya Bunge. Aidha, ni kuweka kikatiba majukumu ya Sekretariati ya Bunge ili kuunda Sekretariati imara yenye kuendeshwa kwa misingi ya weledi na ufanisi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka chombo cha utendaji kinachosaidia Bunge kutekeleza wajibu na shughuli zake kwa ukamilifu na ufanisi. Sababu nyingine ni kuweka bayana sura ya Muungano.

## SEHEMU YA NNE

## UTARATIBU WA SHUGHULI ZA BUNGE

**Ibara ya 139: Kanuni za Kudumu za Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu kutungwa kwa kanuni za kudumu za Bunge kwa ajili ya kuweka na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kutunga Kanuni za Kudumu za Bunge kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bunge. Pia, kudhihirisha uhuru wa chombo hicho kutunga kanuni zao wenyewe katika kuimarisha uwezo na uwajibikiaji kwa kujiwekea utaratibu wake wa kuendesha shughuli zake.

Lengo jingine ni kuweka uhakika na ulingano katika uendeshaji wa vikao vya Bunge na maamuzi yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Mabunge yote duniani wa kuwepo kanuni za uendeshaji wa Bunge kwa kujitungia wenyewe kanuni zao.

**Ibara ya 140: Rais Kulihutubia Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka wajibu kwa Rais wa kulihutubia Bunge katika mkutano wake kwanza na kulifungua rasmi. Pia, Ibara hii inampa Rais haki ya kulihutubia Bunge wakati wowote au kupeleka taarifa yoyote ambayo itasomwa na Waziri Mwandamizi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya ibara hii ni kumpa Rais wajibu wa kulihutubia na kulizindua rasmi Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kibunge duniani kote kwa Mkuu wa Nchi kulihutubia na kulifungua Bunge katika kikao chake cha kwanza.

Ni utaratibu wa Mabunge mengi duniani kwa Rais kulihutubia Bunge mara moja kwa mwaka ili kueleza sera, mipango, utekelezaji, mikakati na mwelekeo wa nchi. Utaratibu huu unajenga na kuimarisha mahusiano kati ya mihimili ya Serikali na Bunge katika kufikia malengo makuu ya taifa.

**Ibara ya 141: Mikutano ya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu kuhusu mikutano ya Bunge. Aidha, Ibara hii inatoa mamlaka kwa Rais kuweza kuitisha Bunge wakati wowote kwa mujibu wa masharti ya Katiba.

Pia, Ibara hii inaeleza kuwa Bunge litaitishwa katika sehemu ambayo kwa kawaida hufanywa vikao vya Bunge au mahala pengine popote atakapoelekeza Spika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya ibara hii ni kuweka utaratibu wa kuitishwa kwa mikutano ya Bunge na mahali pa kufanyiwa mikutano ya Bunge. Aidha, kumpa Rais mamlaka ya kikatiba ya kuitisha mikutano ya Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu na desturi ya Mabunge duniani kufanya mikutano ya Bunge na kumpa Mkuu wa Nchi nafasi ya kuliitisha Bunge inapohitajika kufanya hivyo. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kikatiba unaowezesha kikao cha Bunge kufanyika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano.

**Ibara ya 142: Uongozi na Vikao vya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha masharti ya kikatiba ya uongozi wa vikao vya Bunge na kuelekeza kuwa vikao hivyo vitaongozwa na Spika au Naibu Spika au Mbunge yeyote aliyechaguliwa na Bunge kwa ajili hiyo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka masharti ya uongozi, uendeshaji na usimamizi wa vikao vya Bunge Kikatiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu kwamba vikao vya Bunge vinaendeshwa kwa mujibu wa utaratibu wa kikatiba ili kuvifanya vikao hivyo kuwa halali. Vile vile ni kuweka uhakika wa kuwepo kwa viongozi na vikao vya Bunge wakati wowote.

**Ibara ya 143: Akidi ya Vikao vya Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya akidi ya vikao vya Bunge na utaratibu wa kufikia maamuzi ya Bunge kwa kuelekeza kuwa maamuzi yataamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za wabunge waliohudhuria na kupiga kura. Utaratibu hautahusika na masuala yaliyowekewa masharti mahsusi katika Katiba.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba akidi ya kila kikao cha Bunge ambacho ndicho kigezo cha maamuzi halali ya Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka akidi ya vikao vya Bunge ili kujenga imani ya kuwa maamuzi yanafikiwa kwa idadi ya kutosha ya Wabunge inayowakilisha mtazamo mpana wa wananchi wanaowawakilisha. Sababu nyingine ni kujenga uhalali wa vikao na kuhakikisha kwamba maamuzi ya vikao vya Bunge yanafikiwa kwa njia ya demokrasia.

Sababu nyingine kuzuia kuwepo hali ya utoro na kuhakikisha kuwa Wabunge wanahudhuria vikao na wanatelekeza shughuli za Bunge ipasavyo.

**Ibara ya 144: Kamati za Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha masharti ya kuundwa kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kulipa Bunge mamlaka ya kuunda kamati zake kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake. Lengo jingine ni kuongeza ufanisi kwa kuhakikisha kuwa maeneo muhimu yote yanaundiwa Kamati ili kuweza kufuatiliwa kikamilifu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuboresha na kupanua mijadala na maamuzi ya Bunge na kuhuisha utaratibu wa kibunge wa kuwa na Kamati za Bunge. Sababu nyingine ni kutimiza wajibu wa Bunge wa kuisimamia Serikali, na pale inapohitajika kuwaita na kuwahoji Mawaziri na watendaji wa Serikali kutoa ufafanuzi wa masuala yanayotakiwa na Kamati ya Bunge.

## SEHEMU YA TANO

## MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE

### Ibara ya 145: Uhuru wa Majadiliano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka misingi ya uhuru wa majadiliano Bungeni. Uhuru huu utakuwa wa kutoa mawazo, maoni na majadiliano na hautaingiliwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pamoja na uhuru huo Mbunge hatakiwi kutoa kauli za uongo, kuudhi au kumuumiza Mbunge au mtu mwengine yeyote katika jamii. Ibara hii inampa Mbunge kinga ya kutoshitakiwa Mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema ndani ya Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu uhuru wa majadiliano Bungeni. Aidha, kuwapa kinga Wabunge na kuondoa hofu, kupanua wigo wa ukweli na uwazi katika mijadala ya Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutoa nafasi kwa Wabunge kujadili kwa uhuru, umakini, uwazi na haki hoja zote zinazowasilishwa Bungeni kwa maslahi ya Taifa. Sababu nyingine kupewa kinga Wabunge ili wasiwe na woga katika kuikosoa Serikali na kufichua maovu. Aidha, kupewa kinga na fursa kwa Wabunge ni katika nguzo muhimu ya kuimarisha uhuru wa Wabunge katika majadiliano na maamuzi yao.

### Ibara ya 146: Mipaka ya Majadiliano Bungeni

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelezea masharti ya kikatiba kuhusu mipaka ya majadiliano Bungeni. Miongoni mwa mipaka hiyo ni marufuku kwa Mbunge kusema uongo na kwamba ahakikishe kauli au maelezo kuhusu jambo au suala lolote analiamini kuwa ni la kweli na sio jambo la kubuni au la kubahatisha.

Aidha, Ibara inataja maeneo ambayo Mbunge hatahesabika kuwa amesema uongo. Maeneo hayo ni pamoja na kufanya rejea iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari au nyaraka yoyote nyingine.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii kuweka mipaka ya kikatiba juu ya uhuru wa Wabunge katika majadiliano Bungeni na kuimarisha tabia na utamaduni kwa Wabunge kuwa wakweli na makini katika kauli zao Bungeni.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka mipaka kwa uhuru wa Wabunge wanapotoa maoni na hoja zao Bungeni pamoja na kwamba wana kinga na fursa ya kutoshtakiwa. Sababu nyingine ni kuwa chombo hiki kina watu ambao wanapima na kutafakari wanayoyasema yawe ya kweli na wanayoyatenda yazingatie haki kwa watu wengine ambao hawana nafasi ya kujibu hoja hizo Bungeni.

## SEHEMU YA SITA

## TUME YA UTUMISHI WA BUNGE

### *(a) Tume ya Utumishi wa Bunge*

**Ibara ya 147: Tume ya Utumishi wa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba Tume ya Utumishi wa Bunge. Aidha, Ibara inainisha wajumbe wa Tume kuwa ni Spika ambaye atakuwa ni mwenyekiti, Naibu Spika, Wabunge wawili, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mwanasheria Mkuu na Katibu wa Bunge ambaye ndiye atakuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Tume ya Utumishi wa Bunge kikatiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo ni kuwa na Tume inayosimamia uongozi wa Bunge kwa jumla katika mambo ya utumishi, ajira na nidhamu miongoni mwa watumishi wa Bunge.

**Ibara ya 148: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu inainisha majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge kuwa ni pamoja na kuajiri, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo na kusimamia nidhamu za watumishi wa Bunge na kupokea malalamiko dhidi yao kwa mujibu wa sheria za nchi; na kuandaa na kutekeleza mipango ya kujiendeleza kielimu kwa Watumishi wa Bunge.

Aidha, Ibara inataja jukumu jingine la Tume hii kuwa ni kuandaa na kupendekeza viwango vya mishahara, posho na marupurupu mengine kwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kwenye Tume ya Utumishi wa Umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Tume ya Utumishi wa Bunge na kuainisha majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutoa nafasi ya kusimamia mambo ya nidhamu miongoni mwa watumishi wa Bunge. Sababu nyingine ni kuyatambua kikatiba majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na kusimamia majukumu hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika taasisi ya Bunge.

(b) ***Mfuko wa Bunge***

**Ibara ya 149: Mfuko wa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Mfuko wa Bunge ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Mfuko huo utatumika kugharamia shughuli za uendeshaji wa Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Mfuko wa Bunge ili kulipa Bunge uhakika na uhuru wa kifedha.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuwa na mfuko mahsusi kwa ajili ya muhimili wa Bunge ili kunaimarisha dhana ya mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili ya Bunge na Serikali. Aidha ni kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa kuondoa urasimu uhusiana masuala ya fedha. Kwa sasa upo Mfuko wa Bunge ambao umeanzishwa kwa sheria ya kawaida ya Bunge.

## SURA YA KUMI

## MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO

## SEHEMU YA KWANZA

## MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA

### Ibara ya 150: Kuanzishwa kwa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha mfumo wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani. Aidha Ibara, hii inatamka kwamba mamlaka ya Mahakama ya utoaji haki yanatoka kwa wananchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na mfumo wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Katiba za nchi nyingi duniani kuanzisha na kutambua Mahakama kuwa ni moja ya mihimili ya dola yoyote. Kwa mara ya kwanza Rasimu hii inatamka bayana kuwa Mahakama inapata mamlaka na uhalali wake kutoka kwa wananchi.

### Ibara ya 151: Misingi ya Utoaji Haki

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kanuni za misingi za utoaji haki zinazopaswa kuzingatiwa na Mahakama katika utoaji wa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai. Aidha, Ibara inainisha baadhi ya misingi hiyo kuwa ni kutocheleweshwa haki bila ya sababu ya msingi, kutenda haki bila ubaguzi na kwa wakati, kutoa fidia inayostahili, kukuza na kuendeleza usuluhishi na kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya utoaji haki kikatiba.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya Wananchi wengi waliolalamika kuwa kwa sasa misingi ya utoaji haki haifuatwi na Mahakama, na kwamba uendeshaji na utoaji haki katika Mahakama umetawaliwa na tuhuma za rushwa, upendeleo na kupokea maelekezo kutoka kwa baaadhi ya viongozi wa ngazi za juu au wanasiasa.

Aidha, uwepo kwenye Katiba misingi ya utoaji haki kutaboresha utendaji kazi wa Mahakama. Pia wananchi walililalamikia juu ya Mahakama ya Rufani kutumia masharti ya kiufundi kufuta mashauri badala ya kutumia misingi ya utoaji haki inayozingatia maslahi ya wananchi na taifa.

Aidha, kujenga taswira mpya ya Mahakama kama chombo cha kutoa haki na kuonekana kutenda haki.

**Ibara ya 152: Uhuru wa Mahakama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inafafanua uhuru wa Mahakama katika utendaji wake wa kazi. Uhuru huo ni pamoja na kutokupewa maelekezo na mtu au chombo chochote; Majaji kuhakikishiwa kudumu kazini na mishahara na marupurupu yao kutokupunguzwa baada ya kuteuliwa na kinga ya kutoshtakiwa kwa jambo lolote alilofanya au kutolifanya katika utekelezaji wa shughuli za utoaji haki.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba uhuru wa Mahakama wa kutoingiliwa katika utekelezaji wa majukumu yake, kulinda haki, ajira na uhuru wa Majaji.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza uhuru wa Mahakama kama ni mmoja wa misingi mikuu ya demokrasia na utawala wa sheria. Aidha kuwapa Majaji uhuru ili kuwawezesha kutoa maamuzi yao bila ya woga wala upendeleo kwa kuzingatia misingi ya haki iliyoainishwa katika Katiba na sheria nyingine za nchi.

## SEHEMU YA PILI
## MUUNDO WA MAHAKAMA

### *a)Mahakama za Jamhuri ya Muungano*

**Ibara ya 153: Muundo wa Mahakama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka muundo wa Mahakama kwa kuzitaja Mahakama zitakazokuwa chini ya mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ni Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani. Ibara pia inazipa Mahakama Kuu za Tanganyika na Zanzibar mamlaka sawa katika usikilizaji wa awali wa masuala ya madai na jinai kuhusu mambo ya Muungano katika maeneo yao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka muundo mpya wa Mahakama katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi mbalimbali waliopendekeza mabadiliko ya muundo wa Mahakama kwa kuongeza Mahakama nyingine ya juu. Aidha, wananchi pia walisisitiza kuwa Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakama Kuu ya Tanganyika kuendelea kuwa na mamlaka ya usikilizaji wa awali wa masuala ya madai na jinai kwenye maeneo yao.

Sababu nyingine ni kuimarisha mfumo wa utoaji haki utakaoendana na muundo wa Muungano na Serikali zake.

### *b)Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano*

**Ibara ya 154: Mahakama ya Juu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba kwa mara ya kwanza Mahakama ya Juu katika Jamhuri ya Muungano. Aidha, Ibara inataja idadi ya Majaji wa Mahakama ya Juu, Rais wa Mahakama ya Juu ambaye atakuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu ambaye atakuwa Makamu wa Rais wa Mahakama ya Juu na kuelekeza uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano na kuweka vigezo vya uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Moja ya sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuzingatia maoni ya Wananchi ya kuwepo ngazi nyingine ya juu ya Mahakama ambayo itakuwa na mamlaka ya

kusikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama ya Rufani. Kwa kuwa Rasimu hii imeruhusu matokeo ya uchaguzi wa Urais kuhojiwa ilionekana kuwa chombo kinachofaa kufanya kazi hiyo ni Mahakama ya Juu kama ilivyo kwa Kenya na Uganda.

Sababu nyingine ni kuweka utaratibu ambapo mashauri ya kikatiba baina ya Serikali ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Washirika wenyewe kusikilizwa na Mahakama hiyo ya juu,

**Ibara ya 155: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Juu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka kikatiba akidi ya vikao vya Mahakama ya Juu katika kusikiliza shauri lililopo mbele yake. Aidha, ibara inaelekeza kuwa uamuzi wa Mahakama utafuata kauli ya majaji walio wengi waliosikiliza shauri husika na kuweka akidi ya Majaji wa Mahakama ya Juu kuwa ni watano.

Hata hivyo akidi inayohusu mambo yalioainishwa katika Ibara 156 (1)(a), (b),(c) na (e) itazingatia uwakilishi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la kuweka kikatiba akidi ya Majaji inayotakiwa kwenye vikao vya Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kusikiliza kesi na kutoa maamuzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kawaida katika uendeshaji wa Mahakama ya Juu na akidi ya Majaji wanaosikiliza shauri kwa pamoja. Msingi wake ni kuongeza uhalali na uhakika wa kutoa haki katika kusikiliza na kuamua rufaa kwa kuwashirikisha Majaji wengi kwa sababu hatua hiyo ni ya mwisho kwa raia.

**Ibara ya 156: Mamlaka ya Mahakama ya Juu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mamlaka, majukumu na wajibu wa Mahakama ya Juu. Mamlaka hayo ni pamoja na kusikiliza mashauri mbalimbali ikiwemo matokeo ya uchaguzi wa Rais, mashauri yatakayowasilishwa na Nchi Washirikia kuhusu tafsiri au utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kusikiliza na kuamua migogoro baina ya Nchi Washirika au Nchi Washirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kutoa ushauri wa kisheria. Aidha, inatoa utaratibu wa Mahakama za Nchi Washirika kulazimika kufuata uamuzi wa Mahakama ya Juu.

Aidha, Ibara hii inaipa Mahakama ya Juu mamlaka ya kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi za Washirika pale itakapoombwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuainisha mamlaka na madaraka ya Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano ambayo ndiyo yenye maamuzi ya mwisho.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya Ibara hii ni kuzingatia na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa chombo cha juu zaidi cha kutoa haki.

Kutokana na mapendekezo ya Rasimu ya Katiba kuwa matokeo ya Rais yahojiwe Mahakamani ilionekana ni vyema kufuata uzoefu wa nchi nyengine kama Kenya na Uganda ambapo mashauri kama hayo husikilizwa na Mahakama ya Juu pekee.

Kwa kuwa Rasimu inakusudia mizozo ya Muungnao itatuliwe kwa njia za kimahakama kuliko kisiasa kama ilivyo sasa, ndipo Rasimu ikapendekeza Mahakama ya Juu kuwa na mamlaka ya kusikiliza mashauri ya tofauti za kikatiba katika kutekeleza mambo ya Muungano baina ya Washirika wenyewe au Washirika na Muungano na Jamhuri ya Muungano.

**Ibara ya 157: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu pamoja na masharti ya utendaji wao wa kazi, Ibara hii inawahuruhusu Majaji kukamilisha mashauri ambayo yalikuwa mbele yao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Ni kuweka kikatiba madaraka na wajibu wa Majaji Mahakama ya Juu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwa Jaji anayeteuliwa kwenda Mahakama ya Juu. Hii itamuwezesha kusikiliza na kuamua mashauri aliyokuwa anayasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu ili kuwe na mwendelezo wa kusikiliza mashauri na kupunguza au kuondoa mlundikano wa kesi zinazoachwa na Majaji waliopandishwa vyeo.

***(c) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu***

**Ibara ya 158: Uteuzi wa Jaji Mkuu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa uteuzi na sifa za mtu kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu na mamlaka yake. Ibara inataja sifa hizo kuwa ni pamoja na kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano, muadilifu, mwenye tabia njema, umri usiopungua miaka 45 na uzoefu wa kuwa Jaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika kwa muda wa miaka ishirini au kufanya kazi katika Utumishi wa Umma. Pia, anaweza kuwa ni mwana taaluma kwa muda usiopungua miaka ishirini

mfululizo na mwenye sifa za kusajiliwa kuwa wakili. Ibara hii kwa mara ya kwanza inaweka utaratibu wa Jaji Mkuu awe ni raia wa Tanzania.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara ni kuweka sifa na utaratibu wa kupatikana kwa Jaji Mkuu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuhuisha utaratibu wa kuweka na vigezo vya uteuzi wa Jaji Mkuu ambaye ndiye kiongozi wa mhimili wa Mahakama. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo na uwazi na kutoa fursa sawa kwa watu wenye uwezo, uadilifu na uaminifu katika kutoa haki kupata nafasi.

Aidha walitaka kuwepo kwa vyombo vingine vya kikatiba vya kumshauri na kumsaidia Rais kufanya teuzi mbalimbali za Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali na teuzi hizo kuthibitishwa na Bunge.

## Ibara ya 159: Uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa uteuzi, sifa za mtu kuteuliwa kuwa Naibu Jaji Mkuu na Mamlaka yake. Aidha, inaweka masharti kwamba, Jaji Mkuu akitoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Naibu Jaji Mkuu atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

Ibara inataja sifa za kuteuliwa kuwa Naibu Jaji Mkuu ni pamoja na kuwa raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa na tabia njema, mwaminifu na muadilifu. Aidha, Naibu Jaji Mkuu atatokana na Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika. Pia mtumishi wa umma au mwanataaluma mwenye sifa ya kusajiliwa kuwa wakili kwa miaka 15 mfululizo pia anaweza kuteuliwa kuwa Naibu Jaji Mkuu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kwa mara ya kwanza nafasi ya Naibu Jaji Mkuu na kuweka sifa na utaratibu wa kikatiba wa kupatikana kwake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuzingatia maoni ya wananchi juu ya umuhimu wa Naibu Jaji Mkuu ambae pia atakaimu nafasi ya Jaji Mkuu anapokuwa hayupo au ameshindwa kazi. Aidha, nafasi ya Naibu Jaji Mkuu itaweka sura ya Jamhuri ya Muungano katika uongozi wa Mahakama ya Juu.

## Ibara ya 160: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa uteuzi na sifa za mtu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu. Aidha, Majaji wa Mahakama ya Juu watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa orodha ya majina yaliyopedekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Sifa za kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu ni sawa na zile za Naibu Jaji Mkuu.

### b. Madhumuni na Lengo

Kuanzisha Jaji wa Mahakama ya Juu na kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Naibu Jaji Mkuu.

### c. Sababu za Mapendekezo

Ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa uwazi na kutoa fursa sawa kwa watu wenye uwezo, uadilifu na uaminifu katika kutoa haki, kupata nafasi ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Makahama ya Juu. Pia ni kuweka vyombo vyengine vya kikatiba vya kumshauri na kumsaidia Rais kufanya teuzi mbalimbali za Majaji wa Mahakama ya Juu.

## Ibara ya 161: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelezea utaratibu wa kiapo cha Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu kabla ya kushika madaraka yao.

### b. Madhumuni na Lengo

Kuweka utaratibu wa kikatiba wa kiapo cha Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu. Kujenga imani kwa wananchi kuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kiapo.

### c. Sababu za Mapendekezo

Kuwataka Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu kutii na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekeleza wajibu wao kwa haki, uaminifu na uadilifu.

## Ibara ya 162: Muda wa Kuwa Madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Juu.

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka umri wa kustaafu kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Majaji wa Mahakama ya Juu kuwa ni miaka 70. Pia Ibara hii inaweka masharti ya kukoma utumishi wao kabla ya kufikisha umri wa kustaafu. Hii ni pamoja na kujiuzulu, kushindwa kutekeleza majukumu kutokana na maradhi, kufariki dunia au kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Katiba.

Pia sharti jengine la kuweza kubakia katika nafasi yake pamoja na kutimiza umri wa miaka 70 ya kustaafu ni kumaliza shauri ambalo liko mbele yake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Majaji wa Mahakama ya Juu kushika madaraka.

Pia ni kuweka masharti ya wazi ya kikatiba kuhusu muda na ukomo wa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kawaida wa kustaafu Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama. Aidha, ni muhimu katiba ikatamka bayana sababu nyengine ambazo zinaweza kumfanya Jaji aondolewe katika nafasi yake na sababu hizo zaweza kuwa za kiafya, kiutendaji na kimaadili.

Kutanabahisha Jaji, Naibu Jaji au Jaji wa Mahakama ya Juu kuhusu unapokaribia muda wake wa kustaafu kumaliza mashauri yaliyo mbele yake kuelekea muda wa kustaafu.

## Ibara ya 163: Utaratibu wa Kukaimu Nafasi ya Jaji Mkuu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa kikatiba wa Naibu Jaji Mkuu kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu inapokuwa wazi au akiwa amesafiri au ameshindwa kutekeleza majukumu yake.

Aidha, Ibara hii pia inaeleza jinsi ya nafasi ya Naibu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahakama ya Juu inapotokea moja ya nafasi hizo kuwa wazi na mamlaka na madaraka ya Kaimu Naibu Jaji Mkuu, au Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu atakavyopatikana.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba masharti ya kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu inapokuwa wazi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuhakikisha kuwa wakati wote kuna mtu anaeshika nafasi ya a Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu inapotokea kuwa wazi. Sababu nyingine ni kuepusha kuwepo kwa ombwe la uongozi na usikilizaji wa mashauri na hivyo kuwanyima au kuchelewesha wananchi haki yao.

## Ibara ya 164: Utaratibu wa Kushughulikia Nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa kikatiba wa kushughulikia masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu isipokuwa watu walioteuliwa

kukaimu nafasi ya Ujaji. Aidha, Ibara hii inaainisha sababu na hatua zinazoweza kutumika katika kuweza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Jaji.

Jaji hataondolewa kwa sababu za kinidhamu hadi kwanza Rais aunde Tume ya Uchunguzi ambayo nusu ya wajumbe wake watakuwa ni Majaji kutoka nchi zilizo katika Jumuia ya Madola. Jaji ataondolewa iwapo Tume hiyo itapendekeza kuwa Jaji huyo baada ya kumchunguza kuwa hana sifa ya kuendelea kuwa Jaji.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba utakaofuatwa katika hatua zote za kushughulikia nidhamu za Majaji wa Mahakama ya Juu. Lengo lingine ni kuweka mfumo bora utakaosimamia na kushughulikia masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu na kujenga nidhamu na uadilifu katika Mahakama ya Juu.

**c. Sababu ya Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kulinda Mahakama na kuhakikisha kuwa hatua za kinidhamu zinazochukuliwa zinatenda haki kwa Mahakama na kwa Jaji anayehusika. Utaratibu huu unaondoa hofu ya Jaji kuondolewa kwa mizengwe au hila pindi akitoa uamuzi dhidi ya dola.

Sababu nyingine ni kuendeleza utaratibu wa kinidhamu wa Majaji ndani ya Jumuiya ya Madola.

### ***(d) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya muungano***

**Ibara ya 165: Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na kuweka idadi ya Majaji wa Mahakama ya Rufani, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani na Majaji wasiopungua 17 kwa kuzingatia uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha Mahakama ya Rufani na muundo wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuendelea na utaratibu wa kuwa na Mahakama moja ya Rufani katika Jamhuri ya Muungano ili kutoa nafasi kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika kukata rufani mbele zaidi.

Sababu nyingine ni kuwepo kwa Mahakama moja ya Rufani itakayokuwa na Mamlaka na madaraka ya kusikiliza rufani itakayowasilishwa kutoka Mahakama Kuu za Nchi Washirika.

**Ibara ya 166: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kikatiba juu ya akidi ya vikao vya Mahakama ya Rufani katika kusikiliza shauri lililopo mbele yake. Akidi hiyo ni ya Majaji watatu kwa kila kikao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka kikatiba akidi ya Majaji inayotakiwa kwenye Mahakama ya Rufani kwa ajili ya kusikiliza na kutoa maamuzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kurahisisha utendaji kazi wa Mahakama ya Juu na kutoa uhalali wa maamuzi yatakayofikiwa na Mahakama hiyo.

**Ibara ya 167: Mamlaka ya Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mamlaka, majukumu na wajibu wa Mahakama ya Rufani ya kusikiliza mashauri mbalimbali yatakayowasilishwa na Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya Nchi Washirikia iliyopewa mamlaka maalum ya kusikiliza mashauri ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu. Pia inaipa mamlaka Mahakama ya Rufani ya kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu ya Nchi Washirika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba juu ya mamlaka na madaraka ya Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na kuipa uwezo wa kusikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi mbalimbali ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa Mahakama moja ya Rufani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayosikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika.

**Ibara ya 168: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani pamoja na masharti ya utendaji wao wa kazi. Ibara pia inamruhusu Jaji aliyeteuliwa kuingia katika Mahakama ya Rufani kukamilisha mashauri aliyokuwa anasikiliza kabla ya uteuzi wake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya madaraka na wajibu wa Majaji wa Mahakama ya Rufani katika kutekeleza wajibu wao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwa Jaji anayeteuliwa kwenda Mahakama ya Rufani amalize kusikiliza mashauri aliyokuwa anayasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani ili kuwa na mwendelezo wa kusikiliza mashauri na kupunguza au kuondoa mlundikano wa kesi zinazoachwa na Majaji waliopandishwa vyeo.

**Ibara ya 169: Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inanzisha nafasi mpya ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani na inaweka utaratibu wa uteuzi na sifa za mtu atakayeweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atakayetekeleza kazi na shughuli zake kwa maelekezo au kama atakavyopangiwa na Jaji Mkuu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuwa na utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atakayekuwa Kiongozi wa Mahakama ya Rufani badala ya utaratibu uliyomo katika katiba ya Jamhuri ya Mwaka 1977 ambapo Jaji Mkuu ndiye Kiongozi wa Mahakama ya Rufani.

**Ibara ya 170: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. Aidha, inaainisha utaratibu wa uteuzi, sifa na wajibu wa mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. Pia, Ibara inaweka masharti kwamba Mwenyekiti akiteuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano Makamu Mwenyekiti atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu kuu mbili za mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa ombwe iwapo Mwenyekiti hatakuwepo na kuupa uongozi wa Mahakama ya Rufani sura ya Muungano.

### Ibara ya 171: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa uteuzi na sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Aidha Ibara inaelekeza kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani atateuliwa na Rais kutoka orodha ya majina yatayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Ibara hii isomwe pamoja na Ibara 169 (3) ya Rasimu ya Katiba.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba na sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa watu wanaoteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani wanakuwa na sifa na uwezo stahiki, na wamepatikana kwa utaratibu wa wazi na wa ushindani.

### Ibara ya 172: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani kabla ya kushika madaraka yao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwataka Majaji wa mahakama ya Rufani kutii na kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa haki kwa uadilifu bila upendeleo au huba.

### Ibara ya 173: Muda wa Kuwa Madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inataja umri wa kustaafu kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Majaji wa Mahakama ya Rufani. Pia Ibara inaweka masharti ya Majaji wa Mahakama ya Rufani kukoma utumishi wao kabla ya kufikisha umri wa kustaafu. Aidha, Ibara inaelekeza kuwa iwapo Jaji wa Mahakama ya Rufani atafikisha umri wa kisheria wa kustaafu atalazimika kuendelea na kazi ili aweze kukamilisha mashauri yote aliyoanza kuyasikiliza kabla ya kutimiza umri wa kustaafu.

b. **Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba umri wa kustaafu na muda wa kushika madaraka kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani.

c. **Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba wa kutamka wa umri wa kustaafu kwa Majaji.

Aidha, mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka Majaji wanaostaafu kabla ya kumaliza mashauri waliyoanza kusikiliza wamalize kazi zao ili kuharakisha utoaji wa haki na kuwapunguzia usumbufu wananchi.

## Ibara ya 174: Utaratibu wa Kukaimu Nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani

a. **Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanisha utaratibu wa kikatiba wa Makamu Mwenyekiti kukaimu nafasi ya Mwenyekiti. Aidha inaweka utaratibu wa kukaimu nafasi ya Makamu Mwenyekiti au Jaji wa Mahakama ya Rufani inapotokea moja ya nafasi hizo kuwa wazi.

b. **Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba unaopaswa kufuatwa katika kujaza nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Jaji wa Mahakama ya Rufani ikiwa wazi.

c. **Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa kila wakati kuna mtu anayeshika nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Jaji wa Mahakama ya Rufani kuwa wazi kwa sababu yoyote iliyoainishwa kwenye Katiba.

## Ibara ya 175: Utaratibu wa Kushughulikia Nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani

a. **Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu Katiba inaainisha utaratibu wa kikatiba wa kushughulikia masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani ambao ni sawa na ule wa Majaji wa Mahakama ya juu ulioanishwa katika 164 ya Rasimu ya Katiba.

b. **Madhumuni ya Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa mfumo bora utakaosimamia na kushughulikia masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.

c. **Sababu ya Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kulinda uhuru wa Majaji na hadhi ya Mahakama kwa kuweka utaratibu utakaotenda haki kwa Mahakama na Jaji anayehusika kuchunguzwa.

### (f) *Usimamizi wa Shughuli za Mahakama*

**Ibara ya 176: Msajili Mkuu wa Mahakama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu inaanisha uwepo wa nafasi ya Msajili Mkuu wa Mahakama na sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Msajili Mkuu wa Mahakama na upatikanaji wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuimarisha utendaji kazi wa shughuli za kimahakama katika utoaji wa haki. Aidha, ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambao una mfumo wa Mahakama kuwa na Msajili wa Mahakama kwa ajili ya kuratibu uendeshaji wa shughuli za kimahakama. Sababu nyingine ni kutambua kuwa Msajili Mkuu wa Mahakama ndiye kiungo kati ya Majaji na watumishi wengine wa katika kutekeleza majukumu ya kimahakama.

**Ibara ya 177: Majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama ambayo ni pamoja na kuratibu shughuli na masuala ya kimahakama. Msajili Mkuu wa Mahakama anawajibika kwa Jaji Mkuu ikiwa ni pamoja na kutekeleza kazi nyengine atazopangiwa na Jaji Mkuu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kwenye Katiba masharti yanayohusu majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama. Sababu nyingine ni kumpa Msajili wa Mahakama dhamana na wajibu wa kusimamia shughuli za kimahakama na kuhakisha zinafanyika kwa ufanisi na kwa utaratibu uliowekwa.

**Ibara ya 178: Mtendaji Mkuu wa Mahakama**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakayeteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. Mtendaji Mkuu wa Mahakama atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi wa umma kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma na ataidhinishwa na Bunge. Aidha, Ibara hii inaelekeza kuwa, Mtendaji Mkuu wa Mahakama atwajibika kwa Jaji Mkuu. Ibara hii inaainisha sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambazo

ni kuwa mtumishi mwandamizi wa umma, mwenye uweledi na uzoefu katika masuala ya utawala na fedha.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama mwenye dhamana ya kusimamia utawala, fedha na mipango ya maendeleo ya Mahakama.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuimarisha utendaji wa Mahakama kwa kuwa na mtaalamu wa utawala, fedha na mipango tofauti na ilivyokuwa kabla kwa nafasi hii kushikiliwa na Msajili Mkuu wa Mahakama.

Sababu nyingine ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama.

Halikadhalika ni kuzingatia na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa vyombo vya Kikatiba vya kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa nafasi mbalimbali za Watendaji Wakuu wa Serikali na teuzi hizo kuidhinishwa na Bunge.

## Ibara ya 179: Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kikatiba majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Majukumu hayo ni pamoja na kuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ofisa Masuuli wa Mahakama na msimamizi mkuu wa Mfuko wa Mahakama na masuala ya utawala ya Mahakama. Mtendaji Mkuu wa Mahakama atawajibika kwa Jaji Mkuu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka kwenye Katiba masharti yanayohusu majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama kwa kumuweka mtendaji mahsusi katika mfumo wa Mahakama anayesimamia masuala ya fedha na utawala. Uzoefu wa nchi nyingine kama Jamhuri ya Ireland yenye Mtendaji Mkuu wa Mahakama umeonyesha ufanisi mkubwa katika utendaji wa kila siku wa shughuli za Mahakama.

## SEHEMU YA TATU

## TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA NA MFUKO WA MAHAKAMA

### *(a) Tume ya Utumishi wa Mahakama*

### Ibara ya 180: Tume ya Utumishi wa Mahakama

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Tume ya Utumishi Mahakama, muundo wake, idadi ya wajumbe na taratibu za vikao vya Tume. Wajumbe wake ni pamoja na Jaji Mkuu ambaye ni Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu, Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani, Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar, wawakilishi wawili wa Vitivo vya Sheria kutoka vyuo vikuu mmoja kutoka Tanganyika na mmoja kutoka Zanzibar na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye ndiye atakuwa Katibu.

Tume inaweza kumualika mtu yeyote mwenye utaalamu mahsusi isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Utumishi wa Mahakama na kuainisha kazi na majukumu ya Tume hiyo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuendeleza utaratibu uliopo Tanzania na katika nchi mbalimbali duniani wa kuwepo Tume ya Utumishi wa Mahakama. Aidha kuwepo kwa utaratibu huo kunaweka bayana utengano wa mihimili ya dola katika kutekeleza majukumu yao.

Pia, Ibara inaipa Mahakama, chombo ambacho kinaimarisha uhuru na mamlaka ya Mahakama kwa kushughulikia ajira, nidhamu na maslahi ya watendaji wa Mahakama. Sababu nyingine ni kuwa, chombo hiki kitahakikisha kuwepo kwa uwiano wa wajumbe wa Tume wa Mahakama kutoka pande mbili za Muungano.

### Ibara ya 181: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo ni pamoja na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufaani, Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani na Majaji wa Mahakama ya Juu.

Jukumu jingine la Tume hii ni kuajiri Wasajili na watumishi wengine wa Mahakama na kusimamia maslahi na nidhamu yao.

Aidha, Ibara inaelekeza kuwa Tume inaweza kukasimu madaraka yake kwa kamati mbalimbali zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka kikatiba majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ikiwa ni moja ya vyombo vinavyoimairisha ufanisi na utendaji wa mahakama kwa kusimamia maendeleo ya Mahakama na watumishi wake. Aidha chombo hiki kitasimamia nidhamu ya watumishi wa Mahakama ambao si Majaji ili kuimarisha uhuru wa Mahakama.

### Ibara ya 182: Uanachama Katika Vyama vya Siasa

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inapiga marufuku Majaji wote, Msajili Mkuu wa Mahakama, Msajili wa ngazi yoyote na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuwa wanachama wa chama chochote cha siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuwazuia Majaji na viongozi wengine wa Mahakama kuwa wanachama wa Vyama vya Siasa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za Mapendekezo haya ni kutambua kuwa Mahakama ni chombo cha utoaji haki ambacho viongozi na watumishi wake wa juu ni lazima waonekane wanatenda kwa haki bila ya tashwishi. Sababu nyingine ni kuondoa uwezekano wa watumishi wa Mahakama kufanya maamuzi ya mashauri kwa huba au ushawishi wa kisiasa.

Rasimu imependekeza Ibara hii ili wananchi wawe na imani kuwa Mahakama itatenda haki kwa watu wote bila kujali itikadi za Vyama vya Siasa.

## *(b) Mfuko wa Mahakama*

### Ibara ya 183: Mfuko wa Mahakama

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba Mfuko wa Mahakama wa Jamhuri ya Muungano na kuainisha kazi zake, majukumu yake na upatikanaji wa fedha za kuendesha Mfuko huo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Mfuko wa Mahakama na kuainisha majukumu yake.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu ulioanzishwa wa kila mhimili kuwa na Mfuko wake wa kusimamia gharama za utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, Mfuko huu utaimarisha uhuru na mamlaka ya Mahakama kwa kuwa na uhakika wa fedha za kugharamia shughuli zake.

## SEHEMU YA TATU

## SURA YA KUMI NA MOJA

## UTUMISHI WA UMMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

### Ibara ya 184: Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka Utumishi wa Umma wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya Katiba. Aidha, inaainisha misingi na kanuni kwamba utumishi wa umma ni dhamana kutoka kwa wananchi na hivyo mtumishi anatakiwa kutumikia wananchi kwa uadilifu na uaminifu. Vilevile, kudumisha na kukuza viwango vya juu vya maadili ya kitaaluma, na kuhakisha kwamba ajira na uteuzi katika nafasi mbalimbali vinazingatia uwezo wa kitaaluma, weledi, ujuzi, umakini na uzoefu katika eneo husika.

Pia, kutoa huduma kwa umma kwa njia ya haki, usawa na bila upendeleo. Misingi hii itatumika katika mihimili yote ya dola, taasisi na idara zote za Serikali, mashirika, makampuni na wakala wa Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kutambua kikatiba Utumishi wa Umma wa Jamhuri ya Muungano na kuainisha misingi mikuu na kanuni za Utumishi wa Umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kujua kuwa Utumishi wa Umma ni nguzo muhimu ya mhimili wa Serikali na hivyo kutakiwa kutambuliwa, kukuzwa, kuimarishwa na kusimamiwa kikatiba. Kujenga mazingira ya kuwa na Utumishi wa Umma uliotukuka. Kujenga misingi mikuu ya Utumishi wa Umma itakayotumiwa na mtendaji wa umma katika kutoa huduma kwa jamii bila ya ubaguzi wa aina yoyote wa kijinsi, rangi, kabila, dini au mahali anapotoka mtu anayehitaji huduma hiyo.

### Ibara ya 185: Ajira na Uteuzi wa Viongozi Katika Taasisi za Serikali

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti yanayohusu ajira na uteuzi wa viongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taasisi zake. Aidha, Ibara inaelekeza kuwa ajira na uteuzi utafanywa kwa kuzingatia taaluma, uweledi, ushiriki na uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu ajira katika Utumishi wa Umma na uteuzi wa viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Taasisi zake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwa na sifa na taratibu za kuzingatiwa katika ajira ndani ya Utumishi wa Umma katika Serikaili ya Jamhuri ya Muungano na Taasisi zake. Aidha, kuweka msingi wa kuzingatia uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mapendezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliodai kuwa Zanzibar haishirikishwi kikamilifu katika ajira za Muungano na kuwa kero za muda mrefu.

**Ibara ya 186: Tume ya Utumishi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Tume ya Utumishi ya Umma wa Jamhuri ya Muungano ambayo itaongozwa na Mwenyekiti na kuwa na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, Ibara hii inaainisha sifa za Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma ambazo ni pamoja na kuwa na uzoefu katika utumishi wa umma; upeo mkubwa katika mambo ya utumishi, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka 10.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Utumishi wa Umma na uongozi wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya kuipa hadhi na madaraka ya kikatiba Tume ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake na kutoa uhuru unaostahiki. Aidha, ni kutambua jukumu kubwa liliopewa Tume hii kumshauri Rais kuhusu teuzi mbalimbali.

**Ibara ya 187: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatambua kuwepo kwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma atakayeteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge. Aidha, Ibara inatamka kuwa Katibu wa Tume atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu na mtekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Tume.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia utaratibu uliozoeleka wa tume za aina hii kuwa na Katibu ambaye ndiye Mtendaji Mkuu na msimamizi wa shughuli za Tume.

**Ibara ya 188: Mamlaka ya Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu na mamlaka ya Tume ya Utumishi wa Umma na kutamka kuwa kitakuwa ndicho chombo cha juu katika Utumishi wa Umma chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya utumishi wa umma. Aidha, Ibara hii inaainisha majukumu ya Tume ya Utumishi wa Tume ambayo ni pamoja na: kumshauri Rais juu ya uteuzi wa viongozi katika nafasi mbalimbali za utumishi wa umma, kutoa miongozo mbalimbali ya kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa umma na kuhamasisha utekelezaji wa misingi na kanuni za utumishi katika Sekta zote za Utumishi wa Umma.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba mamlaka na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kuwa Tume ya Utumishi wa Umma ina wajibu na dhamana kubwa kwa Serikali na taifa wa kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wana weledi, uzoefu, uadilifu, na uaminifu katika utumishi wao. Chombo hiki ndicho kinachohakikisha kuwa viongozi wanaoteuliwa na Rais ni wale wenye sifa zilizoainishwa katika sheria na kanuni mbalimbali za Utumishi wa Umma.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuongeza uwajibikaji wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa kusimamia misingi mikuu ya Utumishi wa Umma.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIASA

## SEHEMU YA KWANZA

## UWAKILISHI WA WANANCHI

### Ibara ya 189: Ushiriki Katika Uchaguzi na Kura ya Maoni

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa haki ya kupiga kura kwa kila raia wa Jamhuri ya Muungano mwenye umri wa miaka 18 na akili timamu. Pia inaweka haki ya kuandikishwa na kushiriki kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni. Aidha, Ibara hii inaweka masharti kwa mamlaka ya kusimamia uchaguzi kuzingatia misingi kuwa wananchi watatumia haki ya kisiasa kwa mujibu wa Katiba na uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Ibara pia inaainisha sifa za uchaguzi huru na haki kuwa ni kura ya siri, kutokuwepo matumizi ya nguvu, vitisho, vishawishi wala rushwa. Pia, Ibara hii inatoa madaraka kwa mamlaka itakayosimamia uchaguzi kutangaza majimbo kwa madhumuni ya uchaguzi wa Wabunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ni kuweka haki ya kuandikishwa na kupiga kura au kura ya maoni.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua na kulinda haki ya msingi ya kila raia ya kupiga kura ambayo ni lazima itambuliwe na kulindwa na Katiba. Aidha, ni muhimu kwa Katiba kuweka mfumo wa wazi wa utaratibu wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi na kura ya maoni na kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata nafasi za uwakilishi katika vyombo vya kutunga sheria.

## SEHEMU YA PILI

## TUME HURU YA UCHAGUZI

### *(a) Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi*

**Ibara ya 190: Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaunda kikatiba Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano. Tume hii ndiyo itakayosimamia masuala ya uchaguzi na kura za maoni. Aidha, inaweka masharti ya upatikanaji wa wajumbe wake kwa uwazi kupitia utaratibu wa kuomba nafasi na kuchujwa na Kamati ya Uteuzi kabla ya kuteuliwa rasmi na Rais. Aidha, inapendekezwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wathibitishwe na Bunge. Pia inaweka sifa za watu wanaoweza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume.

Ibara hii inazuia wafuatao kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi: Mbunge wa Jamhuri ya Muungano, Mbunge wa Bunge la Tanganyika, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Diwani katika Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha kikatiba Tume Huru ya Uchaguzi na kuainisha sifa za wajumbe wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ambao wamekuwa wanadai kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi. Tume Huru ya Uchaguzi ni chombo muhimu katika mfumo wa utawala wa kidemokrasia. Aidha uchaguzi huru na wa haki ndiyo njia ya kuwapata viongozi wa taifa wenye ridhaa ya wananchi. Sababu nyingine ya mapendekezo haya yamezingatia misingi inayokubalika duniani ya vyombo huru vya usimamizi wa uchaguzi ambayo ni: uhuru, uadilifu, uwajibikaji na uwazi.

**Ibara ya 191: Kamati ya Uteuzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Kamati ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi. Pia, Ibara hii inaainisha Wajumbe wa Kamati ya Uteuzi pamoja na utaratibu wa upatikanaji wao. Wajumbe hao ni Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Mwenyekiti, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Spika wa Bunge la Tanganyika, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Jaji Mkuu wa Tanganyika, Jaji Mkuu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi na Uwajibikaji.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na kuainisha majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo zimezingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi wateuliwe kwa mfumo wa wazi na unaotoa fursa kwa watu wengi kuomba au kupendekezwa kuwa wajumbe.

Sababu nyingine ni kuondoa dhana ya chombo hiki muhimu kutumiwa na mamlaka iliyokiteua na hivyo kutoaminika na pia kuweka utaratibu wa uwazi katika upatikanaji wa wajumbe wa Tume na kujenga ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

**Ibara ya 192: Ukomo wa Kushika Nafasi ya Madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu ukomo wa Mjumbe wa Tume kushika nafasi ya madaraka katika Tume Huru ya Uchaguzi. Ukomo uliowekwa wa kushika nafasi hiyo ni wa kipindi cha miaka mitano na uwezekano wa mjumbe kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitano. Aidha, Ibara hii inaweka masharti ya kupoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa kukiuka masharti ya kanuni za maadili. Ibara inaweka masharti kwamba kabla ya Mjumbe wa Tume kuondolewa, Rais ataunda Tume ya Uchunguzi ambayo baada ya kumchunguza Mjumbe itatoa mapendekezo yake kwa Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya Katiba kuhusu ukomo wa kushika madaraka ama kwa kumaliza muda wake wa ujumbe au kuondolewa kwa kukiuka kanuni za maadili.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuondoa dhana kuwa nafasi ya ujumbe ni ya kudumu ili kutoa fursa kwa wananchi wengine. Pia, utaratibu wa kubadilisha Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kutasaidia kuleta mawazo mapya na mabadiliko ya kifikra na kimaendeleo katika nchi. Aidha, kuwepo kwa Kamati ya Uteuzi kutawezesha kupatikana kwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mchakato wa wazi kupitia utaratibu wa kupendekezwa au kuomba nafasi na kuchujwa.

**Ibara ya 193: Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi. Wajibu huo ni pamoja na kusimamia na kuendesha shughuli zote za

uchaguzi wa Wabunge na Rais katika Jamhuri ya Muungano; kusimamia na kuendesha kura ya maoni; kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika Jamhuri ya Muungano; na kugawa na kutangaza majimbo ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Ibara pia inaelezea kuwa Tume Huru ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri, maagizo au maoni ya mtu yoyote, mamlaka yoyote ya Serikali, chama cha siasa, Taasisi au asasi yoyote. Aidha, Ibara hii inapiga marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti kuhusu wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi na utekelezaji wa majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo ni kuongeza uadilifu katika usimamizi wa masuala ya uchaguzi na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake bila woga wala upendeleo. Pia kuiwezesha Tume Huru ya Uchaguzi kuwa na uwezo wa kusimamia na kuendesha shughuli zote za uchaguzi na kura ya maoni kwa uhuru, uadilifu, uwajibikaji na uwazi.

**Ibara ya 194: Malalamiko kuhusu Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi itakavyosimamia na kutatua migogoro inayohusu uchaguzi. Aidha, kesi za malalamiko dhidi ya matokeo ya Uchaguzi zitafunguliwa Mahakama Kuu mapema iwezekanavyo baada ya Tume Huru ya Uchaguzi kutangaza matokeo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya kufungua kesi za malalamiko kuhusu uchaguzi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa wananchi kuwasilisha malalamiko yao kuhusu uchaguzi na kutafutiwa ufumbuzi kwenye Tume au Mahakama ili haki ipatikane. Utaratibu huu pia unaupa uchaguzi uhalali kwa kuiwezesha Mahakama, pindi pakiwa na shaka, kuthibitisha matokeo ya uchaguzi baada ya kuridhika kuwa uchaguzi huo ulikuwa ni huru na haki.

***(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi***

**Ibara ya 195: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na hatimaye kuthibitishwa na Bunge. Pia, Ibara hii inaweka masharti ya sifa za mtu kuwa

Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuwa hajawahi kushika nafasi yoyote ya madaraka ya chama cha siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na sifa za kuteuliwa kwake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo wa Tume za Uchaguzi kuwa na Mkurugenzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu anayesimamia shughuli za kila siku.

**Ibara ya 196: Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi ambayo ni pamoja na kuwa msimamizi na mtekelezaji mkuu wa shughuli za kila siku za Tume Huru ya Uchaguzi kuhusiana na masuala ya uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa kura ya maoni.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya majukumu ya Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba wa kuanisha majukumu ya Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wake.

## SEHEMU YA TATU

## USAJILI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA SIASA

### *(a) Vyama vya Siasa*

### Ibara ya 197: Usajili wa Vyama vya Siasa

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kusajili vyama vya siasa. Aidha, Ibara hii inazuia mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote cha siasa au kwa chama cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa. Ibara hii pia inazuia kusajiliwa kwa chama cha siasa iwapo kinakusudia kukuza au kupigania maslahi ya imani au kundi lolote la dini, ukabila, ukanda na kutaka kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano. Pia inazuia kusajiliwa kwa chama kinachotaka kutumia nguvu au mapambano kufikia malengo ya kisiasa na kisichofanya uchaguzi wa mara kwa mara wa viongozi wake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba masharti na makatazo kuhusu usajili wa vyama vya siasa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua jukumu kubwa la vyama vya siasa na kujenga utashi wa kisiasa katika kutwaa uongozi wa nchi. Hivyo basi, ni muhimu visajiliwe kikatiba na kuhakikisha vina muelekeo na muonekano wa kitaifa vikisimamia na kulinda misingi ya kidemokrasia ya utawala wa nchi. Aidha, Ibara hii inampa Msajili wa Vyama vya Siasa nguvu za kikatiba kuweza kuendelea kufuatilia iwapo chama kinafuata makatazo yaliyotajwa katika sehemu hii ya Katiba.

### *(b) Msajili wa Vyama vya Siasa*

### Ibara ya 198: Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge. Pia, Ibara hii inaweka masharti na sifa za mtu kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kuweka utaratibu wa upatikanaji wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ni mlezi na msimamizi wa vyama vya siasa mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa vyama hivyo vinatii Katiba na kufuata misingi ya kidemokrasia katika uongozi wake na uhusiano wake kwa umma.

**Ibara ya 199: Wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa na wajibu huo ni pamoja na kusimamia na kuratibu uandikishaji na shughuli za vyama vya siasa, kutayarisha na kuchapisha taarifa za kila mwaka kuhusu ripoti za ukaguzi wa fedha kwa kila chama cha siasa na kusimamia fedha za kila chama cha siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kuwa Vyama vya siasa ni taasisi za wananchi wenye malengo yanayofanana. Hivyo basi ni lazima shughuli zake, ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha ambazo zinatokana na ruzuku ya Serikali, michango ya wanachama wao na wahisani na hivyo kupaswa kusimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa na umma kufahamishwa.

## SURA YA KUMI NA TATU

## TAASISI ZA UWAJIBIKAJI

### SEHEMU YA KWANZA

### TUME YA MAADILI YA UONGOZI NA UWAJIBIKAJI

**Ibara ya 200: Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji, na kuainisha sifa za mtu kuteuliwa na Rais kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Tume na kuthibitishwa na Bunge. Aidha, Ibara inafafanua kuwa uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utazingatia kuwa iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atatoka upande wa pili wa Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kuwa chombo cha kusimamia maadili ya uongozi na uwajibikaji wao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo hayo ni kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka kuwepo kwa chombo cha kikatiba kitakachokuwa na nguvu ya kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma. Hii ni kwa sababu walidai maadili ya viongozi wa umma yameshuka kwa kiwango kikubwa na hatua za uwajibishwaji hazichukuliwi inavyostahili kwa viongozi wanaovunja miiko na maadili.

Sababu nyingine ni kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi iliyopo haina uwezo na mamlaka ya kuchukua hatua zinazostahili kwa viongozi wanaovunja na kukiuka maadili.

Uzoefu unaonyesha kwamba utaratibu wa kuwa na Tume kama hii kikatiba upo katika nchi mbalimbali duniani. Kwa mfano, Katiba ya Ufilipino ya Mwaka 1987 iliweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma kama njia ya kuzuia rushwa na matumizi mabaya ya madaraka yaliyokuwa yamekithiri kwa takriban miongo miwili ya utawala wa Ferdinand Marcos ili kuwafanya viongozi waliokuwepo kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi.

Katiba ya Afrika Kusini ya mwaka 1994, iliweka misingi ya maadili na miiko ya viongozi iliyowafanya viongozi wa umma kuwajibika katika kuwatumikia wananchi waliokuwa na matumaini makubwa kwa Serikali kusaidia kuboresha maisha yao baada ya miongo kadhaa chini ya Serikali ya kibaguzi.

## Ibara ya 201: Uteuzi na Sifa za Wajumbe

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa uteuzi na sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji. Wajumbe wa Tume hii watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati ya Uteuzi.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba utaratibu na sifa za uteuzi wa mjumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimu wa kuwa na Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji wenye heshima na wanaoaminiwa na wananchi kutokana na dhamana kubwa waliyonayo ya kuwasimamia miiko na maadili ya viongozi wa umma.

## Ibara ya 202: Kamati Maalum ya Uteuzi

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Kamati ya Uteuzi ya Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji na kuainisha muundo wake. Wajumbe wa Kamati hii ni walewale wa Kamati ya Uteuzi ya Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi isipokuwa Mjumbe mmoja ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali anayeingia badala ya Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kuweka vyombo vya kikatiba vyenye mamlaka ya kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume mbalimbali zitakazoshughulikia masuala ya maadili ya Viongozi na watumishi wa Umma na uwajibikaji wao. Utaratibu huu utajenga imani kwa wananchi kwamba uwepo wa vyombo hivi kutaimarisha utendaji na uwajibika.

## Ibara ya 203: Majukumu ya Jumla ya Tume

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya jumla ya Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji ambayo ni kusimamia maadili na uwajibikaji katika utumishi wa umma, kuchunguza tabia na mwenendo wa mtumishi au kiongozi na kuchukua hatua pale inapostahili.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu ya jumla ya Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ambao walipendekeza kuundwa kwa chombo cha kikatiba chenye mamlaka na uwezo wa kusimamia na kuwawajibisha watumishi na viongozi wanaokiuka maadili na kuvunja miiko ya uongozi.

Sababu nyingine ni kuzingatia malalamiko ya wananchi kwamba maadili ya viongozi yameporomoka na uwajibikaji wao umeshuka. Hivyo wananchi wengi walipendekeza kurejeshwa kwa miiko ya uongozi iliyokuwemo katika Azimio la Arusha.

Pia, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi iliyopo sasa haina uwezo na mamlaka ya kuchukua hatua zinazostahili kwa Viongozi wanaovunja na kukiuka maadili.

**Ibara ya 204: Muda wa Kukaa Madarakani kwa Mjumbe wa Tume**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha muda wa kukaa katika madaraka kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji. Kipindi hicho ni miaka mitatu na mtu anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja zaidi cha miaka mitatu. Pia, Wajumbe watateuliwa kwa namna ambayo hawataanza na kumaliza muda wao wa uongozi kwa wakati mmoja.

Aidha, inaelekeza kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume hawatakuwa na sifa za kuteuliwa au kuchaguliwa kushika nafasi nyingine yoyote ya madaraka wakati watakapokuwa madarakani.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa kukaa katika madaraka kwa Wajumbe wa Tume na masharti ya utendaji wa kazi zao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji wanabadilishwa bila kuathiri utendaji wa Tume na kuwa na mwendelezo wa uhakika wa maamuzi na kuwapa uzoefu Wajumbe wapya.

**Ibara ya 205: Kuondolewa Madarakani kwa Mjumbe wa Tume**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kuwaondoa katika madaraka Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume kabla ya kumaliza muda wao wa uteuzi na sababu za kuondolewa kwao. Sababu hizo ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu kutokana na maradhi, kukiuka kanuni za maadili na miiko ya uongozi wa umma, kukosa weledi na utovu wa nidhamu.

Kabla ya kuondolewa wajumbe hao, Raisataunda Kamati Maalum ya Uchunguzi itakayotoa mapendekezo kwake kwa uamuzi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anapokosa sifa za kuendelea kushika nafasi hiyo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kumuondoa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume ambaye ameshindwa kutekeleza majukumu yake au amekosa sifa ili kulinda heshima ya Tume na imani ya wananchi. Hata hivyo, ni vyema kuwepo kwa Tume ya Uchunguzi ili kulinda haki za msingi za kusikilizwa kwa Wajumbe na Tume ya Uchunguzi na kuonyesha haki imetendeka na kuwalinda Wajumbe wasiondolewe kwa sababu za hila.

## Ibara ya 206: Uhuru wa Tume

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka msingi wa uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha kuwa haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ya kutaka Tume ifanye kazi zake kwa uhuru, uaminifu, uadilifu na bila woga au upendeleo.

Sababu nyingine ni kujenga imani kwa wananchi kuwa maamuzi yatakayofaywa na Tume hayatokani na maelekezo, shinikizo au matakwa ya mtu, kikundi cha watu au chombo chochote.

## Ibara ya 207: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara ya hii ya Rasimu ya Katiba inaweka wajibu kwa Serikali kuiwezesha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kwa kuipatia fedha, nyenzo na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka wajibu wa kikatiba kwa Serikali kuhakikisha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji inapatiwa nyenzo na rasilmali za kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikishia Tume ya Maadili upatikanaji wa fedha, nyenzo na rasilmali watu wa kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Hii pia itaepusha uwezekano wa Tume hii kunyimwa fedha, nyenzo na rasilmali watu inazozihitaji kwa lengo la kudhoofisha na kukwamisha shughuli zake ambazo ni pamoja na kuwachunguza na kuwachukulia hatua viongozi na watumishi wa umma.

## SEHEMU YA PILI

## TUME YA HAKI ZA BINADAMU

### Ibara ya 208: Tume ya Haki za Binadamu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Tume ya Haki za Binadamu na kuainisha muundo wake na utaratibu wa kuwateua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna. Ibara pia inaweka masharti kwa uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuthibitishwa na Bunge na kuzingatia msingi kwamba, iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti wake atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ili kuakisi taswira ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha kikatiba Tume ya Haki za Binadamu yenye dhamana ya kusimamia masuala ya haki za binadamu. Pia kujenga tabia na mazoea ya wananchi kutambua na kutetea haki zao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inayoanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka kuwepo kwa utaratibu utakaokuza, kuhifadhi na kulinda haki za binadamu. Aidha, mapendekezo ya Ibara hii ni kutilia nguvu utekelezaji wa mikataba au makubaliano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo.

Sababu nyingine za mapendekezo haya ni kuifanya Tume ya Haki za Binadamu iendelee kuwa chombo cha kikatiba na iwe na madaraka ya kufanya uchunguzi huru na taarifa zake ziwe wazi kwa umma. Aidha, Tume iwe na uwezo wa kutoa maelekezo badala ya kutoa ushauri kwa ofisa wa umma kama ilivyo sasa. Pia, Tume iwe na madaraka ya kufanya uchunguzi huru kwa mujibu kanuni za Paris.

### Ibara ya 209: Kamati ya Uteuzi

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu na kuainisha muundo na majukumu yake. Wajumbe wake ni sawa na wale wa Kamati ya Uteuzi wa Tume Huru ya Uchaguzi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Kuweka kikatiba Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutekeleza utaratibu na matakwa ya mikataba ya kimataifa kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu wapendekezwe na Kamati

Maalum ya Uteuzi. Utaratibu huu ndio uliomo katika Sheria ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora.

### Ibara ya 210: Kazi na Majukumu ya Tume

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kazi na majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu. Majukumu hayo ni pamoja na kuhamasisha hifadhi ya haki za binaadamu na wajibu kwa jamii, kupokea malalamiko na kuchunguza ukiukwaji na uvunjwaji wa haki za binadamu na kufungua mashauri Mahakamani. Aidha, ni pamoja na kuchunguza mwenendo wa mtu au taasisi yoyote inayoshukiwa au kutuhumiwa kuvunja haki za binadamu.

Ibara hii pia inaipa Tume mamlaka maalum ya kumuita mtu yeyote na kumtaka awasilishe nyaraka, kumbukumbu au taarifa anayoifahamu juu ya jambo linalochunguzwa na Tume.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu na mamlaka maalum ya Tume ya Haki za Binadamu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza majukumu ya Tume za Haki za Binadamu yaliyomo katika mikataba ya kimataifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001.

Sababu nyingine ni kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinapewa kipaumbele katika shughuli zote za serikali, vyombo vya umma na sekta binafsi.

### Ibara ya 211: Muda wa kukaa madarakani kwa Kamishna wa Tume

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka muda wa kukaa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na kuainisha ukomo wa kuteuliwa tena kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume. Aidha, inaweka masharti kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume hawatakuwa na sifa za kuteuliwa, kuchaguliwa au kushika nafasi nyingine yoyote ya madaraka wakati watakapokuwa madarakani.

Uteuzi wa Makamishna utafanywa kwa namna ambayo hawataanza au kumaliza muda wao kwa wakati mmoja.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa kukaa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume na masharti ya utendaji wa kazi zao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu wanapatikana wapya bila ya kuathiri utendaji na ufanisi wa Tume kwa kuwa na muendelezo wa uzoefu ndani ya Tume.

**Ibara ya 212: Kuondolewa Madarakani kwa Kamishna wa Tume**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu na sababu za kuwaondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume kabla ya kumaliza muda wao wa uteuzi. Ibara inaeleza kuwa kabla ya kumuondoa Kamishna, Rais ataunda Kamati Maalum ya Uchunguzi itakayomshauri kuhusu hatua za kuchukua.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anapokosa sifa za kuendelea kushika nafasi hiyo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka misingi madhubuti ya kikatiba ambayo kwa utekelezaji wake itawahakikishia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume kufanya kazi zao kwa uaminifu, uadilifu, bila upendeleo na kufanya maamuzi sahihi bila woga wa kuondolewa kwenye Tume kwa hila. Aidha, utaratibu huu unaweka mashart ya kuwaondoa kwa misingi ya haki wanaposhindwa kufanya kazi au kukiuka kanuni za maadili na miiko ya uongozi. Hatua hii italinda heshima ya Tume na Makamishna wake.

**Ibara ya 213: Uhuru wa Tume**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha kuwa haiingiliwi na mtu au mamlaka yoyote katika hatua zote za utekelezaji wa majukumu yake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kubainisha kikatiba uwepo wa uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuifanya Tume ifanye kazi zake kwa uhuru na kuwawezesha Makamishna watekeleze majukumu yao kwa uaminifu, uadilifu na bila ya woga wa upendeleo.

Aidha, mapendekezo haya yanajenga imani kwa wananchi kuwa maamuzi yatakayofaywa na Tume hayatokani na maelekezo, shinikizo au matakwa ya mtu, kikundi cha watu au chombo chochote.

Pia, kuwepo kwa uhuru wa Tume, kutaiwezesha Tume kufanya kazi zake kwa ufanisi na matokeo yake masuala ya Haki za Binadamu yataimarika.

**Ibara ya 214: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka wajibu kwa Serikali kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu kwa kuipatia fedha, nyezo na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba wajibu wa Serikali wa kuhakikisha kuwa Tume ya Haki za Binadamu inapatiwa fedha, nyenzo na rasilmali watu ya kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuifanya Tume kuwa na uhakika wa kupata fedha, nyenzo na rasilmali watu ya kutosha kutimiza wajibu wake kwa ufanisi mkubwa. Hii pia kutaifanya Tume kutokwamishwa kwa makusudi katika shughuli zake ambazo ni pamoja na kuwachunguza viongozi na watumishi wa umma ambao wamekiuka au kuvunja haki za binadamu katika utekelezaji wa kazi na majukumu yao. Sababu nyingine ni kuhakikisha kwamba shughuli za Tume zinapewa kipaumbele stahiki katika bajeti ya Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

### Ibara ya 215: Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na utaratibu wa uteuzi wake na kuelekeza kuwa kabla ya kushika madaraka atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuweka kikatiba utaratibu wa uteuzi wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kumlinda Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kikatiba na kuendeleza utaratibu unaotumika nchi nyingi duniani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Sababu nyingine ni kuhakikisha kuwa hesabu na matumizi ya Serikali yanasimamiwa na kudhibitiwa na chombo ambacho kimepewa dhamana kikatiba.

### Ibara ya 216: Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu na sifa za mtu anayepaswa kuteuliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sifa hizo ni pamoja na kuwa amefuzu mafunzo juu ya uhasibu na kusajiliwa na mamlaka husika na ana uzoefu usiopungua miaka kumi katika masuala yanayohusu ukaguzi wa hesabu za Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka kikatiba sifa na utaratibu wa uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mtu mwenye sifa za kitaaluma, weledi, uzoefu wa kutosha na pia mwenye maadili. Ofisi hii ni muhimu sana katika usimamizi wa matumizi ya Serikali na ina wajibu wa kuzuia na kuchukua hatua dhidi ya ubadhirifu, ufujaji na wizi wa fedha na rasilmali za Serikali.

## Ibara ya 217: Kazi na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kazi na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na uhuru katika kutekeleza majukumu yake. Majukumu hayo ni pamoja na kuhakikisha fedha zilizokusudiwa kutolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina zinatumika kwa matumizi yalioidhinishwa na yamefuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo.

Aidha, Ibara inamwelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka na kutoa taarifa kuhusu hesabu za serikali, taasisi na wakala wa Serikali, Mahakama na Bunge.

### b. Madhumuni na Lengo

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba kazi, majukumu na uhuru wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kikatiba wadhifa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ni nafasi muhimu sana katika utendaji wa Serikali.

Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kumlinda Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kumpa uhuru ili atekeleze majukumu yake bila hofu wala woga wa kuchukuliwa hatua na watu, taasisi anazozikagua na kuzichukulia hatua. Kujenga nidhamu ya kifedha katika matumizi ya Serikali.

## Ibara ya 218: Muda wa Kukaa Madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

### a. Maudhui ya Ibara

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka ukomo wa kukaa madaraka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Ibara inaainisha utaratibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiuzulu nafasi yake.

### b. Madhumuni na Lengo

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaa madarakani ambao ni kipindi kimoja cha miaka saba mfulululizo.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu za mapendekezo haya ni kumlinda kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili afanye kazi yake kwa uhuru akiwa na uhakika wa ajira yake. Utaratibu huu ndio unaotumika katika nchi nyingi duniani wa kumpa Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kipindi kimoja cha muda maalum ili kuepuka athari za kuzoea na kuzoeleka na anaowakagua.

**Ibara ya 219: Kuondolewa Madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu na vigezo vya kumuondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya kumaliza muda wake na kuainisha sababu za kumuondoa. Aidha, sababu hizo ni pamoja na kushindwa kutekeleza majukumu kwa maradhi, kukiuka kanuni za maadili na miiko ya uongozi, kukosa uweledi na utovu wa nidhamu.

Ibara inaelekeza pia kabla ya Rais kumuondoa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali madarakani, ataunda Kamati Maalum ya Uchunguzi yenye Mwenyekiti na angalau wajumbe wengine wawili ambao nusu yao watakuwa ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba na sababu za kumuondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya kumaliza muda wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimu wa nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hivyo kutakiwa alindwe na asiondolewe madarakani isipokuwa kwa utaratibu maalum wa kikatiba. Hatua hii inalinda hadhi na heshima ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi yake.

**Ibara ya 220: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka wajibu kwa Serikali wa kuhakikisha kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapata fedha, nyenzo na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka kwenye Katiba wajibu wa Serikali wa kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili itekeleze kwa wakati na ufanisi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kumhakikishia kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata fedha, nyenzo na rasilmali watu wa kutosha ili kuweza kusimamia matumizi ya bajeti ya Serikali. Wajibu huu ni muhimu na nyeti na hivyo

utaratibu huu utaepusha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukwamishwa kwa makusudi na kumfanya ashindwe kutimiza majukumu yake.

## SURA YA KUMI NA NNE

## MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

### *(a) Mfuko Mkuu wa Hazina na Fedha za Jamhuri ya Muungano*

**Ibara ya 221: Mfuko Mkuu wa Hazina**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya kuanzishwa kwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali zitawekwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Mfuko Mkuu wa Hazina wa Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuwa na chombo kimoja kikuu cha kutunza fedha zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha mapendekezo haya ni kuondoa dhana kwa Wizara na Idara zinazokusanya kodi na maduhuli kudhani kwamba fedha hizo ni zao ila ni za umma na hapana budi kuwasilisha mapato hayo Hazina na kama kugaiwa basi mgao hufanyika kwa maelekezo ya Bunge.

**Ibara ya 222: Masharti ya Kutoa Fedha za Matumizi Katika Mfuko Mkuu wa Hazina**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti na utaratibu wa kutoa fedha katika mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi. Aidha, ibara inaelekeza kuwa fedha hizo zinaweza kutolewa kwa ajili ya matumizi kwa kuzingatia masharti yaliyotolewa na Bunge kwa Serikali wakati wa Bajeti kwa mujibu wa Katiba hii na sheria ya matumizi ya serikali au sheria nyingine ya Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na kuhakikisha kuwa hazitolewi kinyume cha Katiba na sheria zilizotungwa na Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa utoaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Aidha mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa fedha hii ambayo ni mali ya wananchi haitumiki bila ya utaratibu uliowekwa ili kuepuka ubadhirifu, ufujaji na wizi wa mapato ya fedha za Serikali.

### Ibara ya 223: Utaratibu wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Zilizomo Katika Mfuko Mkuu wa Hazina

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ambapo Rais atatoa maagizo kwa wahusika kutayarisha na kuwasilisha kwenye Bunge, katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, Ibara hii inaweka masharti kuhusu Bunge kuidhinisha matumizi ya Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuidhinisha fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi yaliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu mzuri wa kupanga makadirio na matumizi ya fedha kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuweka wazi matumizi ya Serikali. Aidha, ni kulipa Bunge mamlaka ya kutoa idhini ya matumizi ya fedha kwa mipango iliyowasilishwa Bungeni na Serikali na kuridhiwa na Bunge kwa kuzingatia maslahi ya taifa na ustawi wa wananchi. Mapendekezo haya yatahakikisha kuwepo kwa uwiano kati ya mapato na matumizi ya Serikali.

### Ibara ya 224: Utaratibu wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha Kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali Kuanza Kutumika

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuanza kutumika kwa kutoa madaraka kwa Rais kuidhinisha fedha kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kugharamia matumizi ya lazima ya Serikali. Aidha, Ibara hii inafafanua kuwa fedha hizo zitumike ndani ya miezi minne tangu mwanzo wa mwaka wa fedha wa Serikali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuidhinisha matumizi ya fedha za Serikali kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa shughuli za Serikali za lazima hazikwami wakati wa kipindi ambacho mwaka wa Bajeti umekwisha na sheria ya kuruhusu matumizi ya Serikali haijapitishwa.

**Ibara ya 225: Mfuko wa Matumizi ya Dharura**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kuweka masharti ya matumizi ya fedha hizo. Aidha, Ibara inaelekeza kuwa fedha hizo zitatumika tu kwa jambo la haraka la dharura ambalo halikutazamiwa kutokea na ambalo halikupangiwa fedha. Fedha hizo zitakazotolewa zitapaswa kurejeshwa katika Mfuko wa Matumizi ya Dharura baada ya Bunge kupitisha sheria ya matumizi ya nyongeza.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kuweka masharti ya matumizi ya fedha kutoka katika mfuko huo. Aidha, ni kuipa Serikali uwezo wa kukabiliana na changamoto za dharura na majanga.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kulipa taifa uwezo wa kukabiliana na dharura zinapotokea bila ya kusubiri Bunge kuidhinisha fedha za matumizi hayo yanayohitajika haraka. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuifanya nchi kujitegemea kwa kuwa na uwezo wa kuchukua hatua za haraka kukabili changamoto za dharura.

**Ibara ya 226: Mishahara ya Baadhi ya Watumishi Kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaohusika kulipwa mishahara na posho kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia sheria husika. Malipo hayo pia yanajumuisha fedha za malipo ya uzeeni na kiinua mgongo. Pia, Ibara inaelekeza kuwa masharti hayo yanawahusu Majaji, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Tume mbalimbali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watumishi wengine watakaoainishwa katika sheria za nchi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kusimamia mishahara, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kwa viongozi na watumishi wa umma walioainishwa katika Katiba na sheria za nchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya mishahara, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali. Mapendekezo haya ni kuwapa watumishi husika uhakika wa mapato na matunzo yao baada ya kustaafu au kuacha kazi, lakini pia kuepusha watumishi hao kujilipa mishahara na mafao nje ya utaratibu uliowekwa.

### *(b) Deni la Taifa na Mikopo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano*

**Ibara ya 227: Deni la Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaelekeza kwamba Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina. Aidha, Ibara inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kudhaminiwa Deni la Taifa. Pia, Ibara hii inafafanua kuwa Deni la Taifa ni pamoja na Deni la Serikali ya Jamhuri ya Muungano na deni lolote litakalodhaminiwa na Serikali ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka chombo cha kudhamini Deni la Taifa ambacho ni Mfuko Mkuu wa Hazina.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya Mapendekezo haya ni kutambua kuwa Mfuko Mkuu wa Hazina ndio unaotunza mapato yote ya Serikali ikiwa ni pamoja na mali na madeni ya taifa. Aidha, ni kuendeleza utaratibu huu wa kikatiba unaotumika katika sehemu mbalimbali duniani ambapo Serikali inapokopa, Mfuko Mkuu wa Hazina ndio unaochukua dhamana.

**Ibara ya 228: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Kukopa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kugharamia shughuli zilizo chini ya mamlaka yake. Aidha, inapendekezwa kwamba Serikali iwajibike kutoa taarifa Bungeni kuhusu mikopo kwa kuainisha kiasi cha deni lililopo, riba yake, matumizii ya fedha za mikopo na utaratibu wa kulipa madeni ya Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuipa mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa fedha ndani na nje ya nchi na pia kulipa Bunge uwezo kuweka ukomo wa deni la taifa na madhumuni ya deni.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kudhibiti Deni la Taifa ili lisivuke uwezo wa taifa kulipa. Aidha, ni kuhakikisha kuwa mikopo inayochukuliwa ina tija na manufaa kwa maendeleo ya wananchi na kuwa imezingatia misingi ya utawala bora na uwajibikaji. Pia, kutoa taarifa ya madeni Bungeni na kukuza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi. Sababu nyingine ni kuepusha kulimbikiza madeni yasiyo na tija na kuwa mzigo kwa vizazi vijavyo.

**Ibara ya 229: Mamlaka ya Serikali za Nchi Washirika Kukopa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mamlaka ya serikali za Nchi Washirika kukopa. Ibara inaelekeza kuwa Nchi Washirika watakuwa na mamlaka ya kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kugharamia mambo yaliyo chini ya mamlaka zao. Aidha, Ibara hii inaweka masharti kuhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuweza kuchukua dhamana za mikopo iwapo itatakiwa kufanya hivyo na Serikali za Nchi Washirika. Dhamana hiyo itatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano baada ya kushauriana na kukubaliana na Nchi Mshirika itakayokuwa inahitaji mkopo huo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutoa dhamana kwa mikopo ya Nchi Washirika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa Nchi Washirika kukopa ndani na nje ya nchi kwa kudhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kulingana na aina na ukubwa wa mikopo. Aidha, mapendekezo haya ni utaratibu wa kushauriana na kukubaliana baina ya Serkali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Nchi Mshirika kuhusiana na dhamana kwa ajili ya mikopo ya aina hiyo.

Sababu nyingine ni kuondoa vikwazo kwa Nchi Washirika kupata fursa ya kukopa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya nchi zao.

**Ibara ya 230: Masharti ya Kutoza Kodi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kutoza kodi na kwamba hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa na mamlaka ya Serikali ya Muungano isipokuwa kwa mujibu wa Sheria.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya utaratibu wa kutoza kodi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kulipa Bunge pekee uwezo na mamlaka ya kutunga sheria za kutoza kodi.

**Ibara ya 231: Vyanzo vya Mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha vyanzo vya mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwa ni ushuru wa bidhaa, mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na

taasisi za Muungano, mchango kutoka kwa Nchi Washirika, mikopo kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano na mapato mengine.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake bila ya vikwazo vya kifedha, kuondoa mgongano wa vyanzo vya mapato vya Muungano na visivyo vya Muungano; na kutoa uhalali wa ukusanyaji wa kodi na upatikanaji wa mapato kutokana na vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika Katiba.

Mapendekezo ya vyanzo hivi vya mapato yamezingatia mapato na matumizi ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya Muungano kama yalivyochanganuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC), Taarifa za Makusanyo ya Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na bajeti za kila mwaka zinazopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Taarifa hizo za kitaalamu zinaonesha kwamba mapato yanayotokana na vyanzo hivi yanatosheleza kuendesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutokana na uchache wa Mambo ya Muungano yanayopendekezwa na Rasimu hii kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**Ibara ya 232: Ununuzi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu Ununuzi wa Umma ambao utafanywa na Serikali na Taasisi zake kwa kutumia mfumo na utaratibu utakaozingatia haki, uwazi, maslahi ya umma, uwajibikaji, ushindani na thamani halisi ya fedha.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya mfumo na utaratibu wa kufanya ununuzi wa umma.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kusimamia na kudhibiti manunuzi ya umma katika Serikali na taasisi zake. Aidha mapendekezo haya yametokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali na Taasisi zake inatumika katika ununuzi wa bidhaa au huduma kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika vyema na kwa thamani halisi ya fedha.

## *(d)Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano*

### Ibara ya 233: Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano itakayokuwa na majukumu ya moja kwa moja ya: kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu, kuandaa na kusimamia sera na mipango inayohusiana na sarafu; na kudhibiti na kusimamia masuala ya fedha za kigeni. Aidha, Benki Kuu itakuwa huru na haitaingiliwa, kupewa maelekezo au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote wakati wa kutekeleza majukumu yake. Aidha Ibara inaelekeza kuwa Benki hii pia itakuwa na jukumu la kuzisimamia benki za Nchi Washirika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika nchi nyingi duniani wa kuwa na Benki Kuu moja inayozisimamia na kuzielekeza benki za Nchi Washirika.

Pia, sababu nyingine ni kuweka usimamizi na udhibiti wa sarafu na fedha zote za Jamhuri ya Muungano chini ya Benki Kuu kwa vile utaratibu huu ndiyo unaotumika katika nchi za shirikisho au zilizomo katika umoja wa sarafu ya pamoja (*Monetary Union*) kama vile Nigeria, Umoja wa Nchi za Marekani (*United States of America*) na Ujerumani. Pendekezo hili pia limezingatiwa kwa sababu Tanzania ni nchi yenye Sarafu moja.

### Ibara ya 234: Benki za Serikali za Nchi Washirika

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba masharti ya kuziwezesha Nchi Washirika kuwa na benki zao zitakazokuwa na jukumu la kutunza akaunti ya fedha za Serikali zao, kusimamia sera za kifedha na benki za biashara katika mamlaka zao chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya kuanzishwa kwa benki za Serikali za Nchi Washirika na usimamizi wake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katika muundo wa Muungano wenye Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano na Serikali zaidi ya moja ya kusimamia mambo hayo, huhitajika kuwepo kwa Benki za Serikali hizo zaidi ya Benki Kuu. Hivyo, Katiba huainisha na kutofautisha

majukumu ya Benki Kuu na kazi na majukumu ya Benki za Nchi Washirika ili kuepusha migongano na kuyumbisha uchumi na thamani ya fedha.

## SURA YA KUMI NA TANO

## ULINZI NA USALAMA WA JAMHURI YA MUUNGANO

### *(a) Ulinzi na Usalama wa Taifa*

**Ibara ya 235: Usalama wa Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatamka kuwa jukumu la ulinzi na usalama wa taifa ni la kila raia. Aidha, inafafanua kwamba ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano unahusu mipaka ya eneo lote la Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na ardhi, anga, bahari kuu, watu, mali, haki, uhuru na maslahi mengine. Pia, Ibara hii inaweka kanuni zinazosimamia ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na kuongozwa kwa mujibu wa Katiba, kusimamia sheria za nchi, kuheshimu utawala wa sheria, haki za binadamu na tamaduni za jamii mbalimbali.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba jukumu la ulinzi na usalama kuwa ni la kila raia wa Jamhuri ya Muungano.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza mfumo na utaratibu wa ulinzi na usalama uliopo Tanzania ambao chimbuko na hatma yake ni wananchi wenyewe. Kanuni zilizowekwa zinazingatia kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vipo kwa ajili ya wananchi na kwa hiyo ni sehemu ya jamii ya Tanzania. Pia, ni kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano, raia wake pamoja na mali zao zinakuwa salama kwa kuzingatia sheria za nchi na sheria za kimataifa na kwa kuheshimu kikamilifu utawala wa sheria na Haki za Binadamu.

**Ibara ya 236: Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha vyombo vya ulinzi na Usalama wa Taifa ndani ya Jamhuri wa Muungano kuwa ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano na Idara ya Usalama wa Taifa. Aidha, Ibara hii inaweka masharti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na maadili yake. Maadili hayo yanawakataza watumishi wa vyombo vya usalama kuwa na upendeleo wa aina yoyote, kujihusisha na chama cha siasa na sera zake, kutishia, kudhulumu na kuwatendea ukatili raia na watu wengine.

Pia, Ibara hii imetoa uwezo kwa Rais kuunda chombo cha ulinzi kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa ikitokezea haja ya kufanya hivyo.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni kuunda kikatiba vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa katika Jamhuri ya Muungano. Madhumuni mengine ni kumpa Rais mamlaka ya kuunda chombo cha ulinzi na usalama, mamlaka na usimamizi wake, majukumu na wajibu katika ulinzi wa usalama wa nchi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo hayo ni kutambua kuwa vyombo vya ulinzi na usalama ndio moyo wa nchi na alama inayoonekana ya uhuru na mamlaka ya nchi, hivyo, ni vyema vyombo hivyo vikaanzishwa na kikatiba na kuwa chini ya amri moja ya Rais ambaye ni Mkuu wa Nchi kwa nafasi yake ya Amiri Jeshi Mkuu.

**Ibara ya 237: Kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa ambalo litakuwa ndio chombo cha juu cha usimamizi wa masuala yote ya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano pamoja na Nchi Washirika wa Muungano. Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Ulinzi na Usalama na wajumbe wengine wa Baraza hilo ni Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika, Rais wa Zanzibar, Waziri mwenye dhamana ya Ulinzi, Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Nje, Waziri mwenye dhamana ya Usalama wa Taifa, Waziri mwenye dhamana ya Fedha, Mwanasheia Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Mkuu wa Jeshi la Polisi la Jamhhuri ya Muungano wa Tanzania na Kamishna Mkuu wa Uhamiaji.

Pia, Ibara hii inaainisha Sekretarieti ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa ambalo litaongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibra hii ni kuanzisha kikatiba Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa la kumshauri Amiri Jeshi Mkuu juu ya masuala ya Ulinzi na Usalama kikiwa ni chombo muhimu kwa uhai na usalama wa Taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kulitambua kikatiba na kuendeleza utaratibu wa sasa wa kuwa na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa. Baraza hili ni muhimu kwa mashauriano ya ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikijumuisha Nchi Washirika kwa kuwa Ulinzi na Usalama ni suala la Muungano. Aidha, chombo hiki kinamkutanisha Rais wa Jamhuri ya Muungano na Viongozi wa Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar kujadili na kuamua juu ya mambo makubwa ya mustakabali wa Taifa la Tanzania.

### Ibara ya 238: Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha majukumu ya msingi ya Baraza hili ambayo ni pamoja na kuunganisha sera za ndani, sera za mambo ya nje na zile za kijeshi kuhusiana na usalama wa Taifa. Aidha ni kuanzisha sera kuhusu masuala ya maslahi ya pamoja ya usalama na kudhibiti taasisi za kiusalama za Nchi Washirika. Pia, Rais atatoa taarifa kwenye Bunge kila mwaka kuhusu hali ya ulinzi na usalama katika Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuanzisha chombo cha kikatiba cha kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano akiwa Amiri Jeshi Mkuu kumuwezesha kuamua juu ya mambo makubwa na mustakabali wa Taifa la Tanzania. Vilevile, kuwezesha na kurahisisha uratibu wa masuala ya usalama katika Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika.

## *(b) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania*

### Ibara ya 239: Kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litakalokuwa na jukumu la kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri wa Muungano na kusimamia ulinzi na usalama. Aidha, Ibara hii inampa uwezo Rais wa Jamhuri ya Muungano akiwa Amiri Jeshi Mkuu kuanzisha vikosi vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Jeshi moja la ulinzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kwamba ulinzi wa nchi ni suala la mamlaka ya Juu ya Nchi na haligawiki hata katika nchi za Shirikisho au Muungano. Kwa hiyo, Ibara hii inahakikisha kuwepo kwa chombo kimoja cha ulinzi ambacho ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambalo litasimamia masuala yote ya Ulinzi na Usalama wa wananchi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano.

**Ibara ya 240: Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu inaanzisha kikatiba nafasi ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii kuanzisha kikatiba nafasi ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo wa Jeshi la Ulinzi kuongozwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi anayeteuliwa na Amiri Jeshi Mkuu. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa wazi wa kikatiba wa kumpata Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia Majeshi ya Ulinzi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau wa masuala ya ulinzi na usalama na wananchi kwa ujumla waliopendekeza kuwa na utaratibu wa Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

**Ibara ya 241: Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha masharti ya kikatiba kuhusu Rais kwa nafasi ya madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu kuwa na mamlaka ya kuyaamuru majeshi ya nchi kutenda mambo yanayohusika na vita vya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano; kuokoa maisha na mali za watu katika hali ya hatari; kusaidia na kushirikiana na mamlaka nyingine wakati wa dharura au maafa; kusaidia mamlaka au uongozi wa Serikali kutuliza ghasia, fujo au kurejesha hali ya utulivu; kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika ulinzi wa amani pale itakapoonekana inafaa; na kutenda mambo mengineyo ambayo Amiri Jeshi Mkuu ataona inahitajika.

Pia, Ibara hii inampa madaraka Amiri Jeshi Mkuu kuwateua viongozi katika majeshi ya ulinzi ya Jamhuri ya Muungano; kuwateua wanajeshi watakaoongoza vikosi mbalimbali vya majeshi ya ulinzi; kumwamuru mwanajeshi yeyote asitumie madaraka yoyote aliyokabidhiwa na ambayo yanaambatana na kuwa kwake mwanajeshi; na kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri ya Muungano.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua mamlaka ya kipekee ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana ya mwisho ya maamuzi juu ya ulinzi na usalama wa nchi. Sababu nyingine ni kumpa uwezo wa kikatiba wa kuyaamuru na

kuyapeleka majeshi vitani baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na kadri itakavyojitokeza kupata idhini ya Bunge.

Kwa hiyo, ni vyema Katiba ikaainisha kwa ufasaha madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu na udhibiti wake.

**Ibara ya 242: Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba Tume ya Utumishi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia masuala yote ya utumishi wa Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vyake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka chombo cha kikatiba cha kusimamia masuala yote ya utumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vyake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau kwamba pawepo chombo cha kikatiba cha kusimamia masharti ya utumishi na maslahi ya wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vyake. Hii itakuwa ni mara ya kwanza kuwa na chombo kama hiki katika Katiba ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

***(c)Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano***

**Ibara ya 243: Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano lenye jukumu la ulinzi na usalama wa watu na mali zao.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano la Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya Wananchi waliotaka kuwepo kwa Jeshi moja la Polisi litakalosimamia usalama wa raia wote katika Jamhuri ya Muungano ikijumuisha Nchi Washirika.

**Ibara ya 244: Misingi ya Utendaji wa Jeshi la Polisi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha misingi itakayozingatiwa na Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yake. Misingi hiyo ni pamoja na viwango vya juu vya

kitaaluma na nidhamu miongoni mwa wafanyakazi wake; ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu; kanuni za uwazi na uwajibikaji;na kukuza mahusiano na jamii. Aidha, Ibara hii inaainisha namna Jeshi la Polisi litakavyoshirikiana na vyombo vinavyohusika katika kupambana na uhalifu ndani ya Nchi Washirika katika kufanya uchunguzi na kushughulikia makosa ya rushwa na ufisadi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba misingi itakayoongoza utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi kwa ufanisi.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya kutambua dhamana kubwa ya Jeshi la Polisi la kulinda usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo, pamoja na kuwa ni chombo cha nguvu cha kidola bado kinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba, sheria na kanuni zinazokuza na kuimarisha utawala wa sheria na haki za binadamu. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu utakaolifanya Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya kitaaluma, nidhamu, kulinda haki za binadamu, kanuni za uwazi na uwajibikajii na kukuza mahusiano ya kijamii.

**Ibara ya 245: Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba nafasi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau waliotaka Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia usalama wa raia na mali zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ibara ya 246: Uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inampa uhuru Mkuu wa Jeshi la Polisi wa kutekeleza kazi zake bila woga, upendeleo au chuki.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara  ni kuweka kikatiba uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi anafanya kazi yake kwa uhuru kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na kanuni zilizowekwa bila ya kushinikizwa au kuingiliwa na mtu au mamlaka nyingine yoyote.

**Ibara ya 247: Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi kikatiba. Tume hiyo itakuwa na jukumu la kusimamia masuala yote ya utumishi ya askari wa Jeshi la polisi.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi ikiwa ni chombo cha kusimamia masuala yote ya utumishi wa askari wa Jeshi la Polisi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau kwamba pawepo chombo cha kikatiba cha kusimamia masharti ya utumishi na maslahi ya watumishi wa Jeshi la Polisi. Hii itakuwa ni mara ya kwanza kuwa na chombo kama hiki katika Katiba ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***(d) Idara ya Usalama wa Taifa ya Jamhuri ya Muungano***

**Ibara ya 248: Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba idara ya Usalama wa Taifa itakayohusika na shughuli za kuimarisha usalama wa Jamhurii ya Muungano na kulinda Katiba, maslahi ya taifa na ya watu wake.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Idara ya Usalama wa Taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ya ibara hii ni kuanzisha kikatiba chombo kitakachokuwa na dhamana ya kuhakikisha usalama wa taifa na watu wake dhidi ya mataifa ya nje na maeneo ya kimkakati na kiusalama ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kuilinda Katiba ya Nchi.

**Ibara ya 249: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaanzisha kikatiba nafasi ya Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau waliotaka Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia usalama wa taifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ibara ya 250: Usalama katika Nchi Washirika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mamlaka ya Wakuu wa Nchi Washirika kuweza kutoa maagizo kwa kiongozi yoyote wa Jeshi la Polisi au Idara ya Usalama wa Taifa kuchukua hatua yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinda au kuimarisha usalama wa eneo lolote la Nchi Washirika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba yanayowawezesha Wakuu wa Serikali wa Nchi Washirika kuwaagiza viongozi wa Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa kuchukua hatua kwa ajili ya kulinda na kuimarisha usalama katika eneo lolote la Nchi Mshirika husika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimuu na mamlaka ya Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa kwamba hayagawiki lakini pia kutambua umuhimu wa nchi washirika kuwa na uwezo wa kuvitumia vyombo hivi; na hivyo kupewa

mamlaka ya kuwaagiza wakuu au maafisa wengine iwapo kuna haja ya kukabili hali ya kiusalama.

## SURA YA KUMI NA SITA

## MENGINEYO

### Ibara ya 251: Utaratibu wa kujiuzulu Katika Utumishi wa Umma

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya utaratibu wa mtumishi yeyote wa umma kujiuzulu katika Utumishi wa Umma kwa kutoa taarifa iliyoandikwa kwa mkono wake. Aidha, ibara inaainisha mamlaka inayohusika kuarifiwa juu ya kujiuzulu huko kwa kuelekeza kuwa Rais akijiuzilu atatoa taarifa kwa Spika, Makamu wa Rais akijiuzulu atatoa taarifa kwa Rais, Spika, Naibu Spika na Mbunge wakijiuzulu watatoa taarifa kwa Bunge.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kujiuzulu katika utumishi wa umma na Mamlaka ya kuarifiwa juu ya uamuzi huo.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuheshimu kanuni za utawala wa sheria; na kanuni za utumishi kwa kuwa na utaratibu unaoruhusu mtumishi kujiuzulu kwa hiyari yake au kwa kutekeleza maelekezo au maamuzi ya mamlaka za nchi kwa mujibu wa Katiba.

### Ibara ya 252: Masharti Kuhusu Kukabidhi Madaraka

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti ya utaratibu wa kukabidhi madaraka katika utumishi wa umma kwa kutoa uwezo wa kuteua kaimu au mtu ambaye atashika kwa muda na kutekeleza madaraka husika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kukabidhi madaraka katika Utumishi wa Umma.

**c. Sababu za mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Utumishi wa Umma wa kuhakikisha kuwa wakati wote kuna mtu anayeshikilia nafasi ya utumishi ili kuepusha ombwe na kukosekana kwa huduma au maamuzi kwa wananchi. Aidha, mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kukabidhi ofisi unaolingana na Utumishi wa Umma.

**Ibara ya 253: Baadhi ya Watumishi wa Umma Kutoshika Madaraka**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu watumishi wa umma ambao hawatakuwa na haki ya kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa katika nafasi ya kisiasa hadi utakapopita muda wa miaka mitatu tokea kuacha au kustaafu nafasi ya madaraka aliyokuwa akiishikilia. Ibara inaainisha watumishi hao ni Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahakama ya Juu wa Jamhuri ya Muungano; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Jaji wa Mahakama ya Rufani; Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji; Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma; na Msajili wa Vyama vya Siasa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba, kuzuia baadhi ya viongozi wastaafu kushiriki kwenye siasa kwa kipindi cha miaka mitatu tangu walipostaafu au kuachia madaraka.

**c. Sababu za mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuondoa mgongano wa kisiasa katika utendaji wa Serikali na kuepusha uwezekano wa mtu kuchukua maamuzi muda mfupi kabla ya

kuacha uongozi au kustaafu kwa lengo la kumsaidia kugombea au kupata cheo cha kisiasa baada ya hapo.

**Ibara ya 254: Ufafanuzi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika katika Katiba ili kuyapa maana ya matumizi yake ndani ya Katiba.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maneno na istilahi za kikatiba zilizotumika ndani ya Katiba.

**c. Sababu za mapendekezo**

Sababu ni kuendeleza utaratibu wa kutafsiri istilahi za kitaalam katika utungaji wa Katiba. Pia ni kawaida duniani kote wa kuwa na Ibara ya aina hii katika Katiba.

**Ibara ya 255: Jina la Katiba na Kuanza Kutumika**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inataja jina la Katiba ambalo ni "Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014" na muda wa kuanza kutumika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara ni kubainisha jina na muda wa kutumika kwa Katiba husika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kitaalam wa kuhakikisha kuwa jina la Katiba ya Nchi linatamkwa bayana ndani ya Katiba na tarehe ya kuanza kwake.

**Ibara ya 256: Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya 2**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kufuta rasmi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na kuweka Masharti ya Mpito na Masharti ya Muda.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba wa Katiba Mpya kufuta Katiba iliyopo ili kuondoa uwepo au mgongano wa matumizi ya katiba mbili kwa wakati mmoja.

## SURA YA KUMI NA SABA

## MASHARTI YATOKANAYO NA MASHARTI YA MPITO

### SEHEMU YA KWANZA

### MASHARTI YATOKANAYO

**Ibara ya 257: Matumizi ya Baadhi ya Masharti ya Katiba, Sura ya 2**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha muda wa kuanza kutumika kwa masharti yatokanayo na masharti ya mpito yaliyotajwa katika Rasimu. Aidha, Ibara hii inafafanua kuwa Katiba ya mwaka 1977 itakoma baada ya Katiba mpya kuanza kutumika.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu matumizi ya masharti ya kipindi cha mpito na ukomo wa Katiba ya mwaka 1977.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Mhimili wa Mahakama unaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki kwa wananchi katika kipindi chote cha mpito na baada ya hapo.

Sababu nyingine ni kuzuia kukata rufaa kwenye Mahakama ya Juu kwa mashauri yaliyotolewa uamuzi katika Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ni kuondoa mgongano wa utekelezaji wa kazi za Makahama katika kipindi cha mpito.

### SEHEMU YA PILI

### MASHARTI YA KIKATIBA NA SHERIA ZA NCHI

**Ibara ya 258: Kuendelea Kutumika Masharti ya Katiba**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha kuendelea kutumika kwa Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito kama yalivyoorodheshwa katika Rasimu. Pia, Ibara inatambua Sheria maalum zifuatazo kwamba zitaendelea kutumika chini ya Katiba ambazo ni "Sheria Maalum" maana yake ni "the Republic of Tanganyika (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1962, the Interim Constitution (Consequential, Transition and Temporary Provisions) Act, 1965, the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1977, the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1984 na "the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1992".

**b. Madhumuni na Lengo**

Madhumuni ya Ibara hii ni Kutambua kikatiba Sheria na maamuzi yaliyofanywa katika katiba zote zilizofutwa kuwa halali chini ya Katiba mpya.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuainisha na kuzipa uhalali Sheria zitakazoendelea kutumika baada ya Katiba mpya kupitishwa ili kuweka mwendelezo na uhakika wa utawala katika nchi.

**Ibara ya 259: Kuendelea Kutumika Sheria za Nchi**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha Sheria ambazo zitaendelea kutumika katika kipindi cha mpito tangu Katiba Mpya itakapopitishwa na kuanza kutumika. Ibara inataja Sheria zote zilizotungwa zinazohusu mambo ya Muungano, mambo ya Tanzania Bara yasiyo ya Muungano na mambo ya Zanzibar yasiyo ya Muungano zitaendelea kutumika kama sheria halali katika maeneo husika kwa kipindi chote cha mpito.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kuendelea kutumika kwa sheria za nchi zilizotungwa ili kuweka mwendelezo wa sheria hizo na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika kipindi cha mpito cha utekelezaji wa Katiba ya sasa.

### c. Sababu za Mapendekezo

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuna mwendelezo wa sheria na kuzipa uhalali kutumika baada ya Katiba mpya kupitishwa na kuanza kutumika.

## SEHEMU YA TATU

## UTUMISHI WA UMMA

### (a) Serikali ya Jamhuri ya Muungano

**Ibara ya 260: Kuendelea Kuwepo kwa Rais Madarakani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu kwa Rais aliyeko madarakani baada ya Katiba mpya kupitishwa na kuanza kutumika, kuendelea kushika madaraka ya Rais hadi mtu mwingine atakapochaguliwa kushika nafasi ya Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kumtambua Rais aliyepo kuwa anaendelea madarakani mpaka atakapomaliza kipindi chake cha Urais na Rais mwingine kuchaguliwa na kushika madaraka.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.

**Ibara ya 261: Kuendelea Kuwepo kwa Makamu wa Rais Madarakani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu kwa Makamu wa Rais aliyeko madarakani baada ya Katiba Mpya kupitishwa na kuanza kutumika, kushika madaraka ya Makamu wa Rais hadi mtu mwingine atakapochaguliwa kushika nafasi ya Makamu wa Rais.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kutambua kikatiba kuendelea kuwepo kwa Makamu wa Rais hadi Makamu wa Rais mwingine atakapochaguliwa na kushika madaraka hayo. Aidha, ni kurahisisha utekelezaji wa kazi na majukumu ya Makamu wa Rais katika kipindi ambacho Makamu wa Rais mwingine hajachaguliwa.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.

**Ibara ya 262: Kuendelea kwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri.**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa utaratibu kwa Waziri Mkuu aliyepo madarakani baada ya Katiba Mpya kupitishwa kuendelea kushika madaraka ya Waziri Mkuu hadi Rais mpya atakaposhika madaraka. Aidha, Ibara inaweka utaratibu kwa Waziri au Naibu Waziri aliyepo madarakani kuendelea kushika madaraka baada ya Katiba Mpya kupitishwa hadi saa 24 kabla ya Rais mpya kuapishwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuendelea kutambua kikatiba uwepo wa Waziri Mkuu, Waziri na Naibu Waziri katika kipindi cha mpito.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.

***(b) Watumishi wa Umma***

**Ibara ya 263: Kuendelea kwa Watumishi wa Umma**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa utaratibu kwa watumishi wa Umma Serikalini, Bungeni na Mahakamani wataendelea na nafasi zao walizokuwa nazo kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya. Aidha, masharti yote yanayohusu maslahi ya Watumishi wa Umma ya kabla na baada ya kustaafu yatabakia kama yalivyoainishwa kwenye sheria zilizokuwa zinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua kikatiba kuendelea kwa Watumishi wa Umma waliopo katika utumishi wa umma baada ya Katiba Mpya kutungwa na kuanza kutumika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Kuweka masharti yatakayohakikisha haki za Watumishi wa Umma zinalindwa kwa mujibu wa sheria na masharti ya kazi hizo kama ilivyokuwa kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

**Ibara ya 264: Kuendelea kwa Ubunge na Uongozi wa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inatoa utaratibu kwa Wabunge, Uongozi wa Bunge na Viongozi wa Kamati mbalimbali za Bunge kuendelea na nafasi zao hadi uchaguzi Mkuu utakapofanyika wa mwaka 2015. Masharti ya Ibara hii hayatazuia Spika, Naibu Spika, Mbunge, au Kiongozi yeyote wa Kamati ya Bunge kuondolewa katika nafasi zao kwa mujibu wa Katiba ya mwaka 1977.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kutambua kuwepo kwa Uongozi wa Bunge, wabunge na Watumishi wa Bunge mpaka watakapomaliza kipindi chao.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka masharti yatakayohakikisha haki za Uongozi wa Bunge na Wabunge zinalindwa kwa mujibu wa sheria na masharti ya kazi hizo kama ilivyokuwa kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

Kuhakikisha wananchi hawakosi kuwa na wawakilishi wao kwa mujibu wa Katiba ya mwaka 1977.

**Ibara ya 265: Kuvunjwa kwa Bunge**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, inatoa utaratibu wa kuitisha Bunge la Jamhuri ya Muungano lililovunjwa, na ikiwa umuhimu wa kuliitisha utatokea kabla ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu, basi aliyekuwa Mbunge, Spika au Naibu Spika ataendelea na

nafasi yake isipokuwa mtu ambaye hakuwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba ya mwaka 1977 hawezi kuteuliwa.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuwezesha kuitishwa kwa Bunge lililovunjwa wakati Bunge jipya halijaanza kazi pale panapohitajika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo ni kuruhusu kuitishwa kwa Bunge lililovunjwa wakati Bunge jipya halijaanza kazi, kutapelekea Mhimili wa Bunge kuendelea kuwepo na kutekeleza jukumu lolote la dharura litakalojitokeza.

## MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO

### Ibara ya 266: Kuendelea kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka masharti kuwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano zinaendelea kuwepo na kutekeleza majumuku yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya mwaka 1977. Aidha, Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu wataendelea kuwa na Madaraka ya kusikiliza na kutoa hukumu au amri kwa mashauri yaliyofunguliwa au yatakayofunguliwa katika Mahakama hizo kwa mujibu wa Katiba ya mwaka 1977.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba yanayoelekeza Mahakama na Majaji wa Mahakama za Rufani na Mahakama Kuu kuendelea na kazi zao katika kipindi cha mpito.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuwezesha Mahakama kuendelea na kazi za utoaji haki wakati wa kipindi cha mpito na baada ya hapo.

**Ibara ya 267: Kuendelea kwa Mashauri Yaliyopo Mahakamani**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka utaratibu wa kuendelea kusikilizwa mashauri yaliyopo katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu ambayo yalifunguliwa au kukazia hukumu na amri iliyotolewa au itakayotolewa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Hata hivyo, uamuzi wa shauri lolote uliotolewa na Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 hautakatiwa rufani katika Mahakama ya Juu iliyoanzishwa na Katiba Mpya.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba utakaoruhusu kukamilisha kusikilizwa kwa mashauri yaliyofunguliwa kabla ya Katiba Mpya kuanza kutumika.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Mhimili wa Mahakama unaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki kwa wananchi katika kipindi chote cha mpito na baada ya hapo.

Sababu nyingine ni kuzuia kukata rufaa kwenye Mahakama ya Juu kwa mashauri yaliyotolewa uamuzi katika Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ni kuondoa mgongano wa utekelezaji wa kazi za Makahama katika kipindi cha mpito.

## MASHARTI YA MPITO

**Ibara ya 268: Muda wa Mpito**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, inaweka masharti ya muda wa kipindi cha mpito yanayopaswa kufuatwa kwa kipindi cha miaka minne tangu kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba utaratibu wa mchakato wa maandalizi ya Serikali na vyombo vyake, kuingia katika mfumo mpya wa utendaji kulingana na Katiba Mpya.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuifanya Serikali na vyombo vyake iendelee kutekeleza wajibu wake katika kipindi cha mpito cha miaka minne tangu kuanza kutumika kwa Katiba Mpya. Mambo hayo yatatekelezwa hatua kwa hatua kwa mujibu wa mpango utakaopitishwa na Bunge Maalum au kuwekwa na Kamati ya Utekelezaji wa Katiba katika kipindi cha mpito ikionyesha mambo ya muda mfupi, mambo ya muda wa kati na yale yatakayo kamilika wakati wa ukomo wa kipindi cha mpito.

Uzoefu wa nchi nyingine kama vile Kenya, Ghana na Uganda ibara za masharti ya kipindi cha mpito zimewekwa ndani ya Katiba yenyewe badala ya kutungiwa sheria tofauti kama yalivyokuwa mazoea ya Tanzania yaliyofanya watu wengi wasijue uwepo wa sheria hizo zikiwa sehemu ya Katiba.

**Ibara ya 269: Utekelezaji wa Masharti ya Katiba Mpya**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaainisha mambo yatakayopaswa kufanyika na kukamilika katika kipindi cha mpito tangu kuanza kutumika kwa Katiba Mpya. Mambo hayo ni pamoja na kutungwa kwa Katiba ya Tanganyika na kurekebishwa kwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ili kuwiana na masharti ya Katiba Mpya. Aidha, ibara hii ni inaweka utaratibu wa maandalizi ya kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwa kuzingatia masharti ya Katiba Mpya.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la ibara hii ni kuweka katika Katiba mambo yatakayofanyika na kukamilika katika kipindi cha mpito.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha masharti yaliyowekwa na Katiba Mpya yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Sababu nyingine ni kutoa muda wa utekelezaji wa hatua kwa hatua kwa masharti ya Katiba Mpya.

**Ibara ya 270: Kamati ya Kusimamia Muda wa Mpito.**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, inaanzisha Kamati ya Utekelezaji wa Katiba kwa mambo yote yanayopaswa kutekelezwa katika kipindi cha mpito, muundo wake, majukumu yake na masharti ya uteuzi wa Mwenyekiti na Wajumbe, Katibu na Watumishi wa Sekretarieti ya Kamati.

**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Kamati ya Utekelezaji wa Katiba itakayosimamia muda wa mpito na kuanzisha Sekretariati yake.

**c. Sababu za Mapendekezo**

Katika dhana mpya ya utungaji wa Katiba ni muhimu kuwa na Kamati ya utekelezaji wa Katiba nje ya Serikali na nje ya Bunge ili kuhakikisha matwaka ya Katiba na hasa yale yatokanayo na masharti ya muda wa mpito yanatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi.

Uzoefu wa nchi nyingine umeonesha umuhimu wa kuwa na kamati ya utekelezaji wa katiba ili kuhakikisha mabadiliko yaliyoainishwa katika katiba mpya yanatekelezwa kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa.

**Ibara ya 271: Kufutwa kwa Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito**

**a. Maudhui ya Ibara**

Ibara hii ya Rasimu ya Katiba inaweka ukomo kikatiba wa kutumika kwa masharti ya kipindi cha mpito.


**b. Madhumuni na Lengo**

Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya ukomo wa masharti yatokanayo na masharti ya mpito.


**c. Sababu za Mapendekezo**

Sababu za mapendekezo haya ni kuweka ukomo wa kuendelea kutumika kwa masharti ya mpito na kuondoa utata unaoweza kujitokeza ili kuhakikisha kuwa, mambo yote yaliyoainishwa kufanyika katika muda huo yanatekelezwa kama yalivyopangwa na kukamilika kwa wakati.


KIAMBATISHO Na. 1: MUUNDO WA MUUNGANO KATIKA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO YA MWAKA 1977




**KIAMBATISHO Na. 2: MUUNDO WA MUUNGANO KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO**




KIAMBATISHO Na. 3: USIMAMIZI NA URATIBU WA MAMBO YA MUUNGANO NA YASIYO YA MUUNGANO KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO




**KIAMBATISHO Na. 4: MUUNDO WA VYOMBO VYA KUTUNGA SHERIA KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI UA MUUNGANO WA TANZANIA**




**KIAMBATISHO Na. 5: MFUMO WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MUJIBU WA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO YA MWAKA 1997 NA KATIBA YA ZANZIBAR YA MWAKA 1984**



KIAMBATISHO Na. 6: MUUNDO WA VYOMBO VYA UTOAJI HAKI KATIKA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**KIAMBATISHO NA. 7: UTATUZI WA MIGOGORO KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO NA NCHI WASHIRIKA NA KATI YA NCHI ZA WASHIRIKA ZENYEWE**



## KIAMBATISHO NA.8: MISINGI YA UTENDAJI YA MUUNGANO WA SERIKALI TATU

Muundo wa Serikali Tatu umejengwa katika Misingi ya Utendaji (Principles) ifuatayo:

(a) Muungano wa Hiari (Voluntary Union);

(b) ushirikiano ( Co-operation);

(c) uratibu (Co-ordination);

(d) Mshikamano (Solidarity); na

(e) subsidiarity.

### 1.0 Muungano wa Hiari (Voluntary Union)

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Msingi wa Muungano huu ni Makubaliano ya Muungano (Articles of Union) ya mwaka 1964 yaliyofikiwa baina ya mataifa haya mawili. Chini ya makubaliano hayo, mataifa hayo yalikubaliana kwa hiari kuachia baadhi ya mamlaka na kuyapeleka mamlaka hayo katika Serikali ya Muungano. Uhiari huu wa kukubali kuungana kwa mataifa haya mawili ni moja ya misingi ya utekelezaji wa muundo wa Muungano unaopendekezwa wa Serikali Tatu. Ibara ya 1(3) ya Rasimu ya Katiba inapendekeza pamoja na mambo mengine, Hati ya Muungano iwe ni msingi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 1.1 Ushirikiano (Co-operation)

Msingi mwingine wa utendaji katika muundo wa Serikali Tatu ni Ushirikiano. Chini ya msingi huu, Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika zitakuwa na ushirikiano baina yao katika shughuli zote za utendaji na uendeshaji wa nchi ili mradi ushirikiano huo haukiuki Katiba. Ibara ya 65(1) inapendekeza kuwa Nchi Mshirika iweze kuomba ushirikiano kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kufanikisha uhusiano wake wa kikanda au kimataifa. Aidha, Ibara ya 66 inapendekeza masharti kuhusu ushirikiano kati ya Nchi Washirika zenyewe na baina ya Nchi hizo na Serikali ya Muungano kwa lengo la kukuza na kulinda maslahi ya Taifa na kukuza maendeleo ya wananchi.

### 1.2 Uratibu (Coordination)

Katika mfumo wa Serikali Tatu, uratibu wa uhusiano baina ya Serikali hizo ni moja ya misingi muhimu. Ibara ya 67 inapendekeza kuwepo kwa Waziri Mkaazi atakayeteuliwa na

kila Nchi Mshirika atakayefanya kazi akiwa Makao Makuu ya Serikali ya Muungano. Moja ya majukumu ya msingi ya Waziri Mkaazi ni kuratibu uhusiano baina ya Serikali yake na Serikali nyingine ya Nchi Mshirika na kati ya Serikali yake na Serikali ya Muungano. Aidha, Ibara ya 109 inapendekeza kuanzishwa kwa Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais. Kuwepo kwa uratibu kutaimarisha uhusiano wa kiutendaji baina ya Serikali zinazopendekezwa na hivyo kuimarisha Muungano.

### 1.3 Mshikamano (Solidarity)

Mshikamano (Solidarity) ni moja ya misingi muhimu ya utendaji katika mfumo wa Shirikisho. Msingi huu umezingatiwa katika Rasimu inayopendekezwa ili kuhakikisha kuwa Serikali zote tatu zinashikamana na kusaidiana katika kila hali inayoweza kujitokeza. Mathalani, Ibara ya 62(3) inapendekeza kuipa Serikali ya Muungano, kwa makubalino na masharti maalum na Serikali ya Nchi Mshirika, madaraka ya kutekeleza jambo lolote lililo chini ya mamlaka ya Serikali ya Nchi Mshirika. Aidha, Ibara ya 65 na 66 zinapendekeza kuwepo kwa ushirikiano baina ya Serikali za Nchi washirika na kati ya Serikali hizo na Serikali ya Muungano. Msingi huu ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano wananufaika kwa usawa na mshikamano baina ya Nchi Washirika.

### 1.3 Subsidiarity

Msingi wa ***subsidiarity*** unakusudia kuweka utaratibu wa mamlaka za chini kutekeleza majukumu yaliyo ndani ya uwezo wake ikiwa mamlaka hizo zina uwezo wa kutekeleza majukumu hayo kwa ukamilifu. Msingi huu wa ***subsidiarity*** unaruhusu mamlaka ya juu kutekeleza jambo ambalo kwa kawaida hutekelezwa na mamlaka ya chini iwapo mamlaka ya juu ina uwezo wa kutekeleza jambo husika kwa ufanisi au vinginevyo. Ibara ya 65 na 66 zimeweka msingi kwamba, ingawa Serikali ya Muungano itakuwa na mamlaka ya kushughulikia Mambo ya Muungano, Serikali hiyo, kwa ridhaa ya Serikali ya Nchi Mshirika, itakuwa na mamlaka ya kushughulikia masuala yasiyo ya Muungano katika Nchi Mshirika. Msingi huu utasaidia kuimarisha utendaji katika muundo wa Serikali Tatu unaopendekezwa.